ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Sita – Tarehe 18 Disemba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani ya kuomba ridhaa kwa ajili ya kuwasilisha Mswada Binafsi ya Sheria ya Utawala wa Baraza. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 37

Operesheni ya Wahamiaji Haramu Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha mwezi Septemba na Oktoba, 2013, imekuwa ikiendesha operesheni kabambe ya kutambua pamoja na kuwarejesha makwao wahamiaji haramu katika nchi yetu.

(a) Je, zoezi hili lilifika huku Zanzibar.

(b) Kama lilifika ni wahamiaji wangapi haramu walitambuliwa na hatimae kurejeshwa makwao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 37 lenye kifungu (a) na (b) naomba nitangulize maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha mwezi wa Septemba na Oktoba, 2013 iliendesha Operesheni kabambe ya kuwatambua na kuwarejesha makwao wahamiaji haramu kutoka katika nchi yetu, iliyojulikana kwa jina la "Operesheni Kimbunga 2013".

Baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (a) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, Operesheni Kimbunga 2013 haikufika huku Zanzibar wala Mikoa mengine ya Tanzania Bara zaidi ya Kagera, Kigoma na Geita.

b) Mhe. Naibu Spika, licha ya operesheni hiyo kutofika huku Zanzibar, wakati wa kipindi cha mwezi wa Septemba na Oktoba 2013, Idara ya Uhamiaji Zanzibar iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku, ambapo iliweza kuwakamata watuhumiwa wa uhamiaji haramu kutoka nchi zifuatazo:-

   Iran 11, Kenya 12, China 02, South Afrika 03, Sierra Leone 03, Palestina 06, Uganda 09, India 01, Thailand 01, Burundi 02, Holand (Dutch) 01 na Zambia 01.

   Mhe. Naibu Spika, zoezi hili litaendelea mpaka pale tutakapowadhibiti wahamiaji haramu hapa Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kueleza kuwa Operesheni Kimbunga haikufanyika Zanzibar, lakini wafanyakazi wengi wa mahoteli hasa wenye asili ya Tanzania Bara walikamatwa na kuwekwa katika Kituo Kikubwa cha Zanzibar cha Mwembemadema, kwa kushindwa kuonesha vitambulisho na wengine kuachiwa usiku mkubwa.

Je, serikali haioni kwamba haikuwafanyia haki na ukizingatia wanayo haki ya kufanyakazi pande zote mbili za Muungano na kwa nini wasiwafuatilie waajiri wao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie taratibu na akae karibu na *speaker*.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali lako na uinamie hiyo *speaker* vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, kueleza kwamba Operasheni Kimbunga haikufanyika Zanzibar, lakini wafanyakazi wengi wenye asili ya Tanzania Bara walikamatwa na kufikishwa katika Kituo cha Polisi cha Mwembemadema na wengi kuachiwa kwa dhamana kwa kushindwa kuonesha kitambulisho cha kupiga kura au Kitambulisho cha Mzanzibari.

Je, kwa nini serikali iliamua kuwaweka ndani badala ya kuwafuatilia kupitia kwa muajiri wao, kwa sababu kitendo cha kuwakamata na kuwaweka ndani na kuwaachia usiku mkubwa, serikali haioni kuwa ni unyanyasaji dhidi ya raia wake wakati Watanzania Bara wanayo haki ya kufanya kazi popote ndani ya pande mbili hizi za Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza wananchi kutoka Tanzania Bara ni Watanzania kama Watanzania wengine wanayo haki kamili ya kuishi hapa Zanzibar bila ya kubughudhiwa. Lakini inapotokezea kwamba kuna zoezi la kuwatafuta wahamiaji haramu wakati mwengine kwa bahati mbaya sana inawezekana sio tu wakakamatwa wananchi wenye asili ya Tanzania Bara lakini hata Wazanzibari wenyewe hutokezea kukamatwa, kwa sababu ni utaratibu wa kawaida katika kufanya zoezi la namna hii.

Kwa hivyo, mara baada ya kutoa vielelezo vinavyohakikisha kwamba wewe ni Mtanzania au Mzanzibari, basi hapana shaka yoyote na wala si vyema hata kidogo kuwanyanyasa raia ama kuwapa tabu watu ambao hawahusiki na jambo hilo.

Ninaupokea ushauri wa Mhe. Mjumbe, ili tuwasiliane na Uhamiaji kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tuone namna gani tunaliendesha zoezi hilo ili isitokee tena athari kwa baadhi ya wananchi ambao hawakupaswa kupewa usumbufu, tunaahidi kufanya vizuri zaidi kwa ajili ya wananchi wote katika nchi yao, ili waweze kukaa kwa furaha na salama na wale wahamiaji haramu waweze kudhibitiwa wasiendelee kuwepo nchini. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali yetu ina ulinzi kamili hapa Zanzibar. Je, Mhe. Waziri hawa wahamiaji haramu ambao umewataja na wakarejeshwa kwao wahamiaji hawa waliingia vipi nchini wakati serikali yetu inao ulinzi kamili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa nini tunapata wahamiaji haramu. Wakati mwengine inawezekana wakaingia kwa njia za kihalali kabisa kwa kuwa na *Passport* inayowaruhusu kuingia, lakini wakamaliza muda wao waliopewa ruhusa ya kukaa.

Vile vile, inawezekana kutokana na utaratibu wetu maboti ya wavuvi au kupita hata bandarini na kujifanya Mtanzania. Kwa hivyo, zipo mbinu nyingi za watu ambao wanaweza kujipenyeza na wakaingia kama wahamiaji haramu.

Lakini suala zima ni utaratibu mzuri tunaoendelea nao wa kuhakikisha kwamba tunafanya zoezi la kuwatafuta wahamiaji haramu waliopo na jambo la msingi ni wananchi kutoa taarifa pale ambapo wanaona kuna mtu ambae si raia wa nchi hii, na wala hana haki ya kuwepo nchini. Kutokana na hali hiyo, ni vyema tukashirikiana kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa salama na wananchi wetu wale ambao wanaruhusiwa kwa mujibu wa sheria wanaishi kwa salama.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mhe. Waziri. Kwa kweli nataka kujua katika ukamataji huo wa wale ambao amesema wamerejeshwa katika zoezi lililofanywa na Idara ya Uhamiaji, hawa watu kwa sababu wamekaa katika nchi yetu walikuwa wanapaswa kulipia *Visa*, sasa sijui kuna makusanyo yoyote ambayo yaliweza kukusanywa au kuna faini yoyote ambayo wametozwa na ikiwa ipo ni kiasi gani. Vile vile, nataka kujua zile gharama za kuwarejesha, je zinagharamiwa na nani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, hawa wanapokamatwa inabidi kufuata utaratibu wa kisheria uliopo na lazima wapelekwe mahakamani na baadae ndipo panapotolewa uamuzi.

Kwa hivyo, watu hawa waliokamatwa wametozwa faini na baada ya kutozwa faini ndio wakaamuliwa wasafirishwe nje ya nchi. Kwa maana hiyo, zipo taratibu za namna ya kuwasafirisha watu hao na hupaswa nchi husika kulipia gharama za hawa wananchi wao ambao wapo hapa. Kwa hivyo, kuna taratibu za kidiplomasia zinatumika katika kuwasafirisha watu hao, ili kuhakikisha kuwa nchi yetu isipate gharama.

UTARATIBU

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, natumia Kanuni ya 37 kifungu cha 1 ambapo swali langu nimemuuliza Mhe. Waziri, kwamba nilikuwa nataka kujua ni kiasi gani ambacho kimekusanywa kutokana na faini ambazo wametozwa hawa ambao ametutajia na wala hakuweza kunijibu, isipokuwa amesema tu wamepelekwa mahakamani na wametozwa faini, na mimi nilikuwa nataka kujua kiwango cha fedha zilizokusanywa, naomba anijibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba nieleze kwamba lazima tuwe na utaratibu wa kawaida wa kutumia akili ya kibinadamu kwamba mtu ameshakuwa muhamiaji haramu

halafu atakuwaje na mapato ya Visa katika nchi, kwa sababu huyo ni muhamiaji haramu ameshakwepa kila kitu. *(Makofi)*

Nam. 1

Adhabu Ndogo kwa Waharibifu wa Mazingira

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Mwaka 2011 ulipokuwa ukijibu swali langu la nyongeza uliainisha adhabu zilizotolewa kwa watu ambao walitiwa hatiani kwa uharibifu wa mazingira kwa kuchimba mchanga na kusafirisha kinyume na sheria kuwa ni kulipa faini kati ya shilingi 300,000/- na shilingi 150,000/- na wengine kusamehewa kwa sababu magari yao yaliharibika.

(a) Je, Mh. Waziri, huoni kitendo cha kuwasamehe waharibifu wa mazingira ni kuongeza tatizo la uharibifu na uchafuzi wa mazingira hayo.

(b) Je, Mhe. Waziri, huoni adhabu ya kulipa faini hasa kwa kiwango kidogo kama hiki hakiwaogopeshi waharibifu wa mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 1 lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, usimamizi wa matumizi ya maliasili zisizorejesheka zikiwemo masuala ya kutoa vibali vya kuuza mchanga, mawe, kokoto, kifusi na udongo yanasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.Vile vile, matumizi ya maliasili hizo yanasimamiwa pia chini ya Sheria Nam. 2 ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 1996. Sheria hii imeipa uwezo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kusimamia matumizi ya maliasili hizo kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi kuhusiana na matumizi ya maliasili zisizorejesheka. Sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa kuzingatia vigezo na mazingira halisi yanayojitokeza tunapofanya kazi na jamii, viwango mbali mbali vya faini vimekuwa vikitumika na wakati mwengine

hutoa onyo kwa wahusika kulingana na ushahidi wa kosa lenyewe. Viwango hivyo vinatokana na ukubwa wa gari, kuanzia tani moja hadi tani kumi. Hali hiyo imejitokeza kwa sababu hakukuwa na kanuni yenye kuonesha viwango mbali mbali kutokana na uzito wa kosa.

b) Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kulipa faini kwa kiwango kidogo kunachangia waharibifu wa mazingira kutokuogopa adhabu hiyo na pengine kuzidi kuendelea kuyaharibu mazingira yetu, kwa vile wanaamini kwamba wanaweza kumudu kulipa faini hiyo bila ya matatizo yoyote. Tatizo hili ofisi yangu imeshaliona lakini lakini ni kutokana na sheria hii kwa muda mrefu ilikuwa ikitekelezwa bila ya kuwepo kanuni zake.

Hali hii ilipelekea kuwepo na ugumu wa kiasi fulani katika utekelezaji wake, kwani sheria hii ilikuwa haikufafanua masuala ya msingi ya kisheria ikiwa ni pamoja na uzito wa kosa lenyewe pamoja na kiwango cha adhabu ambacho mtuhumiwa alipaswa kupewa.

Kwa mfano sheria haikutofautisha baina ya mshitakiwa aliechimba na kusafirisha mchanga kwa kutumia gari kubwa au ndogo na adhabu yake iwe vipi. Hapo kabla viwango vya adhabu ya makosa haya ilikuwa ni moja tu bila ya kuzingatia ukubwa wa kosa lenyewe na hivyo kisheria lilionekana kuwa ni mapungufu ambayo yalipaswa kurekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, tatizo hili baada ya kuonekana, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili tulifanya kwa makusudi kuipitia sheria hii, pia kutayarisha Kanuni za Matumizi ya Maliasili zisizorejesheka ya mwaka 2013. Kanuni hizi zimetoa ufafanuzi wa kutosha juu ya aina ya makosa na adhabu zinazopaswa kutumika kwa mtu ambae atapatikana na hatia ya uchimbaji na usafirishaji wa maliasili hizo, ukiwemo mchanga.

Kanuni hizo zimeshaanza kutumika na matokeo yake ni kwamba adhabu hizo zinazotolewa hivi sasa, ofisi yetu inaamini kwamba zinaweza kwa kiwango kikubwa kupunguza matukio ya uharibifu wa mazingira yetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, sheria ambayo Mhe. Waziri, ameiejelza inalenga kudhibiti mazingira na kulinda rasilimali za nchi. Kwa hivyo, naomba kujua ni kwa kiwango gani kwa tathmini ya wizara, wananchi wanaharibu mazingira, na kwa kiwango gani miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani wa maendeleo au makampuni ya nje.

b) Mara kadhaa Mhe. Rais wa Zanzibar, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wamefanya ziara pamoja na Mhe. Waziri kuangalia jinsi makampuni mbali mbali yanayoharibu mazingira katika maeneo ya Mwambe, ambapo kutoka mwaka 1990 hadi leo tayari tumebahatika kupata visima zaidi ya kumi kutokana na uchimbaji wa kifusi. *(Makofi)*

Kwa nini makampuni ya nje serikali huyafumbia macho na huku wananchi wakiteketea na wakati athari ya kimazingira ikitokezea watakaoathirika ni wananchi wa Mwambe. Kutokana na hali hiyo, serikali inatuambia bora wananchi wa nje kuliko wa ndani. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, katika swali lake la kwanza Mhe. Mwakilishi ametaka kujua ni kwa kiasi gani uharibifu unaosababishwa na *contractors* wetu wanaotekeleza shughuli za maendeleo pia na wananchi.

Kwa hakika hakuna tathmini ambayo kwa sasa ambayo naweza kumpa kwa uhakika hasa na nani wameharibu zaidi. Lakini kwa ujumla, wote wawili aliowataja wanahusika katika uharibifu wa mazingira.

Vile vile, katika swali lake la pili ni kweli ziara kadhaa zimefanywa na viongozi wakubwa na mimi nikiwemo katika ziara hizo kwa ajili ya kuangalia uharibifu wa mazingira ndani ya maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala ambalo yeye mwenyewe Mhe. Mwakilishi amelizungumzia kuhusu Mwambe. Mwambe katika Jimbo la Kiwani kulikuwa na matatizo ya uchimbaji mchanga ambayo nayo yameacha mashimo, pia kulikuwa na suala la wananchi ambao wanakata matofali kwa ajili ya shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mjumb, kwamba Kanuni ambazo tumeziweka sasa zinalenga katika kuwazuia watu wote au kampuni ambazo zitakuja kufanya shughuli za maendeleo na kuhakikisha kwamba maeneo ambayo watachimba mchanga au watafanya shughuli nyengine, wanayarudisha katika hali yake ya uhalisia angalau kwa kiasi fulani.

Kwa hivyo, katika Kanuni hiyo ya mwaka 2013 kipo kifungu kinaelezea ni jinsi gani ama hatua itakayochukuliwa, faini na hata kifungo kwa mtu ambae ataharibu mazingira na kutokuweza kuyarudisha katika hali yake ya uhalisia. Serikali inathamini sana wananchi wa nchi hii na ndio *priority* yake kwanza kuliko wageni.

Nam. 58

Kutelekezwa kwa Wajasiri Amali wa "Sunday Market"

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza:-

Kwa kuwa kwa makusudi ya serikali iliamua kuanzisha Soko la Jumapili (*Sunday Market*) ili kuwaendeleza wajasiriamali hasa wanawake hapo Michenzani, na kwa kuwa serikali kwa muda mrefu imeacha kuwapa huduma muhimu wajasiriamali hao, kama vile mashamiana, meza na viti na kuwaacha wakiungua na jua.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea kukatishwa huduma hizo wakati wenyewe pia walikuwa wakizichangia.

(b) Je, serikali haioni kuwa kuna haja ya kuendelea kuwasaidia wajasiriamali hao, ili waweze kujiendeleza na kujiajiri.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 58 lenye kifungu (a) na (b), lakini kabla ya kutoa majibu naomba nitoe maelezo mafupi kwa ajili ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Soko la Jumapili limeanzishwa Januari mwaka 2012 ikiwa ni sehemu ya Sherehe za Mapinduzi matukufu ya Zanzibar (kutimiza mwaka 49). Soko hili lilizinduliwa rasmi na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi. Madhumuni ya soko hilo ni kuwasaidia wajasiriamali kupata eneo la kuonyesha bidhaa zao ili kupata soko.

a) Mhe. Naibu Spika, wakati lilipoanza soko hili, mashamiana, viti na meza vilikuwa ni vya kukodi na baadae muda si mrefu iliyokuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi, Kiuchumi na Ushirika ilipata vifaa hivyo na vikawa vinatolewa kwa wajasiriamali bila malipo yoyote. Wizara ilikubaliana na wajasiriamali hao kwa jukumu la kubeba vifaa hivyo kutoka Makao Makuu ya Wizara

vinakohifadhiwa na kuvirejesha baada ya kufunga biashara zao vitakuwa ni vyao.

b) Mhe. Naibu Spika, kutokana na gharama za kusafirisha vifaa hivyo, Wajasiriamali walikuwa wakichangia kila siku ya Jumapili, ili waweze kumlipa mwenye gari pamoja na vijana waliokuwa wakiwafungia mashamiana. Fedha hizo zilikuwa zikihifadhiwa na wao wenyewe kupitia mshika fedha wao ambae ni Mjumbe wa Kamati ya Wajasiriamali ya usimamizi wa Soko la Jumapili.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Kutokana na Unguja na Pemba kuwa kuna Soko la Jumalpili, je, wizara yake inaunganisha vipi wajasiliamali hao ili waweze kubadilisha uzoefu kwa faida na maendeleo yao.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, ni kweli Pemba liko Soko la Jumapili Chake Chake na Unguja pia Michenzani. Wajasiriamali hawa tunawaunganisha wakati tunapowapa mafunzo kwa mfano ya pamoja. Kwa hivyo, wajasiriamali wa Soko la Chake Chake na waliopo hapa Unguja wanajuana vizuri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza.

a) Haoni Mhe. Waziri, kwamba hivi sasa ipo haja ya kuwatafutia eneo kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa ajili ya kuwapa eneo la uhakika.

b) Mhe. Waziri, amesema kwamba tayari ameshawapa mafunzo hawa wajasiriamali. Lakini kutokana na hali ilivyo ya umasikini je, na mifuko ya kuendesha biashara hiyo wizara yake imewatafutia.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba niungane naye kuhusu ushauri wake kwamba kuna haja ya kukaa pamoja mimi na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa ajili ya kuwatafutia pahala pa uhakika, na hilo nakubaliana naye. *(Makofi)*

Vile vile, kuhusu swali lake la pili, basi tutakapokuwa tayari tutawawezesha wenzetu, ili biashara zao ziendelee kukua vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, niulize swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kumbukumbu za Masoko ya Jumapili kwa akinamama zinaoneshwa kwamba zilianza tangu wakati wa Dkt. Salmin Amour Juma na Soko lilianzishwa katika eneo la Bwawani, mbele ya Msikiti Mablue.

Kwa hivyo, nataka kujua sababu za kufeli kwa soko lile lililoanzishwa wakati wa Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Salmin Amour Juma. Vile vile na hali iliyoanzia katika Soko lililoanzishwa la Michenzani. Je, Mhe. Waziri, haoni kwamba wizara yake haijawa makini katika kusimamia masuala ya kuwasaidia akinamama katika kuanzisha masoko.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba lilipoanzishwa Soko hili la Jumapili liliekwa kule Msikiti Mablue. Lakini sasa kwa mara hii ya pili tumeweka Michenzani, pale ni *Center* . Kwa hivyo, tumeona ni rahisi tuweke pale.

Kuhusu swali lake jengine kidogo naomba arudie.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali la (b).

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali halisi ya Masoko yetu ya Jumapili tulipoanza Bwawani Mablue jinsi lilivyokwenda na matokeo yake kutokomea kabisa, na hali halisi inayoonekana Michenzani kwamba watu walianza kwenye maturubali na sasa watu wapo chini ya mti. Haoni kwamba wizara yake bado haijajiandaa katika suala zima la kuwasaidia akinamama katika haya masuala ya masoko.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi, kwamba asiwe na wasi wasi na pale tulipowaweka wajasiriamali bado biashara zao zinakwenda vizuri na wao wenyewe hawajatoa malalamiko yoyote. Lakini kukitokezea tatizo lolote tunaweza tukawahamisha tukawapeleka sehemu nyengine.

Nam. 35
Kukosekana kwa Mashine ya Kuchunguza Mizigo
Uwanja wa Ndege Pemba

Mwanaidi Kassim Mussa Kny/ Mhe. Shadya Moh'd Suleiman – Aliuliza:-

Serikali inajitahidi kuimarisha miundombinu ya usafiri kama vile viwanja vya ndege, lakini jambo la kusikitisha sana ni kuona hadi hii leo kiwanja cha

ndege cha Pemba hakuna mashine ya kuchunguzia mizigo ya abiria na kuwapa shida wasafiri kwani nguo zao kwenye mizigo hutolewa nje moja baada nyengine ambapo haileti picha nzuri kwa wasafiri hao.

Je, serikali inalichukuliaje suala hili na kutafuta njia za haraka kukipatia kiwanja cha Pemba mashine hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba niombe radhi kama sauti yangu haikutoka vizuri, kwa sababu jana nilikesha zikirini Ukongoroni.

Mhe. Naibu Spika, kama sote tunavyofahamu kwamba suala la usafiri hasa wa ndege ni usafiri unaohitaji utaratibu na umakini mkubwa hasa kwa kuzingatia matukio mbali mbali yaliyokwisha kujitokeza Duniani.

Aidha usafiri huo wa ndege kwa mujibu wa taratibu zake huwa mara nyingi huepushwa na kuwakinga abiria au wasafiri na jambo lolote linaloweza kuwajenga hofu hata kama kwa nadharia. Katika utaratibu huo ndio kumeandaliwa utaratibu maalum wa ukaguzi wa watumiaji wa uwanja wa ndege pamoja na ukaguzi wa wasafiri na mizigo yao.
Kwa upande wa mizigo ni busara kutumia mashine ya kuweza kutambua kilichomo ndani ya mkoba huo au makasha, kisha pale unapokuwa na shaka hutakiwa muhusika kutoa maelezo ya kusaidia kuutambua ukweli wa jambo lenyewe. Hata hivyo ukaguzi kama huu hufanyika kwa muhusika mwenyewe ingawa dunia nzima utamaduni uliozoeleka na kuaminika zaidi ni ule mtindo wa kupapasa kwa madhumuni ya kuhakiki kwa njia ya mikono na uono wa macho.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali umuhimu huu wa mashine za kuchunguzia mizigo na kutambua vifaa vya vitu hatarishi kwa usalama wa wasafiri wetu ni muhimu. Katika kufanikisha hilo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) katika bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika mwaka wa 2013/2014 tayari suala hilo limezingatiwa na hivyo vifaa vitanunuliwa ili viweze kusaidia katika utoaji wa huduma hizo muhimu na za kiusalama.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuomba Mhe. Mjumbe kwamba naomba sote tukubaliane kwamba umuhimu wa kuzingatia usalama wa wasafiri wetu

kwamba kiwe ni kipaumbele cha kwanza na kama kuna usumbufu wa aina yoyote katika mnasaba huo tuvumiliane hadi pale vifaa hivyo husika vitakapopatikana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ili nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, na pamoja na kusema kwamba katika kipindi cha Bajeti ya mwaka 2013/2014 wamelizingatia suala la kununua mashine ya kuchunguzia mizigo ili kuondoa huo usumbufu. Sasa napenda nimuulize mashine hizo nategemea kwamba zinakwenda kwa umeme na kiwanja chetu cha Ndege hivi karibuni kulikuwa na tatizo la umeme kumalizika.

a) Je, haoni kwamba utaratibu huo si mzuri na kufanya hivyo ni aibu kwa kiwanja chetu cha Pemba.

b) Je, hawaoni kuwa na umeme wa kununua na kutumika hadi kumalizika ni aibu kwa Kiwanja chetu. Ni lini aibu hiyo itaondoka.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru, Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, lakini kwa sababu suala hili lilitokezea na mimi nikapata taarifa mapema, kwa hivyo niliweza kulifuatilia na nikajua chanzo chake.

a) Mhe. Naibu Spika, kila Wizara na Idara inakuwa ina bajeti maalum kwa ajili ya matumizi. Bahati mbaya hivi karibuni umeme ulipanda bei, kwa hivyo bajeti ilikuwa haijafanyiwa marekebisho ya haraka, ikatokezea siku moja tu, katika masaa 4 ikawa umeme haupo. Lakini jambo hilo limefanyiwa marekebisho na halitoweza kutokezea tena isipokuwa pale umeme utakapokatika kwa njia nyenginezo. Kwa hivyo, hiyo tunaomba radhi kwani haikuwa ni jambo la kukusudia.

b) Suala la kwanza lililojibiwa mimi nimefuatilia kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri tayari mpango wa bajeti unaandaliwa kupata mashine katika mwaka huu wa bajeti. Hivyo, uchambuliwaji wa nguo utapungua sana kwani pia kuna malalamiko kwamba wanapoingiza mikono kwa kupekuwa vitu, kunakuwa na viwembe na mambo mengine. Lakini sisi tutawapa *claves* nzito ili kuweza kupunguza athari wanazopata ili wasisasambue nguo kwa njia nyengine.

Kwa hivyo, tunawaomba radhi sana wananchi wote wanaosafiri, na tutajitahidi kupekuwa kwa njia iliyokuwa bora zaidi, na wakati huo huo tunafuatilia upatikanaji wa mashine haraka iwezekanavyo. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kiwanja cha Ndege cha Pemba ni kiwanja kinachomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wala sio Kampuni ya mtu binafsi. Na kwa kuwa suala la kukatika umeme pale na hatimae joto kusumbua wananchi pamoja na wageni wetu katika nchi hii halimuaibishi Mhe. Waziri, na watendaji wake tu, bali inaliaibisha Taifa hili la Zanzibar ambalo lilipata uhuru wake kwa kupitia Mapinguzi mwaka 1964;

a) Mhe. Waziri, haoni kwamba kwa sababu juzi alinunua umeme Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akatia. Je, sikunyengine akija akinunua Mzungu akitia umeme, mgeni wa nchi hii haitokua aibu katika serikali yetu ambayo tumeipata kwa Mapinduzi.

b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika suala hili la msingi kwamba mpango upo wa kununua mashine. Kwa kuwa hadi leo hii bado tunapita pale na kuanza kupapaswa papaswa pale unapotiliwa shaka. Tena wakati mwengine unapapaswa na watoto wadogo (wasichana) kabisa, na sisi ni watu wazima. Mhe. Waziri, haoni kwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na ibara ya 15 ya Katiba ya Zanzibar inayozungumzia faragha ya mtu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama maelezo aliyotoa Mhe. Waziri kwamba kuna tukio la kukatika kwa umeme na ni kweli kwamba kulikuwa na makosa hayo. Kama alivyoeleza Mhe. Waziri tumeomba radhi kwa tukio hilo kutokana na makosa ya watendaji wetu pamoja na utaratibu wa masuala ya utawala na upatikanaji wa fedha kuweza kulipia huduma hiyo.

a) Mhe. Naibu Spika, kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub, alinunua umeme huo, mimi niseme ndio uzalendo wenyewe. Na kama kuna mapungufu si hapo tu na kwengine tunahitaji msaada wake kama kutakuwa kuna mapungufu katika utendaji wetu wa serikali, yeye ni Mzanzibari na yeye ni Mtanzania, anawajibika na analazimika kuzisaidia serikali zake. Kwa hiyo, kama ametoa tunaendelea kumpongeza, kwa uzalendo wake mzuri kwa kufanya kitendo chema. Lakini sisi kama wajibu wetu tutahakikisha makosa kama haya hayatokei tena.

b) Mhe. Naibu Spika, naomba kumkumbusha Mhe. Mwakilishi kwamba utaratibu wa kupapaswa katika viwanja vya ndege ni utaratibu wa kimataifa. Hakuna uwanja wowote duniani ambao utakwenda *physical* usipapaswe, lazima upapaswe, utapita kwenye mashine, utaangaliwa lakini ni lazima usimame uangaliwe. Kama kuna Uwanja wowote wa Ndege duniani anaoufahamu yeye ambapo mtu unapita kwenye mashine hufanyiwi ukaguzi wa mikono atueleze. Sisi tunachotambua kwamba kuna upungufu katika mashine, tutahangaika kutafuta mashine hizo lakini utaratibu wa kuhakiki mtu kwa mikono utaendelea.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, hichi chombo ni chombo kikubwa sana, na nashukuru Mhe. Naibu Spika, Ofisi yako imekuwa makini katika kutunga Kanuni zinazosimamia uendeshaji wa chombo hiki madhubuti cha wananchi. Moja kati ya kanuni zetu zinatilia sana umuhimu wa kuwa na uhakika na unachokisema.

Kwa kuwa Waheshimiwa Wawakilishi wameshasafiri katika nchi mbali mbali mbali, Je, anaweza kutoa uthibitisho juu ya kauli yake kwamba katika kila nchi unayopita unapapaswa.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa mimi natoa ushahidi juzi tumekwenda Kwalalumpa (Malaysia) mimi, Mhe. Spika na Mwenyekiti, tumefanyiwa utaratibu huo, unapita kwenye machine halafu mnanyoosha mikono unaangaliwa sio kupapaswa. Maana kupapaswa ni lugha nyengine na kuangaliwa ni lugha nyengine. Kwa hivyo, lugha ya kupapaswa haipo lakini kuangaliwa ipo.

Nam. 40

Matengenezo Gati ya Wete na Wesha

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu gati ya Wete imekuwa katika hali mbaya kutumika kwa shughuli za usafiri wa vyombo vya baharini. Sambamba na gati hiyo ya Wesha nayo ilifanyiwa matengenezo makubwa katika miaka michache iliyopita.

(a) Ni lini serikali itaifanyia matengenezo stahiki gati ya Wete ili vyombo vya usafiri baharini viweze kuitumia muda wowote.

(b) Baada ya matengenezo ya gati ya Wesha, kuna mpango wowote wa kuimarisha gati hiyo ili iweze kutoa huduma kwa vyombo mbali mbali vya usafiri na mizigo kwa muda wa masaa 24.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Shirika la Bandari iliifanyia matengenezo makubwa gati ya Wete mnamo mwaka 2001 kwa kuwa gati hiyo ilikuwa imeporomoka kabisa. Baada ya matengenezo hayo katika jitihada za kuiendeleza gati hiyo Shirika la Bandari liliifanyia matengenezo mengine (mwaka 2004) kwa kuirefusha kuelekea kina kirefu cha maji kuwezesha vyombo vikubwa kufunga gati.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya, baada ya kazi hiyo hivi sasa kumejitokeza tatizo jengine la kudidimia, sehemu ya mbele ya gati ambapo Shirika limeanza kufanya uchunguzi ili kujua sababu na chanzo cha tatizo hilo na kutafuta ufumbuzi wake.

Mhe. Naibu Spika, wizara yetu kupitia Shirika la bandari ina mpango wa kuirefusha zaidi gati hiyo kufikia kina kikubwa zaidi ili vyombo viweze kuitumia muda wowote, kazi hiyo itafanywa baada ya kukamilisha marekebisho yaliyotajwa na Shirika la Bandari kuweza kutenga bajet mahsusi kukamilisha kazi hiyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Shirika la Bandari, ina mpango wa kuirefusha gati ya Wesha ili ifikie kina kikubwa cha maji na kuwezesha vyombo mbali mbali kuegesha hapo wakati wowote. Kama tunavyotambua kwamba katika maeneo ya gati ile ya Wesha kumezungurukwa na mikoko kwa upande mmoja. Hivyo, maelekezo tuliyoyapata kutoka Idara husika tumelazimika kufanya uchunguzi wa athari za kimazingira kabla ya utekelezaji wa mradi wenyewe. Kwa hatua hii hivi sasa tayari Shirika la Bandari limeshatangaza zabuni za kazi hiyo. Hivi sasa mchakato wakumpata mshauri unaendelea ili kuweza kufanya tathmini ya kimazingira baadae kuweza kwenda katika utaratibu wa kuirefusha gati hiyo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri na ya kutia tamaa aliyotoa. Hata hivyo nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) , (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwa sababu gati ya Wete ilifanyiwa matengenezo makubwa mwaka 2001 na mwaka 2004. Kwa kuwa imeonekana pia kuna sehemu imedidimia sasa imo katika njia za kitaalamu ili kufanyiwa matengenezo, kabla ya matengenezo makubwa yatakayofuata hapo baadaye.

a) Kwa vipindi vyote viwili vya matengenezo ni jumla ya kiasi gani cha fedha zilizotumika katika kuifanyia matengenezo gati hiyo. Pamoja na kuwa inafanyiwa matengenezo, lakini Mheshimiwa haoni kuwa ile hali ya gati ile ilivyo hivi sasa ya gari kuingia kinyume nyume na kutoka katika hali ya kawaida kila siku wakati haina vizuizi vya kutosha ni kuhatarisha maisha ya wananchi, wakati pale ile ni bandari na magari yanakwenda kuchukua mizigo kila wakati.

b) Kwa gati hii ya Wesha ilitumia fedha kiasi gani katika matengenezo yake na ikiwa kweli kuna mpango wa kusimamia *feasibility study* kuhusu mazingira ili baadae irefushwe. Suala hili lilitokea miaka ya mwaka 2003 mpaka leo ilikuwa serikali inafanya nini ikawa bado haijapata mtu huyo wa kuweza kufanya hivyo mpaka iwe inamtafuta hivi sasa.

c) Mara ya mwisho gati hii ya Wesha kuna dubwasha limewekwa kule lile limewekwa kwa madhumuni gani.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika,

a) Mhe. Mwakilishi, alitaka kujua kiasi gani cha fedha kimetumika katika magengenezo ya mwaka 2001 na 2004. Swali hili Mhe. Naibu Spika, tutamjibu kwa maandishi. Ni lazima turudi kwenye *records* tuangalie matumizi haya na tupate uhalisia wake.

   Mhe. Mwakilishi pia amezungumzia kwamba gati ya Wete ni nyembamba. Tunakiri kwamba kweli gati ya Wete ni nyembamba na gari haipati nafasi ya kuzunguruka. Tulichokieleza kwamba dhamira yetu sisi ni kufanya marekebisho. Katika hatua za awali tuna wenzetu ambao tumeshasaini nao MoU wanafanya *study* kwa bandari ya Mkokotoni, Mkoani, Wete pamoja na Wesha. Mategemeo yetu kwamba katika *study* hii inaweza ikatupa uwanja

mpana zaidi wa kuweza kujenga kwa kuzingatia upana ili kuweza kuakisi haya matarajio yetu.

b) Suala la pili amezungumzia suala la gati ya Wesha, suala zima la upatikanaji wa mtu kufanya *study*. Tumeeleza kwamba sisi kama serikali wajibu wetu ni kufuata taratibu na sheria za nchi. Kiutaratibu hatuwezi kutoka tukanda tuka m-*pick* mtu kwenda kufanya kazi hiyo ni lazima kwamba tutangaze. Tumeeleza kwamba tayari hivi sasa tumetangaza zabuni na tunaendelea na mchakato wa kuzipitia zabuni hizo ili sasa tuweze kutafuta mshindi afanye kazi hiyo ikamilike tuendelee na utaratibu unaofuata. Nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba tuvute subira ili tukamilishe taratibu na sheria ambazo tumejipangia ili baadae tukimbie *queries* zinazoweza kuepukika.

c) Mhe. Mwenyekiti, ameulizia suala dubwana lilowekwa upande wa mwisho wa gati ya Wesha. Dubwana lile lipo kwa ajili ya matumizi ya kiusalama na kuongozea vyombo pamoja na kufunga vyombo vinavyokwenda kupata huduma katika gati husika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nilikuwa naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Bandari ya Wesha na Wete, serikali imeshindwa kabisa kuzifanyia matengenezo zikalingana na usafiri na usafirishaji wa ulimwengu wa kileo. Na kwa kuwa kuna mfanyabiashara anayemiliki hii kampuni ya Azam Marine yuko tayari kujenga *jet* ya hapa Wete au Wesha na tayari taarifa zinaonesha kwamba ameshapeleka maombi yake serikalini ili aweke kitu cha uhakika cha usafiri na usafirishaji, kama alichokifanya hapa Malindi Unguja.

a) Je, suala la Bw. Said Salim Bakhresa ni kweli kwamba ameshaomba serikalini kuweka kitu hicho.

b) Na kama ameomba ni sababu gani za msingi ambazo zimefanya hadi leo hii hajapata ruhusa hio, wakati upande mmoja wa nchi wamempa kule wasimpe kwa nini.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi nimuombee kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema maana jana tulipata taarifa kwamba hali yake ya afya haiko vizuri na alikuwa Dar-es-Salaam, Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kwamba Bw. Said Salim Bakhresa kwa kupitia kampuni yake ya *Azam Marine* amekuja na tumefanya nae mazungumzo. Ameonesha nia na dhamira kutaka kushirikiana na serikali katika kuimarisha na kuboresha gati ya Wete. Hatua za awali amekwenda yeye mwenyewe binafsi kwa kupitia wataalamu wake.

Sisi kama serikali hatuna nafasi ya kukataa msaada au mshirika wa maendeleo. Yeye mwenyewe atakaporudi mara ya pili tutampokea mikono miwili, amekuja akaangalia akaondoka! Alichokwenda kukifanya hatujamuuliza. Kwa sababu yeye amekuja na dhamira tumeisikiliza na hatukumkatalia.

Mimi nikuombe tu Mhe. Mwakilishi, kama una mahusiano makubwa na Mhe. Bakhresa basi mwambia Wizara ya Miundombinu wanakusubiri, ukakamilishe lile jambo ambalo mlizungumza.

Nam. 50
Wananchi wa Pete Kulipishwa Gharama za Kuunga Umeme Kukiwa na Ahadi ya Rais

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza swali langu kwanza nataka nichukue fursa hii kwa dhati kabisa nimpongeze Rais Mstaafu Dkt Amani Abeid Karume kwa jitihada alizozichukua katika visiwa vya Unguja na Pemba likiwemo hasa suala la umeme kule kisiwani Pemba. Hata hii skuli yangu ya Pete imefaidika kwa suala hilo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi ni muajiri wa wananchi wa Jimbo la Muyuni na leo hii Mwalimu Mkuu yupo pale kuja kusikiliza kilio cha muda mrefu karibu miaka mitatu hii. Suala ambalo ni zito, naomba nipate jawabu.

Wananchi na wanafunzi wa skuli ya Pete wamefarijika sana kwa hatua ya Rais Mstaafu Dkt Amani Abeid Karume kutekeleza ahadi yake ya kuvuta umeme katika skuli ya Pete na kuondolewa tatizo la muda mrefu kwa wanafunzi wa skuli hiyo.

(a) Kwa nini Shirika la umeme limeanza kuwadai gharama zote za uunganishaji umeme wakati hatua ya utekelezaji wa ahadi hiyo ni agizo la Rais kupitia Ofisi yake.

(c) Iwapo wananchi kupitia Kamati ya Skuli watabeba mzigo wa gharama za uunganishwaji umeme, ahadi ya Rais itakuwa katika

nafasi gani ya utekelezaji wake kama wasemavyo waswahili “ahadi ni deni”.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 lenye kifungu (a), na (b) kama hivifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu, Shirika linapokea maombi mengi pamoja na ahadi za Viongozi kama ilivyotokea hapo Pete. Shirika hujipanga kutekeleza moja baada ya jengine kutokana na uwezo tulionao. Inapotokezea mahali ambapo ombi hilo na wananchi wakaanza kutoa michango yao basi Shirika hutoa umbele kwa mahali hapo.

b) Kwa kuwa wananchi wa Pete wamelipia agizo hilo kwa bahati mbaya, Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme itazirejesha fedha hizo kwa kuwaingizia wananchi hao kwenye *account* yao ya matumizi ya umeme.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kwa kuweka *hansard* sawa hili deni ni shilingi (Sh 2,495,322.29) milioni mbili, laki nne, tisiini na tano, mia tatu ishirini na mbili *point* mbili, tisa.

Je, serikali inatoa kauli gani hivi sasa kupitia chombo cha wananchi, kwamba deni hilo linafutwa kwa kuanzia hivi sasa. Maana wakenda kununua umeme wa Sh. 50,000/= wanaambiwa Sh 20,000/= tunakata, hiyo ni kauli ya serikali kutoka hivi sasa, hilo deni linafutika wakenda kununua umeme wa Sh. 50,000/= watapata wa Sh. 50,000/= bila ya kukatwa pesa zozote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, deni hilo hata kama lingekuwa la shilingi milioni sita wakati limeingia kwa bahati mbaya kama nilivyoeleza hapo awali kwamba Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme, italifuta deni hilo kwa kuwaingizia kwenye *account* yao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, swali langu jengine hajanijibu. Nimeuliza wananchi au walimu wa Skuli ya Pete watakapokwenda kununua umeme wa Sh. 50,000/- au 60,000 hawatokatwa kitu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Wananchi wanapolipia deni la umeme au ununuzi wa umeme basi kuna gharama ya

service charge ambalo hilo tunakata kutokana na kile kiwango ambacho anacholipia mwananchi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi ya pekee niishukuru sana Wizara hiyo ambayo imewaona wananchi wanyonge. Na kwa kuwa kulitokea ahadi kubwa ya kiongozi wetu mstaafu na kuweza kulirejesha deni hilo. Naomba nitoe shukurani za dhati kabisa ndani ya nafsi yangu.

Mhe. Naibu Waziri, sasa hivi wananchi wengi vijijini wanakuwa ni wanyonge. Na kwa kuwa viongozi wetu wengi wanatoa ahadi za kuwatilia umeme ule mkubwa na kuwafikishia katika *line* ndogo. Je, Mhe. Waziri, umeme kama ule ukifika kwa wananchi ile ahadi ya Mhe. Rais wananchi wapewe kwa njia ya mkopo bado ipo pale pale katika Wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi naomba nitoe shukurani zangu kwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa kuishukuru Wizara yangu kwamba inatekeleza ahadi zake na inatekeleza maagizo yanayotolea na Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Rais wa Kwanza na Mkamau wa Pili.

Lakini vile vile, niseme kwamba ahadi hutekelezwa baada ya wale wananchi watakapoleta maombi yao kwa kutaka kuungiwa umeme wa mkopo na wizara yangu inalichukua ombi hilo na inalifanyia kazi.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Nilitaka kujua Mhe. Naibu Spika, hilo deni ni la muda gani na Wizara italilipa baada ya muda gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, hilo deni ni la muda mrefu na ilikuwa bado hatujapewa malalamiko au hatujaelezwa ile hali halisi iliyotokea. Lakini niseme katika malipo ya deni hilo inategemea jinsi ya matumizi yao ya umeme kwa sababu tutawalipa kupitia *account* yao, wanapokuja kununua umeme basi na sisi tutaliingiza deni hilo au malipo ya deni hilo kwa mujibu wa vile wanavyokuja kununua umeme.

Nam. 55

Kusimamishwa Masomo kwa Baadhi ya Wanafunzi Chuo cha Afya Mbweni

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza:-

Hivi karibuni limesikika tangazo la kusimamishwa masomo kwa baadhi ya wanafunzi wa Chuo cha Afya Mbweni wa kada mbali mbali kutokana na sababu za kutofuata utaratibu.

(a) Je, suala hili ni kweli.

(b) Na kama ni kweli, ni taratibu gani hizo zilizokiukwa.

(c) Na kwa nini waliruhusiwa kuanza masomo bila ya kufuata taratibu hizo ambazo tayari zipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.55 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Wizara ya Afya iliwasimamisha wanafunzi 61 ambao walioingia mwaka wa kwanza wa chuo kwa kipindi cha 2013-2014 bila ya kufuata utaratibu na kuachwa wale ambao wangestahiki kuingia. Na baada ya kulifuatilia vizuri suala hili waliokuwa hawakustahiki kuwepo chuoni sio 61 isipokuwa walikuwa 68.

(b) Taratibu za kuingia Chuo cha Afya ni kama zifuatazo:-

1. Kuomba na kudahiliwa katika chuo wakati tangazo la kujiunga na chuo linapotolewa kwa muda maalumu uliowekwa,

2. Kuwekwa kwa nafasi za ufaulu kwa mtitririko unaohusiana na vigezo vya kuingia chuoni kwa kutumia compyuta,

3. Kuwatangazia wale waliokidhi viwango kwa idadi ambayo chuo inataka kuchukua na kuweka *list* ya akiba kwa wale ambao wamekidhi viwango lakini nafasi ya kuwachukuwa haikuwepo,

4. Kuhakikiwa vyeti vyao kama si bandia na wote waliokidhi viwango na kuwatoa wale wenye vyeti hivyo,

5. Kugawiwa makundi tofauti kulingana na aina ya fani ziliopo na walizoomba kwa uchaguzi wa fani 3,

6. Kuitwa chuoni wale waliokidhi vigezo vya kujiunga na chuo,

7. Ikiwa idadi ya walioitwa haikutimia, kuwaita walio katika *list* ya akiba kwa kufuata mtiririko ili kujaliza lile pengo lililojitokeza kufikia idadi inayotakiwa,

8. Kupewa tarehe maalumu ya kuripoti chuoni kuanza masomo muhula unapoanza.

Uchukuaji wa wanafunzi chuo cha sayansi cha Afya kwa mwaka huu haukuzingatia utaratibu huo kwa makusudi na kukazua malalamiko mengi na yakaripotiwa Wizarani. Kwa vile uongozi wa Wizara ya Afya Mkurugenzi Mkuu, ndie mwenye dhamana ya chuo na kwa kuzingatia kwamba Wizara ya Afya kuwa ndie muajiri mkuu wa wahitimu wa chuo hicho ikaonekana ipo haja ya kuliingilia kati jambo hilo. Maamuzi ya wizara ikawa ni kuwasimamisha wale waliotuhumiwa ili kupisha uchunguzi ufanyike na kujiridhisha kwamba tuhuma hizo ni za kweli au la ili haki itendeke.

(c) Wanafunzi waliweza kuanza kusoma kwa sababu waliruhusiwa na chuo kufanya hivyo. Kama ni kosa ni la uongozi wa chuo chenyewe kutokufuata utaratibu na vigezo kama vile yalivyowekwa kwa sababu ya muhali, kujuana, ujamaa, shindikizo la baadhi ya viongozi wa kisiasa na wa serikali, udugu na urafiki na inasemekana na rushwa pia ilitumika. Matokeo yake chuo kikapoteza muelekeo na kikaacha kufuata utaratibu uliokuwapo na kuchukua wanafunzi wasiostahiki na kuwaacha wale wanaostahiki ambao wamefuata taratibu zote na walikuwa na vigezo vyote wakaachwa kwa sababu wao hawakuwa na watu wa kuwatilia turufu.

Baya zaidi Baraza linalosimamia chuo hicho lilipewa taarifa za mwanzo ambazo ndizo zilizokuwa za kweli na wakapitisha maaamuzi ya wanafunzi kuchukuliwa. Baada ya hapo uchakachuaji ukaanza na kupenyezwa bila ya ukomo wa muda, wenye sifa na wasiokuwa nazo, jambo ambalo pia ni kinyume cha utaratibu.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Waziri, kuna taarifa kwamba imebainika kuna baadhi ya viongozi wameshiriki katika

kukiuka taratibu hizo, je, swali hili ni kweli na kama ni kweli ni viongozi gani hao na hatua gani zimechukuliwa.

b) Je, kuna mikakati gani iliyowekwa na Wizara ama Chuo ili masuala haya yasitokee tena katika miaka inayofuata.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, katika jibu mama nimesema kwamba katika uchukuaji wa wanafunzi kilichojitokeza kulikuwa na nguvu za watu wakiwemo viongozi, Wawakilishi walioko hapa na ukimsikia Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anapiga kelele sana mmoja wa watoto wake yumo ndio maneno yote yanatoka kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa sababu mtoto wake katolewa na Wawakilishi wengine kama mnawataka nitawataja mmoja baada wengine, Mawaziri wamo, Viongozi wa Vyama, Wakurugenzi wakubwa wakubwa katika serikali wamo, fikiria Mhe. Naibu Spika, kama hilo ndilo serikali tuliopewa jukumu halafu wenzetu hawa Mawaziri, Wawakilishi, Wakurugenzi, watu wa siasa, wanakwenda kuyafanya hayo wametukusudia nini.

Mimi kule silimi shamba kama mpunga ukikauka Japan ataleta mchele, ninahudumia maisha ya watu na ili uweze kuhudumia maisha ya watu unatakiwa upate watu wenye uwezo. Leo mtu ana dini ana Kiswahili anakuja kuletwa pale awe daktari. Leo hii mtu unakwenda kwenye kituo badala mshipa kutia damu kupeleka hivi, anatia hivi, hayo ndio matokeo ya Chuo cha Afya Mbweni. Badala ya kumtia mtu *catheter* kwenye njia ya mkojo, anamtia ukeni hivyo ndivyo tunavyofanya.

Halafu watu hao hao wanakuja hapa wanapiga makelele kwa sana watendaji, watendaji, watendaji, lakini wao ndio wanaowayumbisha watendaji, hivyo ndivyo tunavyotaka. Tumewafukuza na tutaendelea kufukuza. Taratibu tuliziweka miaka miwili zilifuatwa, mwaka huu hazikufuatwa. Tutakachokifanya tumeanza kuwatoa na Mwalim Mkuu tutamtoa na Baraza tumelipa ilani na kila kitu tutakachokifanya. Mimi kule nimepewa kazi ya maisha ya binaadam, nimekula viapo vitatu kama daktari, nimekula kiapo cha uwaziri na nimekuwa kiapo cha hapa, mnataka mimi kiapo kinidhuru. Viapo 3 halafu nende nikafanye mambo kama haya, nimewafukuza na nitaendelea kuwafukuza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, mimi ninampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake kwa jinsi walivyochukua hatua kuwatoa wale ambao hawana sifa walipenya mgongo ambao si halali. Swali langu:

(a) ni kwamba miongoni mwa watu waliopelekwa pale ni mwanafunzi ambaye ana *division* ya kwanza ya masomo ya sayansi kutoka Jimbo la

Kiwani ambaye tulimpeleka baada ya mahitajio ya Kituo cha Afya cha Tasini ambacho juzi wamekifungua mwaka huu. Swali langu hivyo yule mwanafunzi ambaye alitoka Kiwani *division one science* pia hakuwa na sifa na kama hakuwa na sifa je, Wizara yako itakuwa tayari kuwatuma Wawakilishi tukachunguze hao waliobakia kama wana sifa kuliko zile.

b) Ikiwa Wawakilishi miongoni mwao ni mimi niliyepeleka mtoto baada ya kuomba Wizara na hao wenzangu wengine utawataja humu Barazani ili tuone sifa za yule wa Kiwani aliyetolewa na wale wengine waliobakishwa ili wazanzibari waone kwamba kweli Wizara yako imewajibika na iko katika hatua nzuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hija Hassan Hija, ndio katika walioleta watoto nje ya utaratibu. Taratibu nimesema hivi watu wameanza kutiwa chuoni kuanzia mwezi wa Mei mpaka Septemba, utaratibu wote ukafuatwa. Mhe. Hija Hassan Hija, mwanae ana vigezo vyote sikatai, lakini hakuingia kwa utaratibu. Kama alikuwa kweli anajua mwanae ana utaratibu kwa nini asifate vigezo, kwa nini ende akampenyeze wakati masomo yeshaanza, si utaratibu, nimemfukuza akitaka aombe mwakani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, mimi si mtaalau wa afya na mimi naunga mkono sana, mimi nilikuwa katika Kamati ya Ustawi kama kuna watu ambao walipenya kwa mgongo usio halali naunga mkono moja kwa moja. Mtoto wangu kutoka Kiwani sikumpenyeza kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, amejaza fomu na akalipa benki shilingi laki sita zikapokewa na Wizara yake kupitia Chuo na akasoma miezi zaidi ya miwili.

Sasa ninachosema kama utaratibu huo pia si halali baada ya kuomba Wizara kwamba Kiwani kuna mahitajio ya mtaalam wa Afya ambaye hatuna tukaambiwa mtafuteni kijana mwenye sifa tukamtoa Dar es Salaam ambaye alikuwa anakwenda form V tukamkatisha kwa kushauriana na Wizara, kama si halali basi Baraza lipewe fursa likachunguze hao walioingia kihalali, je, wana sifa angalu za C tatu, wangu mimi ana zaidi ya B mbili na C zaidi ya tano, ikiwa kuna watu wana C zaidi ya hizo, basi hao wana sifa tuwache waendelee. *Unless* kama kuna watu wamejipenyeza, basi watajwe hapa iliwatolewe tuone hadharani.

Mhe. Naibu Spika: Mimi nadhani nisaidie serikali imesikia, ichukue suala hilo wende wakaangalie utaratibu uliotumiwa.

Mhe. Naibu Waziri: Ripoti hii hapa ya Chuo imefanywa na wataalam kutoka Chuoni na Wizarani haimaanishi kwamba lazima mtoto atoke Kiwani mfanyakazi wa Wizara ya Afya, anaweza akatoka popote. Sasa kama una

lazima atoke Kiwani ndio afanye Kiwani si utaratibu wa serikali, katika ripoti hii wanafunzi hawa waliosajiliwa wakwako hayumo, Mhe. Hija Hassan Hija, usitake kujipapatua unalijua vyema suala hili na Mhe. Juma Duni Haji, alikwambia kwamba wewe Mhe. Hija Hassan Hija, kelele zote zile unazopiga halafu bado unatupenyezea watoto ukasema mwanangu ana vigezo. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. ahsante Katibu tuendelee, kiti kinasema tuendelee nakuomba Mjumbe ukae. Katibu tuendelee.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nazungumzia kanuni ya 67 inazungumzia Spika kutilia nguvu kanuni.

Mhe. Naibu Spika, kanuni ya 67(1) inasema:

"Spika atawajibika kutilia nguvu kanuni zote za Baraza na endapo Mjumbe yoyote hatoridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake kwa Kamati ya Maadili ambayo itatakiwa ikutane mara moja kufikiria na kutoa ushauri wake kwa Spika juu ya jambo hili"

67(2) "Spika anaweza kumtaka Mjumbe yoyote anayekiuka kanuni hizi kujirekebisha mara moja na Mjumbe yoyote anaweza kusimama na kumuarifu Spika, kuwa Mjumbe fulani anakiuka kanuni ambayo ataitaja"

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni zetu hizi tafsiri ya neno Spika, katika maelezo ya utangulizi wa kanuni zetu inasema:

Spika maana yake ni Spika wa Baraza isipokuwa kwamba Naibu Spika, Mwenyekiti wa Baraza au Mwakilishi mwengine yoyote aliyechaguliwa kwa ajili hiyo anapokuwa anakalia kiti cha Spika, katika kikao chochote cha Baraza au anapokuwa akitekeleza shughuli yoyote ambayo ni kazi ya Spika atakuwa na madaraka na mamlaka yote ambayo amekabidhiwa kwa Spika, kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni hizi.

Mhe. Spika, nimesimama kuomba utaratibu kwa sababu ni juzi tu tumetahadharishwa humu ndani kwamba chombo hiki ni kikubwa tukiheshimu, lakini namna ya baadhi ya lugha, majibu hata mkabala hata *style* ya baadhi yetu katika kujibu maswali yanashusha hadhi ya chombo hiki na pamegeuka kama vile tuko katika harusi au matanga, watu wanashushuana. Mhe. Naibu Spika, wala huu si ukumbi wa taarab kama tunakuja kuoneshana mipasho hapa.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Naibu Spika, tukiheshimu kiti kitilie nguvu kanuni kwamba hizi taratibu ziheshimiwe, kama si hivyo tutakuja kufika pahala Mhe. Naibu Spika, itakuwa kila mmoja anafanya anavyotaka humu ndani, hadhi, heshima na nafasi ya chombo hiki katika jamii itaporomoka na kikiporomoka chombo hiki, maana yake tumeiangusha nchi yetu yote Mheshimiwa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe kanuni zote hizo ulizosema tutazisimamia na tutazitekeleza na serikali imeliona hili suala. Kwa hivyo, hatua zitachukuliwa na tutaweza kuzungumza na wenzetu wanaohusika ili masuala kama haya yawe pande zote mbili yanakwenda sawa. Na Mhe. Mjumbe, nadhani kama hukuridhika kanuni ya 66 imeeleza ufanye nini. Kwa hivyo, tunakuruhusu kama hukuridhika, unaweza ukafanya halafu Kamati ya Maadili itakaa itaweza kuangalia hali hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, sikuwa na lengo hata siku moja la kusema kwamba nikipeleke kiti katika Kamati ya Maadili haidhuru kwamba mimi mwenyewe ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Maadili. Lakini kwa sababu yangu hiyo, ndio maana nimesimama Mhe. Naibu Spika. Kwa sababu nadhani tujifunze humu ndani kwamba kiti kinapotoa maelekezo lazima tuheshimu, sasa Mhe. Naibu Spika, kama nyinyi mnokalia viti hamsimamii, kwa mfano sasa hivi umeshasema kwamba umetoa muongozo halafu ukasema tuendelee.

Ananyanyuka mtu anasema nijibu mie halafu anaendelea kujibu, sasa tunajiuliza Mheshimiwa katika nafasi kama hiyo anayekiongoza kikao anakuwa aliokaa juu ya kiti au anayeamua mwenyewe kama anataka kujibu au hataki kujibu. Mwenye kuamua swali lijibiwe au lisijibiwe ni Mwenyekiti. Anayeamua uzungumze au usizungumze ni Mwenyekiti na tuna taratibu zetu kwamba akitoa kauli hata kama umesimama unatakiwa ukae kitako ndio taratibu zetu.

Kwa hivyo, naomba sana Mheshimiwa, sina nia ya kupeleka popote isipokuwa nilikuwa ninasisitiza tu kwamba ni kukiheshimu kiti kwako na kwetu Mhe. Naibu Spika, na yeyote atakaekalia kiti hicho kwamba tuheshimu kiti. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Sawa sawa tumeelewa tutaheshimu pande zote mbili, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Wajumbe.

Nam. 34

Baadhi ya Vifungu vya Katiba ya Zanzibar Kupingana na Demokrasia na Haki za Jamii

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, naomba swali langu lijibiwe, lakini kabla ya kujibiwa naomba kufanya marekebisho yafuatayo:-

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba niseme yafuatayo:

Mhe. Mjumbe amebadilisha vifungu vya suala lake vya Katiba, Katiba Mhe. Naibu Spika, si kitu cha kuchezea hatuwezi tu tukaja hapa kifungu cha (3) akaweka kifungu cha (13), maana yake ile tafsiri sasa ni tofauti kabisa. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mjumbe anapouliza a-*quote* vifungu ambavyo ndivyo anavyotaka ajibiwe, vyenginevyo swali tutakalomjibu linaweza likawa ni tofauti na vile anavyotaka. Kwa hivyo, naomba nitoe taarifa hiyo.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, ni kawaida wenye maswali yao yote wanapoona kuwa halikuandikwa kama alivyokusudia kuleta masahihisho na kujibiwa, lakini majibu yangu hayakuridhisha na ambayo ndio yenye makusudi hasa yanayopingana na kifungu nambari 9(1) naliondoa swali langu.

(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 61

Kuchelewa Kutungwa kwa Kanuni za Sheria

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Kwa kawaida Baraza la Wawakilishi miongoni mwa kazi zake ni kutunga sheria na mara nyingi baada Baraza kufanya kazi hiyo sheria husika huagiza kutungwa kwa kanuni ambazo huwa zinatoa ufafanuzi wa sheria husika na mara nyingi huagizwa Waziri kutunga kanuni hizo.

(a) Ni sheria ngapi zilizotungwa hapa Zanzibar ambazo hadi hii leo kanuni za sheria hizo bado hazitatungwa na Waziri husika.

(b) Kama zipo sheria hizo ambazo hazijatungwa kanuni ni sababu gani zinazofanya kukawia kutungwa kwa kanuni hizo.

(c) Je, ni athari gani zinazopatikana kutokana na kutokuwepo kwa kanuni hizo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Sheria yoyote inayotungwa na Baraza lako tukufu Mhe. Spika, basi sheria ile huwa na msimamizi wake maalum, na si Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Spika, msimamizi anayehusika huwa ni Waziri anayehusika na masuala hayo ambayo sheria hiyo inahusika na inalenga kuyashughulikia. Na ndio maana Waziri anayehusika na mambo ya kilimo kwa mfano huleta sheria inayozungumzia mambo kama hayo.

Sheria kama hiyo hutayarishwa na Wizara husika, ikapita katika Kamati maalum na hatimae kupelekwa katika Baraza la Mapinduzi. Baraza la Mapinduzi ikikubali basi hupelekwa Baraza lako tukufu kwa kupitishwa. Baada ya sheria kupitishwa na kutiwa saini na Mhe. Rais, Waziri anayehusika ndie anayepaswa kuisimamia kwa utekelezaji wake sheria hiyo. Ndio maana takriban sheria zote katika kifungu cha tafsiri husemwa hivi:

Waziri maana yake ni Waziri anayehusika na mambo hayo yaliyomo katika sheria hiyo. Kwa maana hiyo Waziri wa Katiba na Sheria hahusiki na sheria hiyo hata kidogo.

Hata hivyo, sheria zinazopitishwa nyengine huwa zina vifungu vinavyomtaka Waziri huyo kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sheria hiyo. Kanuni hizo huwa ni baina ya Wizara wenyewe, lakini hutakiwa wawasiliane na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili Afisi ya Mwanasheria Mkuu aweze kuziandika vizuri kisheria na hatimae aweze kuzitangaza katika Gazeti la Serikali.

Sheria zinaweza kutekelezwa bila ya kuwa na kanuni ikitegemea tu kuwa utekelezaji huo hauhitaji kutungwa kwa kanuni. Na ndio maana sheria hutoa mwanya na kusema kwamba Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sheria hii. Kwa maana hiyo, hakuna ulazima wa kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hiyo. Vyenginevyo inapotokea kuwa lazima kuwe na kanuni hii ili sheria iweze kutekelezeka,

basi kucheleweshe kutunga kanuni hizo kutaathiri sana uanzaji wa utelekezaji wa sheria husika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu ambayo ameyatoa Mhe. Waziri ambayo mengine sikuridhika nayo kwa sababu swali langu mimi ninaiuliza serikali na ninachojua mimi serikali inawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi, akiwa Waziri wa Sheria, akiwa Waziri wa Viwanda, lakini serikali ni serikali na yeye ni mmoja kati ya hao *cabinet.* Kwa hivyo, kuniambia kwamba masuala haya labda yatajibiwa ile Wizara husika iliyokuwa imetunga ile sheria mimi ninafikiri sio sahihi, yeye pia alikuwa anapaswa kujibu kama anazijua, kama hajui jambo jengine.

Lakini mimi nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri kwamba, je, kwa kuona zile sheria zinazotungwa ambazo zinahitaji kuwepo na kanuni zile zinakawia kutungwa na zile Wizara husika au yule Waziri husika ambaye ameagizwa. Huoni kuna haja kwamba sheria zote zinazoletwa Barazani zakaja na kanuni zake ili tuzipitishe kwa pamoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, nakubali kwamba serikali ni serikali, lakini naomba ujuwe kwamba serikali kuna kitu kinachoitwa *individual responsibility* ya Wizara, sasa Waziri anayehusika na sheria ndio muhusika mkubwa wa sheria. Wizara yangu haihusu sheria zote za serikali nzima, kila Waziri ana jukumu la sheria yake. Na anapotaka kutengeneza kanuni, Waziri ndie anayetengeneza Kanuni sio Wizara ya Katiba. Kwa hivyo, Waziri wa Katiba au Wizara ya Katiba haijui kanuni ambazo zimetengenezwa au hazikutengenezwa hilo ni la kwanza.

Lakini la pili, huwezi wakati unafanya sheria ukatengeneza kanuni, lazima kanuni ije baada kumalizika kwa sheria. Na hii ni kwa sababu katika sheria kuna kifungu kinachosema kwamba Waziri anaweza kutunga kanuni ikiwa ataona kwamba kuna ulazima wa kutunga kanuni. Kwa sababu kanuni si kitu cha ulazima katika utekelezaji. Pale ambapo Waziri atahisi kwamba kuna haja ya utekelezaji wa Kanuni, basi Waziri atatunga Kanuni huyo anayehusika sie Waziri wa Katiba na Sheria. Huyo Waziri anayehusika akitaka kutunga kanuni atatunga yeye na maofisa wake watapeleka Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuandishwa vizuri ndio utaratibu uliopo.

Na pale ambapo hakuna haja ya kutunga kanuni, sheria inaweza ikatekelezwa bila ya kuwepo kwa kanuni. Kwa hivyo, sioni kwamba kuna umuhimu wa kila sheria inayokuja hapa ije na kanuni, tunaweza tukapoteza wakati pengine kanuni zile hazina maana kwa wakati ule.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa Katiba yetu ya Zanzibar ya 1984 kifungu cha 5(a) (1) inatambua dhana nzima ya mgawanyo wa madaraka yaani *separation of power* na kwa kuwa kwa vyovyote vile hakuna muhimili ambao unatakiwa kuingilia kazi za mhimili mwengine. Je, kazi ya kufunga sheria ndogo ndogo yaani kanuni kuendelea kuachia mhimili wa *executive* kufanya kazi hiyo badala kazi hiyo kufanywa na *legislature*, sio kwenda kinyume na Katiba chini ya kifungu ambacho nimekitaja.

(b) kutokuwepo kwa kamati ya sheria ndogo ndogo ambayo inaanzishwa chini ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu cha 116 huoni kwamba ni sababu tosha ya kuzotesha utungwaji wa kanuni kwa sababu kunakuwa hakuna ufatiliaji wa kazi ile.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwa mujibu wa Katiba kuna mgawanyo wa madaraka. Kuna *executive*, kuna *legislature* na kuna *judiciary*. Kazi zinazofanywa na *legislature* Baraza hazipaswi kufanywa na *executive* kwa maana hiyo, kazi zinazofanywa na Baraza la Wawakilishi hazipaswi
kufanywa na Mawaziri au na serikali. Lakini Katiba ndio Katiba mama Katiba imesema kwamba shughuli hizo zitafanywa kwa sheria kwa mfano iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Sasa sisi hapa sote tunapotunga sheria tuna *delegate powers* kwa Mawaziri tunasema Waziri anaweza kutunga kanuni. Kwa hivyo, sisi Wawakilishi hapa tumeshatoa idhini ya kumpa Waziri kutunga kanuni.Kwa hivyo, Waziri anapotunga kanuni hendi kinyume na Katiba kwa sababu ni sisi hapa tuliompa kwa mujibu wa Katiba, la kwanza.

Lakini la pili ikiwa tunataka tuzione zile kanuni zinazotungwa hapa Barazani kuna utaratibu wake.Tunapotunga Katiba ili kuthibitika kuna mambo mawili, kwanza kanuni zinaweza zikatungwa na kwenye sheria tunasema tukishatunga kanuni zitatumika pale tu Waziri atapotia sahihi. Sisi wenyewe hapa ndio tunaowapa kibali hicho mawaziri. Lakini tunaweza tukaandika katika sheria kwamba kanuni hizi lazima ziwe *laid be for the assembly*, kwamba kanuni haziwezi kutumika mpaka kwanza ziwekwe Barazani, ukiweka Barazani pale kuna mambo mawili, ku-*lay be for the assembly* ni kuziweka tu kama tunavyoweka magazeti ya serikali, lakini kuna *lay be for the assembly* na Wawakilishi pengine kuzijadili ni sisi wenyewe tu kuamua.

Sasa kama hayo hayajaamuliwa kwa utaratibu uliowekwa kisheria basi Waziri bado ana haki ya kikatiba ambayo tumempa sisi Wawakilishi kutunga kanuni na hayo ndio yanayotokea kwa hivi sasa. Kwa hivyo, hatwendi kinyume na Katiba nakushukuru.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi

(Majadiliano yanaendelea)

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hoja iliyokuwepo mezani imewasilishwa na Mhe. Ali Mzee Ali, Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi na kwa bahati hoja sasa hivi inajadiliwa yeye mwenyewe hayupo, sasa sijui hii michango itakayokuwa inachangiwa hapa kwa sababu baadae atatakiwa aje asimame kwenye kiriri kwa ajili ya kutoa ufafanuzi. Sasa hizi hoja zitakazojadiliwa hapa sijui nani ataziratibu na baadae tuje tupate majibu muwafaka.

Mhe. Naibu Spika, naomba muongozo wako.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri kwa utaratibu tunaweza kuendelea, kwa sababu ile kamati…

(Hapa Mhe. Ali Mzee Ali, Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi aliingia):

Mhe. Naibu Spika: Nadhani yamekaa sawa kaa kitako.

Mhe. Ali Mzee Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi): Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa yako nilikuwa na kazi ninafanya, lakini nina wenzangu kwenye kamati wapo na tumepeana majukumu ya kuchukua michango.

Mhe. Naibu Spika: Sisi kwa utaratibu wetu hizo kazi nyengine waachie wenzako wewe ubakie humu uchukue maelezo.

Mhe. Ali Mzee Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi): Sawa, wenzangu watakwenda kufanya kazi hiyo, waache wachangie.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi isipokuwa nimshukuru *Allah* kwa asubuhi hii kutupa hali ya afya nzuri na kuweza kupata nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika suala zima hili la Kamati Teule kuhusu Migogoro ya Ardhi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze kamati hii adhimu iliyofanya kazi ambayo ilipewa na Baraza hili tukufu la Wawakilishi. Kwa kweli walifanya kazi kubwa na ngumu yenye matatizo aina kwa aina.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba tatizo hili la ardhi ni kubwa na ni la miaka mingi, hii ni miaka 50. Hivyo, kama ni mti basi ulikuwa unaweza kutoa sarfa ya aina yoyote unaotaka. Kwa kweli hii kazi iliyofanywa na hawa wenzetu mimi nasema ni robo ya matatizo ya ardhi yaliopo Zanzibar.

Kwa hivyo, jambo hili si jambo la kulibeza kwa sababu sifa ya ardhi haiongezeki kila kukicha inapungua kutokana na hali ya kima cha maji ya bahari kuzidi na kuweza kuchukua maeneo mbali mbali ya ardhi. Sasa hii ardhi ndogo tuliyonayo basi ni vyema kuipa heshima kubwa na tukaienzi ili kizazi chetu kilichopo na kijacho kiweze kufaidika katika ardhi hii.

Mhe. Naibu Spika, katika hadidurejea zilizofanyiwa kazi na kamati hii adhimu kwa kweli zote zimesibu, hakuna hadidurejea ambayo walipewa na Baraza hili ikawa sio kweli yaliyosemwa na Wajumbe wa Baraza hili. Hadidurejea zote zimeelezea wazi kwamba hili ni tatizo na matatizo hayo yapo. Kwa hivyo, hayo yalikuwa ni mapambano baina ya kamati na wahusika waliochukua maeneo haya.Hivyo, kazi waliyoifanya wenzetu ni kazi kubwa na ya muhali, kazi ya mapambano na bado mimi nasema wanastahiki pongezi kubwa katika kushughulikia matatizo haya.

Mhe. Naibu Spika, katika kazi hii mimi mwenyewe na watu wangu wa Jimbo la Tumbe tumeathirika sana katika maeneo haya ya ardhi yaliyotolewa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati bila ya kujali kwamba wananchi wa Jimbo la Tumbe nao wana haki ya kupata ardhi hii. Kwa kweli inasikitisha kiasi fulani kwa sababu Mhe. Naibu Spika, Katiba yetu ya Zanzibar Sura ya Pili, kifungu cha 9(2)(a) kinasema kwamba,

> "Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na Katiba utatoka kwa wananchi wenyewe"

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa kauli hiyo ya Katiba wananchi wa Kijichame, Tumbe ni miongoni mwa wananchi wa Zanzibar, ni miongoni mwa wana wa

Serikali ya Zanzibar. Na wananchi hawa walipohisi kwamba hii ardhi inaanza kupimwa na kuuziwa watu wengine kinyume na wale ambao wapo katika maeneo yale wakapeleka madai yao serikalini, madai hayo serikali ikakubali kwamba na wao wana haki ya kupewa ardhi hiyo. Barua yao iliandikwa tarehe 12/5/2010, kupeleka serikalini na serikali ikakubali, wakatoa muda kwamba baada ya siku 60 wananchi hao waweze kupewa maeneo hayo na wao waweze kuishi.

Serikali ikakubali kwamba katika viwanja walivyovipima wapewe asilimia 70, lakini Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha wananchi hao wamekoseshwa haki yao ya kikatiba. Kwa hivyo, nasema Mhe. Naibu Spika, bado hatujawa tayari kufuata sheria na taratibu tulizojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika viambatisho kuna watu waliopewa maeneo hayo ambao wa kupewa mwanzo ni wale walioitunza ile ardhi, tushasema kwamba ardhi yote ni mali ya serikali, lakini hii serikali na hawa watu wa Kijichame, Tumbe nao ni jumla ya watu wa serikali, lakini bila kujaliwa wananchi wale, wamepewa watu wengine ambao mimi nahisi kwamba hata hiyo taarifa kama mtu ana eneo la kiwanja pale hana.

Mhe. Ali Mzee Ali, aliposoma hii hoja alivyoelezwa na watu wa ardhi kwamba walitakiwa wananchi hawa walipie shilingi laki mbili kwa kila kiwanja, lakini wameshindwa kupeleka. Kwa maombi yaliomo humu Mhe. Naibu Spika, ninaamini kwamba na hawa waliopewa hakuna shilingi iliyotolewa kwa watu hao waliopewa viwanja. Kwa sababu maombi mengi yametoka katika taasisi hayakutoka kwa watu wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hapa waliopewa viwanja hivyo kuna Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ndio waliotoa maombi kupewa watu kama vile orodha ya viongozi wanaomba kupewa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Maafisa Wadhamini, Maafisa wa Wilaya na Mikoa. Sasa hawa wananchi wa eneo hilo ambalo eneo hilo tangu mwaka 1964 wanalitumikia, wanaliheshimu, wanalienzi, leo wakubwa wote wa serikali hii ndio waliopewa maeneo hayo, wao wananchi kwa nini wasipewe na wananchi hao bado wanazaa. Sasa aliyechini ya lile eneo hapewi.

Mhe. Naibu Spika, kuna watu eneo hili wako mwisho Unguja, hapa ana ardhi Tumbe, ana kiwanja cha nyumba Tumbe. Mheshimiwa hii si haki kwanza angelijaliwa huyu aliyeienzi hii ardhi. Ningelimuomba sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa maombi ya watu hawa mengi ya maombi haya yaliyoanza mwaka 2008 mpaka 2009. Kwa hivyo, hawa hawana tena haki ya ardhi hii. Kwa sababu muda wa miaka miwili tayari umeshamaliza.Hivyo, haitopendeza wakati haitakuwa haki kuona kwamba

watu hawa waliopewa kwa wakati huo bado wanaendeleza hizi ardhi kuwanazo. Kwa sababu hakuna hata mmoja aliyeanza kuitumia ardhi hii.

Sasa kama hii sheria tunaijadili, siku moja alitwambia hapa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwamba na nyinyi Wawakilishi tulikupeni viwanja hamjavifanyia kazi. Kwa hivyo, viwanja vile vitarudi serikalini. Sasa kabla ya kurudi vya Wawakilishi ambavyo wamepewa mwaka 2001, kuna watu hawa washapewa toka mwaka 2008 na 2009 hawajafanya lolote. Ningelikuomba sana Mhe. Waziri, viwanja hivi virudi serikalini wananchi wetu waweze kufaidika na maeneo haya.

Mhe. Naibu Spika, watu wa ardhi waliwaambia watu wa maeneo hayo kwamba watapata *phase* ya pili viwanja katika upimaji. Kwa bahati nzuri wananchi wa maeneo haya wakakataa na wana sababu tosha ya kukataa, kwa sababu ni maeneo ya maziwa yanayotuama maji wakati wa mvua na kuhama kwake maji hayo yana muda mrefu. Kwa hivyo, watu waliokuwa hawana uwezo ndio wanaowapeleka kwenye madimbwi ya maziwa wale wenye uwezo ndio wanaopewa maeneo ya starehe zaidi, hii itakuwa hatujawatendea haki wazee wetu, inauma kabisa.

Kwa hivyo, mgawanyo huu Mhe. Waziri wa Ardhi, sisi watu wa Tumbe hatukubali kabisa, hapa bado wananchi wa Tumbe hawajatendewa haki, kwanza wapate wananchi wa Tumbe panapobakia serikali iangalie na wengine, lakini mwananchi mzalendo pale hapewi eneo, wanapewa watu wengine wa mbali mno na eneo kwa kweli hiyo si haki. Kwa sababu kama ardhi ni mali ya serikali hawa nao watu wa serikali. Hivyo, wana haki zote kama walizokuanazo watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, hili nalizungumza kwa maeneo matatu; eneo la Kijichame, eneo la Tumbe kwa Mwanasoza maarufu anaitwa kwa Mzigua na eneo la kilimo na watu wa kilimo na ardhi. Hili eneo liko chini ya watu wa Tumbe Kibiriti, leo ukiangalia majina yaliyokuwemo humu ni watu wanaotoka mbali, ni Wazanzibari sawa, lakini wanatoka mbali na eneo na sisi bado haya maeneo tuna shida nayo ndio bado ukaona tunazaa, itakuwaje kuwa sasa baada ya kukaa mtu karibu na wazazi wake ende akahamie maeneo mengine ya mbali.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, haki hii nakubaliana na maoni yote ya kamati irudi serikalini na sababu hiyo ni nzuri kwa sababu hata muda waliopewa hawa watu ushapitwa na wakati, zaidi ya miaka mitano hapajafanywa lolote. Kwa hivyo, irudi serikalini kwanza serikali iwaangalie wananchi wa maeneo haya waweze kupata haki yao hii.

Mhe. Naibu Spika, kuna eneo la mwekezaji Makangale, kuna mwekezaji pale maarufu anaitwa Mpapindi. Hii ardhi wahusika wa eneo hili ni wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe, wananchi hao baadhi ya wengine wako Msuka, lakini eneo hili akapewa mwekezaji bila ya wale wananchi walio na vipando vyao, miti na mambo mbali mbali kujaliwa na hawa wakafuatilia serikalini toka mwaka 2004. Serikali ikakubali kwamba lililofanyika ni kosa bila ya kuwalipa fidia wananchi wa eneo lile. Lakini fidia hiyo Mhe. Naibu Spika, hadi hapa niliposimama saa tano kasoro kama dakika kumi hivi, wananchi hawa fidia yao hawajalipwa hadi leo.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na hoja yao na hoja ya kamati kwamba muda ushakuwa mrefu wa kulipwa wananchi hawa shilingi 15 milioni, kwa kweli umeshapitwa na wakati. Ni vyema serikali ikajali kilio cha wananchi hawa na ni vyema kwamba mwekezaji huyu toka awekeze hapa Makangale na Vumawimbi, hajaisaidia serikali hata senti tano halipi.

Sasa mimi linakuwa linanisikitisha sana hili, tunaweka wawekezaji ili nchi yetu tupate mapato, wananchi wetu wanatoa ardhi au serikali inachukua ardhi za wananchi walizokuwa wanazimiliki wanawapa wawekezaji, mwananchi halipwi ile fidia yake, ardhi anapewa mwekezaji, mwekezaji naye pia halipi. Toka mwaka 2004 mwekezaji huyu hajailipa serikali hata mara moja anapewa heshima zote, anapewa huduma zote ndani ya nchi hii, sijui anasimamia sheria gani huyu ya muda wote huo kuwa halipi, lakini bado anaendelea kuishi na ardhi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi eneo hili la kwa Mpapindi nishakwenda mara mbili, mara ya kwanza nilikwenda na Kamati ya Fedha, Kilino na Biashara na mara ya pili, nikapelekwa na tume hii tuliyoidhinisha kusimamia kero hizi za ardhi. Mhe. Naibu Spika, kwa hali yoyote mwekezaji huyu anaigiza. Kwa sababu ukifika katika maeneo yake ana boti iko juu, lakini boti hiyo inaelekea inakwenda baharini, kwa sababu hakuweka pale kama ni *furniture* hapana. Ile boti inakwenda baharini sijui kazi yake inakwenda kufanya nini. Lakini boti iko nzima kabisa na inaelekea inafanya kazi. Kwa hivyo,vyote atakuwa ana kitu anaingiza na kuingiza kwake yeye anauza na anapata faida, lakini toka mwaka 2004 Serikali ya Zanzibar haijafaidika na kodi ya ardhi hii.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hili mimi linani-*disturb* sana kila kodi tunawapandishia wananchi tu, kila kitu anapandishiwa mwananchi tu, kumbe pana watu wengi hapa nchini tumewapa mali zetu, lakini hawatoi kodi. Kwa kweli tunamuumiza nwananchi huyu, bwana alitakiwa alipe dola kila mwaka dola 8 sijui nimesahau kidogo, lakini tucheze na dola 9. Kwa hivyo, kwa pesa za Tanzania ni pesa nyingi hizo Mhe. Naibu Spika, na huyu sio peke yake.

Mhe. Naibu Spika, ukienda kwenye kitabu cha Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali matatizo hayo ya ardhi yapo mengi mno, watu wamepewa ardhi, lakini hawalipi kodi ya ardhi sisi tunazidi kuwakandamiza wananchi tu kuwaongezea kodi. Hapa tutakuwa hatutendi haki, haiwezekani mgeni akaja hapa akawa na hali zaidi kuliko mwenyeji wa nchi hii, hili ni kosa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hizi sheria si za kubandika bandua na kwamba tumetunga wenyewe, kama tumetunga usimamizi si wa Mzungu, Muingereza wala Mjapani, usimamizi ni wetu wenyewe; kama ni wetu wenyewe, kwa nini ikawa tunashindwa, kwa nini wageni ikawa wako juu kuliko wenyeji.

Mhe. Naibu Spika, ili tufike katika maendeleo kwanza ni kuondosa muhali, inaelekea tunaogopa sana muhali na kama tunaliogopa hilo basi maendeleo yaguju hayatopatikana Zanzibar. itabakia nyinyi wakubwa kwenda huko nje tu, mkija hapa mkitusifia kwamba nchi fulani washapiga hatua hii, nchi fulani wako hivi ndilo litakalobakia tu hilo. Kwa nini wafikie huko, hawajaungwa hao na mikono minne, wala miguu minne isipokuwa kubadilishana mawazo tu.

Lakini sasa sisi tumechukua haki yetu tunawapa watu bila sisi wenyewe kuwafuatilia na wanaishi hapa na kufanya wanavyopenda. Lakini Mwananchi kuchukua siku moja au mbili tu tayari vikwazo, mwananchi huyu atatakiwa ardhi ile airejeshe *No*, haiwezekani hiyo Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, mimi naipongeza sana kamati kuweza kuyachimbua haya, kazi kubwa na naiomba serikali wakati tatizo lile la ardhi ni kubwa tusitosheke na kubakia na haya yaliyoletwa na kamati. Ni vyema serikali ikaadhimia kabisa kuunda kamati *special* au Baraza la Wawakilishi likatengeneza kamati rasmi ya kushughulikia matatizo na mgogoro ya ardhi, kinyume na hivyo Mhe. Naibu Spika, hatutofika popote.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali tumeshaunda kamati nyingi teule kushughulikia matatizo mbali mbali, jawabu ya kamati hizo mara nyengine yanakuja hayaridhishi ikabidi zirejeshwe tena serikalini. Kwa hivyo, naiomba sana serikali suala hili la ardhi lisimamiwe ipasavyo, tukiendelea kupuuza puuza mambo aah, wacha bwana wee, hatufiki mwishoni Mhe. Naibu Spika. Waswahili walisema, “Kuficha mwana kulia basi utalia wewe”. Mimi naona humu hakuna Waziri hata mmoja aliyekuwa hakupewa kiwanja Tumbe, Wakuu wa Vikosi wote wamepewa viwanja Tumbe, Wakuu wa Mikoa wa Pemba, Wakuu wa Wilaya Pemba na Maafisa wao wote serikali nzima iliyoko Pemba wamepewa viwanja Tumbe, lakini watu wa Tumbe wenyewe hawakupewa hata mmoja.

Mhe. Naibu Spika, kweli hii inasikitisha sana, kuna mawaziri wengine wanasema wao hawana sawa, lakini kama hawana ukichukua asilimia 99 ni wao. Kwa hivyo, Waswahili wanasema "Samaki mmoja huozesha shazi lote". Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hii si haki kwa kweli na tunaendesha mambo mfano wake tunaona kama mambo haya yatamalizika katika hii *face* ya dunia, wengi tunaona hivyo na kumbe hivyo sivyo. Kila unalolifanya hapa linaandikwa na linadhibitiwa likiwa la kisiasa, dini au lolote hilo linadhibitiwa.

Kwa hiyo, furaha ya hapa duniani ni kilio kikubwa kisichonyamazika cha Akhera. Wee kunja tu kila pahali sema pangu, hapo ni pangu, hapa ni pangu, huu upangu iko siku utakuja kujijutia. Mheshimiwa, tujaribu kutoa haki kwa wenye kaki,

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naiomba sana serikali watu wa maeneo haya wapewe haki zao na wale wote waliopewa muda umekuwa mkubwa, sheria haiwaruhusu tena kupewa kwa sababu miaka miwili imepita na huu ni mwaka wa tano tunaoumaliza. Hivyo, maeneo haya yarudi serikalini ili wenye haki ya maeneo haya waweze kupewa.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu, *Mola Mtukufu Allah Subuhana Wataalla* kwa kutujaalia asubuhi ya leo kuamka tukiwa hai na wazima na tukawepo katika chombo hichi ambacho ni muhimu sana katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mjadala wa hoja hii ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kuchunguza migogoro mbali mbali ya ardhi, ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri mzee wangu Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Naibu Spika, itakuwa sitendi haki kabisa kama sikuanza na mimi kwa kuipongeza Kamati hii, na ninaamini hasa Mwenyekiti wake, kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya. Jana wenzangu walisema na mimi ninaendelea kusema kwamba kamati imefanikiwa kufuta zile hisia ambazo zikielezwa au zikinong'onwa kwamba labda Kamati hii haikuwa na nia ya kufanya kazi iliyokabidhiwa na labda ilikuwa ikipoteza muda tu.

Muda ambao wameutumia ambao ninasikia muda hasa waliolipwa kwa kazi hii ni mchache sana kuliko kazi kubwa ambayo wameifanya na siku ambazo wamezitumia kufanya kazi hii. Mimi nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, ripoti hii na vielelezo vyake, mimi ninaweza kusema ni ya kwanza ya aina yake katika Baraza la Wawakilishi. Tumeunda kamati nyingi na bila shaka zimefanya kazi kubwa na zimeleta ripoti zake, lakini Mheshimiwa hii imeandikwa vile ripoti za asili za Zanzibar zilizokuwa zikiandikwa hasa kwamba imeanza na historia, utangulizi, imeweka mambo katika muktadha wake kabla ya kuchambua yale ambayo walipewa kazi kuyafanyia kazi na mwisho imetoa hitimisho zuri sana katika maeneo mbali mbali. Kwa hivyo, mimi napongeza sana kazi hii ambayo imefanyika.

Mhe. Naibu Spika, niombe kabisa jana Mhe. Mwenyekiti, katugaia hapa baada ya kuitaja katika ripoti, nakala za ripoti ya kamati ambayo iliundwa kwenda kuchunguza mgogoro wa ardhi Vitongoji iliyokuwa ikiongozwa na aliyekuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar zama hizo Sir John Grey.

Tumeipata, tumeletewa na tutapata kuitumia kama ni rejea kwa sababu imechapishwa. Niombe Mhe. Naibu Spika, ripoti hii kwa sababu inagusa suala zito na muhimu sana la ardhi, basi Baraza lako lichapishe kijitabu sio kama hivi ilivyo sasa hivi, ripoti yenyewe na vielelezo vyake vyote ili ikae katika kumbukumbu za Baraza na kumbukumbu za nchi hii kwa ajili ya kufanya rejea huko siku za mbele.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika maudhui ya Kamati na nitakuomba univumilie kidogo ili niseme yale ambayo nimekusudia kuyasema katika mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, la kwanza kabisa na mimi niungane na Kamati kwamba mgogoro wa ardhi katika dunia hii si jambo la leo wala jana, na katika nchi hii ina historia refu sana, na siku zote limekuwa ni sababu ya mitafaruku.

Mhe. Naibu Spika, mara nyengine jamii zimegongana na kutuhumiana za Zanzibar hizo, kwa sababu ya suala la ardhi. Mhe. Naibu Spika, ninayo hapa *hansard* ya *LEGICO*; Baraza la Kutunga Sheria la *Legislative Council* ya mwaka 1933 hadi 1934.

Katika kikao cha tarehe 29 Juni, 1934 serikali iliwasilisha mswada wa kufanya marekebisho katika sheria inayoitwa *the violation of land, restriction and evidence bill 1934*. Katika sheria hiyo Mhe. Naibu Spika, serikali ya Kikoloni ilileta sheria ambayo iliwabana wale waliokuwa wakikopesha fedha; *money lender* ambao wengi walikuwa wana asili ya Kihindi, kuwaambia kwamba hawawezi kutumia kutokuelewa au maarifa duni ya jamii za watu wenye asili za Kiafrika na Kiarabu ambao huenda wakaweka mashamba yao rehani, wakaingiza katika masharti magumu na baadae wanaposhindwa kutimiza wakachukua ardhi zao.

Wakapeleka sheria kuzuia au kuweka vizingiti fulani juu ya kutekeleza suala hili. Lakini likazua mzozo Mhe. Naibu Spika, na mmoja katika aliyechangia alikuwa bwana mmoja akiitwa Mr. B. H. Wiggins ambaye aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar zama hizo, lakini wakati anachangia alikuwa si Mwanasheria Mkuu tena, lakini ni Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria la *Legislative Council.*

Katika mchango wake sitaki kuusoma kwa urefu lakini kuna sehemu anasema, ninanukuu Mhe. Naibu Spika,

> *""In the first place it would seem to an impartial outsider that the present Government, and by the present Government I mean the Government since Sir Richard Rankine came into power, has been either consciously or subconsciously definitely anti-Indian. This feeling has increased each year until we have reached the climax by the introduction of this Bill which is obviously drawn up with a view to relieve the Arab and Native from what the Government consider is the stranglehold of the harsh and unconscionable Indian Moneylender"*

Kwa kifupi anasema kwamba kashuhudia kwa miaka kadhaa tangu imekuja serikali chini ya huyo aliyekuwa Balozi Mkaazi wa Uingereza Sir Richard Rankine kwamba imekwenda na sera za kuwaonea au kuja na msingi ambao ni dhidi ya raia waliokuwa na asili ya Kihindi.

Na akasema imefikia kilele kwa mswada kwa mswada huo kwamba serikali inataka kuwatetea jamii za asili ya Kiarabu na wenyeji dhidi ya hawa wanaonekana wakopeshaji fedha wenye asili ya Kihindi ambao hawawatendei haki watu hawa.

Kwa hivyo anaituhumu serikali katika masuala ya ardhi kwamba inataka kuwaonea hawa wanaotaka kukopesha pesa zao kwamba ni haki yao kuchukua ardhi ile, kwa hivyo suala lilikuwa mwaka 1934 lilijitokeza.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi sana nitakuja suala na nitawaonesha kwa nini anazungumza haya katika muktadha wa ripoti hii. Katika mwaka 1950 aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria la *Legislative Council* Sheikh Ameir Tajo alipeleka suala serikalini. Katika kikao cha tarehe 11 Disemba, 1950 na *hansard* yake hii hapa Mhe. Naibu Spika, akauliza na ninaomba:-

"*THE HONOURABLE AMEIR TAJO asked:*

(19)(a) Has His Highness' Government possessed any piece of land in the Town area;

(b) If the answer to (a) is in the affirmative, how many acres do they occupy and in what areas are they situated;

(c) Of those Government lands, how many plots were sold to people or given to them as gifts?

Anaulizia kwamba je, serikali ya Sultan inamiliki sehemu yote ya ardhi katika maeneo ya mji, na kama jibu ni ndio ni eka ngapi ambazo wanazo na katika maeneo gani zipo, na katika maeneo hayo ya ardhi ya serikali ni maeneo mangapi ya ardhi yameuzwa au kutolewa kama ni hiba kwa watu mbali mbali. Sasa serikali inajibu nini Mhe. Naibu Spika,

> THE HONOURABLE THE CHIEF SECRETARY replied:-
> *"The information sought by the Honourable Member will be furnished in due course if practicable in the form of a written reply"*

Kwamba jawabu italetwa kwa maandishi.

Sasa katika *hansard* hii hii baadae likaletwa hilo jibu la maandishi linafurahisha sana Mhe. Naibu Spika, na haya yanayoendelea leo. Linasema nini Mhe. Naibu Spika? Baada ya kuambiwa atajibiwa kwa maandishi, jawabu la serikali ni hivi limeambatanishwa kama ni kiambatanisho huku mwisho.

Inasema: - *"The following is the Government reply:-*

> *It has been found that it will not be possible to obtain the information required by the Honourable Member without considerable expenditure of both time and money. Government is unaware of any public advantage to be gained by this information which would justify such expenditure"*

Yaani inasema serikali imeona haitoweza kupata taarifa hizi bila ya kupoteza muda na gharama, wala serikali haijui faida yoyote ya umma ambayo itapatikana kwa kuingizwa kwa gharama hizi kutafuta taarifa hizi ambazo Sheikh Ameir Tajo kaziuliza mwaka 1950.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nimeyataja haya kwa sababu kwanza inaonesha suala la umuhimu wa kujua ardhi inamilikiwa na nani, ninadhani limekuwepo katika nchi hii kwa muda wa miaka mingi sana.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Kamati katika ripoti yake imetutolea tu historia nzuri sana ya migogoro ya ardhi huko nyuma. Lakini kamati ikatuonesha mwisho kwamba kilele cha yote haya ilikuja pale tarehe 8 Machi, 1964 Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar Marehemu Sheikh Abeid Aman Karume alipotangaza katika uwanja wa Cupas kwamba ardhi yote kuanzia siku ile ni mali ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, uamuzi ule haukufanywa tu kwa sababu labda ya jumla jumla, maelezo yake yameelezwa vizuri katika viambatanisho ambavyo katika ripoti hii vimetajwa. Mhe. Naibu Spika, kiambatisho KTA 1B inaelezea gazeti la Serikali la Kweupe, kwa nini serikali ikachukua hatua hii.
Inasema;

> "Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar imechukua hatua hii kwa sababu ya kuwasaidia maskini wote, tumechukua hatua hii kwa manufaa ya umma, watu wengi sana wa nchi hii hawana ardhi, na ardhi yote imechukuliwa na watu kidogo tu, mabwana wakubwa wakubwa, kwa hivyo hatua hii ya kwanza kuichukua ardhi yote itafuatwa na hatua nyenginezo ambazo zitamsaidia kila mnyonge na maskini yeyote yule aweze kuishi maisha bora"

Sasa Mhe. Naibu Spika, huko ndiko tulikotoka. Na katika ripoti hii hii katika kiambatanisho cha mwanzo kabisa tumeoneshwa orodha ya watu 74 au familia 74 tu, ambazo zikimiliki jumla ya mashamba makubwa 745 katika nchi hii. Yamechukuliwa na serikali, lengo lake ni lile limeelezwa katika gazeti la Kweupe baada ya tarehe 28 Machi, 1964.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ninachokiona leo baada ya ripoti hii kuletwa hapa na yanayoendelea huko mitaani, ni kwamba kama sababu kubwa ya kufanywa Mapinduzi kama ilielezwa ilikuwa ni suala la ardhi na watu wengi kukosa ardhi na watu wachache kuimiliki. Mhe. Naibu Spika, naogopa kwamba vitendo vya serikali yetu na viongozi wake ambao hawana huruma na wananchi wanyonge maskini wa nchi hii inaturejesha kule kule. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, tumeelezwa hapa na Kamati kwamba sheria zetu zipo wazi kwamba kila mwananchi anaruhusiwa kuwa na ardhi mbili kwa mujibu wa Kifungu cha 39 cha sheria ya ardhi. Ardhi moja katika eneo lake alipo na eneo moja katika sehemu nyengine. Lakini vile vile anaruhusiwa na ardhi nyengine moja tu ya kilimo. Halafu pakatajwa kuwa na ardhi kwa ajili ya biashara au viwanda, lakini hilo kwa mujibu wa sheria hii ni lazima ipitie ZIPA na upate kibali cha ZIPA.

Mhe. Naibu Spika, katika buku hili viambatanisho vimeonesha humu na ripoti imeeleza kwamba sasa badala ya lile lengo la Mzee Karume kwamba ardhi wapewe watu wananchi wanyonge kuwasaidia kuwanyanyua maisha yao, ardhi inamilikiwa na wanasiasa na watendaji wa serikali. Tumeona Mhe. Naibu Spika, humu kwamba Mawaziri wamo humu, Wawakilishi wamo na wengine tumo ndani humu humu, Wakuu wa Mikoa wamo humu, Wakuu wa Wilaya wamo humu, Maafisa Tawala wamo humu, Wakuu wa Vikosi wamo humu, habari za ulinzi na usalama zimo humu na Wakurugenzi waliokuwepo katika sehemu za ardhi na Maafisa Wadhamini wamo ndani wamechukua ardhi. (*Makofi*).

Mimi Mhe. Naibu Spika, moja ambalo nitamuomba Mhe. Waziri, akija atwambie. Hebu tuanze uhakiki humu ndani kwanza, humu ndani ya Baraza la Wawakilishi tuliomo, tuanze humu tuliomo ndani. Kuanzia Makamu wa Pili wa Rais mpaka Mawaziri, mpaka sisi Wawakilishi wa kawaida hebu tufanyiwe hesabu atakapokuja kutoa jawabu ya serikali kujibu hoja ya Kamati hii, tuje tuambiwe kila mmoja katika sisi anamiliki ardhi kiasi gani katika nchi hii. (*Makofi*).

Je, kweli hakuna aliyezidisha viwanja viwili kupewa katika historia yake yote, kwa sababu hakuna viwanja kwamba nimekuwa Mwakilishi tu, viwanja viwili kwa mwananchi kwisha tu, iwe Mwakilishi si Mwakilishi, uwe Waziri si Waziri, uwe Makamu wa Pili wa Rais si Makamu wa Pili wa Rais, uwe Rais si Rais, uwe Makamu wa Kwanza wa Rais sio Makamu wa Kwanza wa Rais, ni viwanja viwili vya kujenga na ardhi moja ya kilimo. (*Makofi*).

Sasa tufanyiwe hesabu na ninaomba Mhe. Waziri, akija hapo atakapokuja kujibu ripoti rasmi ya serikali baada ya kupitishwa, ninaamini itapitishwa ripoti hii, aje atwambie hivyo. Na vile vile, tunamdai Mhe. Waziri nilizungumze kabisa hapa, alitwambia katika kikao mwaka huu huu mwanzoni, kwamba katika eka ilikuwa sheria ni kwamba mtu anaruhusiwa kumiliki eka tatu alizopewa. Lakini kanithibitishia yeye kwamba wapo waliozidi na alitwambia atakuja kuwataja, hakuwataja mara hii, naomba atakapokuja kujibu ripoti hii aje atuletee orodha ya viongozi ambao wanamiliki zaidi ya eka tatu.

Mhe. Naibu Spika, yapo maelezo na watu wanajua kwamba nchi hii ni ndogo. Kuna viongozi wana ardhi Selem pale eka 30, wengine eka 14, wengine wana Selem, halafu ana na Kiboje eka 40 kakusanya kiongozi. Lakini kuna wananchi humu hata nusu eka hana.

Tunagawana viwanja vya kujenga humu kila kinapotolewa wanasiasa wamo, wakigawanywa Matemwe wanasiasa wapewe, vikigawanywa Tumbe

wanasiasa wapewe, vikigawanywa Tunguu wanasiasa wapewe lakini kuna wananchi humu, na niliwahi kutoa kadhia moja humu ya mwananchi wa Mji Mkongwe, kaomba kiwanja na barua nikamkabidhi Mhe. Waziri wa Ardhi tangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna hapa, kaomba tangu 1980 ile barua ya kuchapwa kwa *typewriter* ya zamani mpaka leo hajapewa kiwanja, lakini kuna watu humu hawajaomba wamepewa ripoti hii inaonesha Mhe. Naibu Spika. Hawakuomba katika eneo la Vitongoji tumeoneshwa humu, aliyeomba ni mwananchi mmoja na Kamati inasema hata yeye fomu yake ilikuwa na mashaka mashaka, lakini angalau huyo mmoja kaomba.

Na ushahidi kwamba angalau kaomba kama kapita *ZIPA* lakini akasema atafanya uwekezaji. Lakini wengine hakuna barua za kuomba wamepewa humu, wamo ndani Mhe. Naibu Spika. Sasa nitatoa ushauri Mhe. Naibu Spika, kwamba tumemwambia Mhe. Waziri, tunategemea akija atupe maelezo hayo, tuanze humu ndani kujuana, halafu tuwajue hawa waliotajwa humu ndani. Wananchi watatoa hukumu Mhe. Naibu Spika, na ninasema tusiwafikishe pahala yakawa mambo haya ni siri, nimetoa makusudi nimenukuu kauli ya Mhe. Ameir Tajo mwaka 1950, kwamba anaomba maelezo, serikali ya Kikoloni imekataa kumjibu, imemwambia haioni *public interest,* hakuna maslahi ya umma, leo katika Serikali ya Jamhuri ya Wananchi wa Zanzibar hakuna maslahi ya umma, wananchi wa Zanzibar kujua ardhi yao inamilikiwa na nani na inamilikiwa vipi. Tuelezwe Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, nimesema ile orodha aliyoitaja Mhe. Ali Mzee Ali, imo ndani ya kitabu hiki hapa, ya wananchi 74 au familia 74 zilizokuwa zikimiliki ardhi kabla, mashamba 745 imo ndani ya kitabu hiki na kishoka cha *Afro*-Shirazi kipo hapa hapa juu. Hoja yangu ni kwamba ikiwa zimetoka familia 74 za wakati ule, sasa kuna familia 74 mpya chini ya Serikali ya Jamhuri waliojiita wananchi, wana uchungu wa nchi hii Mhe. Naibu Spika, hatufiki. (*Makofi*).

Halafu Mhe. Naibu Spika, hawa hawa au sisi tunapanda juu ya majukwaa tukawadanganye wananchi tuwatumilie kwamba wakija hawa ardhi zitachukuliwa, zirejeshwe kwa wenyewe, zitachukuliwa zipo wapi na zote mushazimaliza? na ushahidi huu hapa Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nasema ni muhimu sana hilo kulitazama. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ni fundisho katika ripoti hii. Ilipotajwa migogoro ya ardhi Mhe. Rais alipoanza kuingia, huyu wa Awamu ya Saba alisema walioanza migogoro hii waimalize wenyewe. Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo yaliyokuwemo humu ndani aliyeanzisha migogoro hii hawezi hata siku moja akaimaliza mwenyewe. Kwa sababu wengine humu wamepewa

ardhi wala hawakujenga, wameshauza, wameshachukua fedha. Huyu aliyeuziwa baadae ndio anakuja kufutiwa hati ya kumiliki, huyu aliyekwishachukua pesa, je, Unamwambia hawa wakamaliza matatizo haya, hayawezi.

Nimuombe Mhe. Rais katika hili arejee tena kauli yake, ripoti hii ifanyiwe kazi na serikali tuje tupewe maelezo. Yale yaliyotajwa humu na mengine yaliyokuwepo nje ya humu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala jengine limenishtua na hivi naomba niiambie serikali. Ni kuonesha katika ripoti hii haidhuru inaonekana labda watu wengine hawakuiona, kuna sehemu katika ripoti hii Mhe. Naibu Spika, inaonesha kwamba sitaki kutumia kutoa taarifa za uongo, lakini ninataka kutumia hiyo hiyo kwamba viongozi, Mawaziri wa Serikali katika Baraza hili hawatwambii kweli humu ndani.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 9 wa ripoti umezungumzia kadhia hii ya Bwana Ali Murad. Kwenye ukurasa wa 9 imeonesha taarifa iliyotolewa ndani ya Baraza na Mhe. Waziri, kwamba suala hili limekuwa limeshamalizika na kwamba wenyewe wameelewana baada ya huyu Bwana Murad kukubali kufidiwa ardhi sehemu nyengine.

Lakini ripoti ya Kamati imethibitisha kwamba Bwana Murad hakuridhika na kenda mbele ya kamati, katoa ushahidi na vielelezo. Sasa yale majibu aliyotupa Mhe. Waziri, katika Baraza tuyahesabu vipi Mhe. Naibu Spika. Na ninapata wasi wasi kwamba hili linajulikana lakini na majawabu mangapi tunajibiwa na Baraza hili kwamba jee, yanaakisi uhalisia wa mambo au watu wanaondoshwa njiani ndani ya Baraza hili? Mhe. Naibu Spika, ninafikiri la pili serikali ijifunze katika ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, suala la Kisiwa cha Kwale. Katika ukurasa wa 24 wa ripoti Mhe. Naibu Spika, hili kamati imelipitia. Mwisho maoni ya kamati yakasema kamati inapendekeza kuwa taratibu zinazohusika katika suala hili ziharakishwe katika kuchukua hatua ili kulimaliza suala hili kwa manufaa ya nchi.

Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, aje alitazame tena. Wananchi ambao wanakitegemea Kisiwa cha Kwale wana malalamiko ya msingi na hawaridhiki na suala la kisiwa hiki kutolewa kwa mwekezaji. Na haiwezekani katika yale niliyozungumza mwanzo ikawa mwekezaji anataka kupewa haki zaidi na hali zaidi kuliko wananchi wanaofaidika katika eneo lile. Kwa hivyo, nilikuwa naomba serikali ilitazame tena, kamati imeitaka serikali ilifanyie

kazi, naomba serikali itakapolifanyia kazi izingatie maslahi ya wananchi ambao wanakitumia kisiwa kile cha Kwale.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nimeliona humu na ninaomba wizara ilitupie jicho la karibu sana ni suala la kodi za ardhi. Imeeleza Kamati humu kwamba kuna kampuni zimefutiwa. Kwa mfano Kampuni ya *Sunset Paradise* ilikuwa ikilipa dola 39000 $ kama kodi ya ardhi. Lakini imefutwa kapewa mwengine analipa dola 2500$. Sasa ninajiuliza huyu aliyefuta katafuta maslahi ya nani hapa, mbali ya suala la kwamba kaendeleza au hakuendeleza, ile kama nchi kufaidika, hivi baina ya dola 39000 na dola 2500, nchi inafaidika na zipi zaidi ya hapo. Ufute ardhi ambayo kodi yake dola 39000, umpe mtu mwengine kwa dola 2500.

Naomba litazamwe tena. Na hili Mhe. Naibu Spika, linaambatana na *formula* ambapo kamati pia imetaja. *Formula* ya malipo ya kodi kwamba haipo. Tumeona ardhi zenye ukubwa tofauti zinalipwa kodi ambazo hazilingani, ardhi kubwa kodi ndogo, ardhi ndogo kodi kubwa. Hakuna *formula* inayolingana.

Na hayo Mhe. Naibu Spika, yametajwa hata katika ripoti hii ya Mkaguzi. Tunasubiri itakapokuja kujadiliwa kwa kina, lakini imo humu ndani katika ukurasa wa 47 ya ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012 pamoja na ripoti ya ukodishwaji wa ardhi kwa wawekezaji, imeonesha maelezo hayo.

Na wakati fulani Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikichangia niliwahi kusema humu ndani kwamba zipo taarifa kwamba mara nyengine kunakuwa na maelewano baina ya watendaji wa mamlaka zinazohusika, idara na wawekezaji, kwamba wanalipa tofauti lakini zinaingia mifukoni, lakini huku katika risiti zinaoneshwa zinazolipwa ni tofauti yapo hayo.

Mhe. Waziri atupie jicho hayo, katika kamati nimeshawahi kumwambia na leo ninarejea tena ndani ya Baraza humu ili watu wote walisikie Mhe. Naibu Spika, kwamba tuna tatizo hilo kubwa sana. Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, limeonekana humu kwamba katika serikali hakuna nidhamu za kiutawala, limeonekana humu. Vipi Mhe. Naibu Spika.

Kwa mfano kesi ya Bruno iliyotajwa kwenye ukurasa wa 28. Unaambiwa kwamba imefutwa tarehe 6/06/2011, lakini barua au hati ni tarehe 13/06/2011. Yaani imekwenda baadae, kuna mgongano. Lakini kuna mengine yameoneshwa humu. Kuna kwa mfano Kampuni ya *The Address* eneo la Matemwe. Hapa pia Mhe. Naibu Spika, pana kitu cha ajabu sana. Hii

inaonesha jinsi gani mpaka mtu unakuwa Waziri lakini huna uaminifu kwa nafasi yako kinyume na kiapo ulichokula katika nchi hii Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, tumeona humu ukitazama ile orodha iliyogaiwa ardhi Matemwe pale ambayo imenyang'anywa kwa mwekezaji mmoja, kapewa mwengine, unaweza kudhani kwamba wamepewa watu tofauti, kumbe ukija ukifanya utafiti na vielelezo viliomo humu ndani, vyote kapewa mtu mmoja au familia moja.

Kuna ardhi ambayo imetolewa kwa kampuni ya *The Address* ambayo baada ya kufuatiliwa na kamati, imethibitishwa kwamba tarehe yake ya usajili ni baada ya kupewa, na hiyo tarehe wameiomba kutoka katika Mrajis Mkuu wa Biashara za Serikali. Kwa hivyo, ni taarifa rasmi ya serikali. Lakini nani wenye hisa katika kampuni hiyo, ni Saleh Mohamed Said na Elizabeth Mayala.

Halafu mbali ya hao, nani sasa waliokuja kupewa haki ya matumizi; *occupancy*, ile kwanza wamepewa kama ni uwekezaji, halafu eneo hilo hilo wamepewa hati ya matumizi ya ardhi, nani wamepewa? Saleh Mohamed Said kapewa moja na Elizabeth Mayala kapewa moja, hawa ni mtu na mama watoto wake.

Mhe. Naibu Spika, siamini mimi kwamba Waziri aliyefanya mambo haya kwamba alikuwa hayaoni haya, ikiwa nimeyaona mimi nobe, Jussa. Nimepitia haraka haraka tu kwa jana moja sijapewa nyaraka nipitie, nimeweza kuyaona hayo kwamba aliyesaini huku na kushuhudia ni yule yule na aliyepewa hati, vipi unahalalisha eneo lote umemnyang'anya mtu mmoja mwekezaji kwamba hakuendeleza, halafu wewe unafanya mambo kama haya, halafu bado tuseme Mhe. Naibu Spika, watu kama hawa kwa viapo wanavyovila wana haki ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Kweli wana uchungu na wananchi wa Zanzibar hawa?

Mhe. Naibu Spika, bahati mbaya ni mengi na muda unasonga, lakini jengine ambalo linanishughulisha sana, ni suala ambalo watu kupewa viwanja. Mtu pengine umepewa kwa taratibu halali ikiwa ni mwananchi au kwa mwekezaji, lakini hasa viwanja vya kwenye fukwe. Nchi yetu ni visiwa, maisha ya wananchi wanategemea bahati. Kuna wavuvi, kuna wale wanaolima mwani.

Leo watu wanagawana viwanja halafu anatia kuta anaunganisha pengine baina watu wawili tofauti au baina yeye mwenyewe peke yake, halafu anaziba njia wananchi wenye nchi hii anawazibia njia kufika katika bahari. Yapo kila pahali Mhe. Naibu Spika, kwa Unguja na Pemba yapo haya.

Hii kweli haki na wasimamizi wa sheria, serikali ipo wapi? Haya Mhe. Naibu Spika, yapo hata katika maeneo haya haya ya karibu karibu. Kuna suala hapa Mbweni hapa tunapozungumza. Huko nyuma watu walikuwa wakifanya wanavyotaka lakini kuna mtu hapa ana viwanja, kanunua kiwanja kimoja na kanunua cha pili, sawa una pesa zako umenunua. Ingawa Mhe. Waziri, katwambia hakuna haki ya kununua ile haki ya kutumia, unachoweza kununua ni kitu baada ya kuona kimeshajengwa juu ya ardhi, katwambia Mhe. Waziri wa Ardhi hapa.

Lakini baina ya kiwanja hiki na hiki, hapa mbele Mhe. Naibu Spika pana barabara katika ramani ya serikali. Yeye huyu anataka kuunganisha kiwanja chake hiki na hiki na barabara atie kati kati afungie wananchi njia ile. Yapo hayo Mhe. Naibu Spika, katika nchi hii. Sasa haya yapo katika maeneo haya, leo ramani za miji zitakaa wapi, tutazungumza miji iwe na haiba, tutatoa haiba ikiwa kila mtu mwenye pesa ana nguvu anafanya anavyotaka Mhe. Naibu Spika, huyu mnyonge ambaye Azimio la tarehe 8 Machi, 1964 alisema Mzee Karume kwamba anataka kumkomboa, tunamkomboa kweli?

Ndio nikasema kama kulikuwa kuna familia 74 zitakuja nyengine na ilikuwa ndio sababu ya kufanya Mapinduzi tusije tukashangaa wananchi wakaja wakatafuta hatua nyengine, kwa sababu yale yaliyosababisha Mapinduzi 1964 tunayarejesha tena sisi wenyewe Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hili litizamwe sana na serikali, maeneo ambayo yanafunga njia, kwa sababu tu mtu ana fedha na mengine Mhe. Naibu Spika, tushajidhalilisha.

Kuna kesi ameitaja Mhe. Hamza Hassan Juma, sana hapa ya *Cristal* katika eneo la Paje. Mimi karibuni nilikuwa semina kule nikacheka. Nikasema ndio maana wanatumiwa kwa mambo haya. Nimekuta pale polisi usoni mwake, nimekuta *Cristal* kajenga nyumba za polisi katoa msaada kwa polisi. Mimi imani yangu ni kwamba wananchi wanapopeleka malalamiko yao kwa polisi hayachukuliwi hatua, watachukua wapi hatua wakati wameshafadhiliwa wamejengewa nyumba.

Sasa kama wamesaidia maendeleo ya nchi ni sawa, lakini isiwe ndio sababu tena ya kuwanunua wasimamizi wa sheria ikawa tena wao hawawezi kuchukuliwa hatua Mhe. Naibu Spika, haikubaliki, ndio malengo ya Mapinduzi hayo.

Mhe. Naibu Spika, mengine nimeshayazungumza sitaki nipoteze muda mrefu sana. Lakini kuna eneo jengine ambalo limetajwa humu ni suala la majenzi ya *jetty* ambalo linahusika na hifadhi ya mazingira. Imeshatolewa kauli ndani ya Baraza hili hili kwamba kwa mujibu wa sheria zetu, huwezi kujenga ndani ya fukwe au mita 30 kutoka kwenye fukwe. Lakini Mhe. Naibu Spika, bado

tunashuhudia wanakuja wawekezaji wanaendelea kujenga na ma-*jetty* yanaendelea kujengwa.

Mhe. Naibu Spika, visiwa vyetu kila siku tunaambiwa athari yake katika uharibifu wa mazingira, lakini watu wanaendelea kufanya wanavyotaka tu, hii nchi haina mwenyewe Mhe. Naibu Spika, hivi hawa wanaokuja kutufanyia mambo haya, sisi tunaweza kutoka tukaenda katika nchi zao tukafanya mambo kama haya. Hivi Mhe. Naibu Spika, mimi naweza kutoka nikaenda Italy nikafanya ninavyotaka. Kwa nini tuonekane kwamba tumetiwa mikononi mwa wawekezaji, kwa nini Mhe. Naibu Spika?

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba ripoti hii ni muhimu ifanyiwe kazi. Kama nilivyosema Mhe. Waziri, ana kauli zake, *hansard* hii hapa ya tarehe 9/10/2013 tulipokuwa tukijadili mswada wa marekebisho ya sheria ya ardhi. Iko *hansard* yake ya nyuma alipotoa kauli ile kwamba mtu haruhusiwi kuuza kiwanja. Wangapi tunachukua ardhi halafu tunauza kabla ya kuziendeleza, ndio hii tunapiga foleni kila baada ya kugaiwa viwanja sisi tuko wa mwanzo, sio kwa sababu tunataka kujenga imekuwa ni mradi. Ilizungumzwa humu katika kamati kwamba viwanja vimekuwa pesa sasa hivi.

Kwa hivyo, tunamtegemea Mhe. Waziri, atakapokuja kama nilivyosema, nasisitiza tena Mhe. Naibu Spika, kwamba aje atuletee orodha, aanze na humu ndani, kuanzia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mawaziri mpaka watu wa kawaida. Tunamiliki ardhi kiasi gani, tunafuata sheria, halafu aje atumalizie na wale ambao wametajwa katika ripoti hizi. Halafu aje atuambie na wale aliotuambia kwamba anawajua wakubwa ambao wanamiliki eka zaidi ya vile walivyoruhusiwa na sheria, pia alituambia atatuletea, tunamngoja atakapokuja kujibu hoja za ripoti hii tutazitaka Mhe. Naibu Spika. Vyenginevyo tunamuambia kama bajeti ya Mawasiliano katika kikao kilichopita ilipitishwa na Spika, na yake yeye labda ategemee rungu la Spika, lakini sisi tutaikataa humu ndani kama haina majibu haya.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa wenzangu walizungumza na mimi nataka kulizungumza. Hii dharau inayooneshwa na watendaji wa serikali dhidi ya chombo hiki na Wajumbe wake. Ripoti hii Mhe. Naibu Spika, pamoja na uzuri wake, basi ingekuwa nzuri zaidi hii ingekuwa imekamilika. Lakini sio sehemu moja, sio sehemu mbili wala sio sehemu tatu, inasema kwamba wametaka vielelezo wizara imekataa kuwapa, mimi nasema imekataa, kwa sababu mpaka barua zao za kukumbusha wameziorodhesha humu ndani, bado serikali imekataa kutoa.

Mhe. Naibu Spika, jana Mhe. Salmin Awadh Salmin kasema, na mimi leo nataka kuongezea kwa kukinukuu kile kifungu hasa. Mhe. Naibu Spika,

kifungu cha 18(3) cha sheria ya haki, kinga na fursa ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, sheria nambari 4 ya mwaka 2007 inasema;

Kifungu cha 18(3);

> "*Subject to the provisions of subsections (1) and (2) of this section, any person who refuses to be examined before or to answer lawful"* narudia tena *"or to answer lawful and relevant questions put by the House or Committee unless such refusal be excused as herein before provided, commits an offence and shall on conviction be liable to a fine not exceeding fifty thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding three years or to both such fine and imprisonment*"

Ni kosa la jinai, ni tofauti na kile kifungu cha 9 ambacho kimetoa haki ya Mjumbe, ambacho kinasema;

Kifungu cha 9;

> "*Subject to this Act and to any statute relating to security of the government,a member shall be furnished by the public Officer Concerned, any information he requests"*

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kwa bahati mbaya hakikuwekewa kosa kama Mjumbe kaomba hakupewa taarifa ni kosa, lakini kile kifungu cha 18(3), ikiwa Baraza au Kamati ya Baraza imekutaka ukatoa ushahidi au ukatoe taarifa yoyote kwake na ikiwa hujatoa ni kosa la jinai.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hili liko juu ya kiti mnachokikalia hapo. Ili kurejesha heshima, asubuhi nilisimama kuomba utaratibu kuhusu majibu tunayojibiwa. Naomba tena mimi kama kuna mtu anajiona hawezi kutumikia Unaibu Waziri kujibu maswali yetu, basi amuambie Mhe. Rais ampumzishe, hatakuwa na haja ya kutushikia kiuno sisi na kutunyooshea kidole. Kama kachoka amuambie Mhe. Rais kuwa mimi siwezi kujibu maswali ya wala mule ndani naomba unipumzishe.

Lakini hilo mbali, utaratibu mwengine ni huu kwamba ili chombo hiki kiheshimiwe, nafanya utaratibu sasa kwamba hawataki kutoa taarifa kwa Baraza au kwa kamati na hayo yanaripotiwa na kila kamati inayokuja hapa ndani Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, imefika pahala kiti chako kichukue hatua ya kuiarifu mamlaka inayohusika ili mashtaka yaweze kupelekwa, tutoe fundisho kwa watu wengine kukiheshimu chombo hiki. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu

Spika. Nasema kwamba nilianza kwa kuipongeza kamati hii na namalizia tena kwa kuipongeza Kamati hii. Nampongeza Mhe. Ali Mzee Ali, kwa kuweka historia nyengine katika Baraza la Wawakilishi hili kwa ripoti yake hii.

Vile vile, naiomba serikali iipe uzito unaostahiki ripoti hii, wasidhani kwamba wanaweza kutuvurunga vurunga tu, wanaweza wakatupotosha sisi lakini wananchi wanasikia huko nje. Kama nilivyosema kikifika kipindi cha bajeti, kama hatukupata majibu ya kuridhisha katika haya, basi patakuwa na mbinde humu ndani juu ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na naiombea utekelezaji mwema. Ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili au matatu katika ripoti ambayo imewasilishwa na Mhe. Mwenyekiti Mhe. Ali Mzee Ali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mimi niendelee kukubaliana na wenzangu ambao wamenitangulia kuikubali ripoti ambayo imewasilishwa na Mhe. Ali Mzee Ali, katika Baraza letu hili tukufu la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ripoti hii iliyokuwa imewasilishwa hapa ni baadhi tu ya mambo, kesi na kadhia ambazo zinahusu sekta ya ardhi ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar. Lakini kwa sababu hapa ndipo pa kuanzia, ningeomba sana serikali tuanze basi kuchukua hatua kwa haya ambayo tayari yamekwishawasilishwa kwetu kwa mustakabali wa mambo ambayo Kamati Teule ilikuwa imeona.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo nasimama hapa kuzungumzia zaidi lile suala la vielelezo. Kwa kweli jana nilikuwa nimekaa kwenye kiti chako hicho Mhe. Naibu Spika, katika utaratibu wetu tuliokuwa tumejiwekea. Lakini ilipokuja hoja ya kwamba Kamati Teule imeshindwa kupata vielelezo, ndani ya wizara ambayo mimi naisimamia kama Mwenyekiti, kwa kweli nilishtuka sana na nikataka kupata ufafanuzi wa kina ambao utaweza kunitosheleza mimi pamoja na Wajumbe wenzangu, lakini na Wazanzibari wote kwa ujumla ni kwa sababu gani vielelezo vile vilishindikana kuwasilishwa katika Kamati Teule, kwa sababu suala la vielelezo ni suala ambalo linaweza kupelekea yale malengo ya utafutaji wa ile kadhia iliyokuwepo iweze kupatikana, na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria ambazo tulijiwekea.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile Mhe. Waziri, atapata fursa ya kuja hapa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo, atuelezee ni sababu zipi zilizosababisha vielelezo vile vikashindwa kuwasilishwa katika Kamati Teule.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, katika buku letu hili la taarifa huku mwisho kabisa kuna maelekezo ambayo yalitolewa na Mhe. Mwenyekiti wakati alipokuwa akiwasilisha ripoti yake. Mhe. Mwenyekiti, ripoti ile ilikuwa inasisitiza juu ya namna ya kufuata sheria na sera ambazo tunazo ili zitumike kwa maslahi ya nchi yetu. Ningependa kusema kwamba vyombo vinavyohusika na masuala ya sheria, ningewaomba sana tuanzishe utamaduni wa kufuata sheria bila ya kushurutishwa, ili tuweze kwenda kwa mujibu wa taratibu na hatua ambazo wenyewe tulikuwa tumejipangia.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nataka kuja katika suala la uvunjifu wa taratibu hizi za *plan* ambazo tunazitoa. Mhe. Naibu Spika, imekuwa ni mazoea, baadhi ya hawa wageni wanapokuja hapa nchini na wanapopewa maeneo yao kwa ajili ya maombi yao waliyoyaleta kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za uwekaji vitega uchumi ndani ya nchi yetu, huchukua na maeneo ya ziada. Maeneo hayo Mhe. Naibu Spika, hawachukui wenyewe, bali huwa wanapewa na baadhi ya watendaji katika taasisi zetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naungana na wenzangu katika kulifuatilia na kuona kuwa ile kadhia ambayo imejitokeza katika baadhi ya maeneo, wananchi wakakosa kupata maeneo ya kupita na badala yake wawekezaji hawa wakatumia kuyafunga maeneo yale, ili waweze kutimiza miradi yao ambayo walikuwa wamekusudia.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar bado ni kubwa na maeneo bado ni mengi, tungeomba sana wale ambao waliomba maeneo kwa ajili ya shughuli zao na wakaona kwamba maeneo yale waliyonayo hayawatoshi, basi waje katika serikali yetu, serikali yetu ni sikivu, tutawabadilishia maeneo mengine ili wafanye yale ambayo wamekusudia, lakini sio kufunga njia ambazo zinahusu na zinawapa kadhia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, katika kesi ambayo ilikuwa imetajwa na wenzangu ambao wamenitangulia hususan hii kesi ya Paje. Kuna kipindi tulipata maelekezo kutoka kwa hawa ambao wanamiliki hoteli hii ya *Cristal* na maneno yao ambayo hayana msingi, kwa kweli yalinisikitisha sana kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi katika wizara inayohusika.

Mhe. Naibu Spika, tatizo lililokuwa limejitokeza katika maeneo haya ya Paje, linahusu zaidi wananchi na tayari yule mwekezaji ambaye yuko pale amekwishavunja taratibu na sheria za nchi. Lakini wakati viongozi mbali

mbali walipokuwa wanakwenda kulifuatilia suala hili, basi wanadiriki hata kuwadhalilisha na kuwatukana wale watu ambao wanafuatilia masuala yale.

Sasa je, Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Waziri, hii nchi inamilikiwa na wawekezaji ambao wanakuja katika nchi hii au wanamiliki wenyewe wananchi ambao wamefanya Mapinduzi kwa sababu ya kujikomboa wao wenyewe.

Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, ile kadhia ambayo inawahusu wananchi wa Paje na maeneo mengine, yakiwemo maeneo ya Kilimani, Mbweni na maeneo mengine, yale matatizo ambayo yapo yanaikabili serikali kwa sasa, tunaomba sana kabla ya kuja hapa kuwasilishwa bajeti kwa wizara hii, basi matatizo yale yawe yametafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelekezo hayo, mimi niseme tu kwa mara nyengine tena kwamba ripoti ya Kamati ambayo imewasilishwa hapa mimi naikubali kwa asilimia mia kwa mia na naiunga mkono. Naiomba sana serikali iyachukue na ikayakalie kitako, lakini vile vile ikayafanyie kazi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na watu wote kwa ujumla. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika. Mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kikwajuni, naunga mkono ripoti hii. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima. Pia, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye ripoti hii muhimu ya Mhe. Sir Ali Mzee Ali.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi sina maelezo mengi, baada ya Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kutoa maelezo ya kina ambayo kwa kweli yametosheleza kwenye suala hili la ripoti ya Mhe. Ali Mzee Ali.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mhe. Ali Mzee Ali, kwa jinsi ambavyo wametuletea ripoti nzuri, yenye ufanisi mzuri na ripoti ambayo imeweka wazi misimamo ya Baraza hili.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, niwapongeze watendaji wote wa serikali ambao walitoa mashirikiano ya dhati kabisa, katika kufanikisha ufanisi wa ripoti hii, na leo ripoti hii inawasilishwa mbele yako kwa ajili ya kuwatetea Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaenda kwenye ripoti hii naomba serikali niikumbushe na niikumbushe kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, chini ya Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Mzee Ali amesema katika ripoti hii kwamba Baraza la Wawakilishi ni ngome ya wananchi. Hiyo ilitamkwa na Mhe. Aboud Jumbe Rais wa Pili wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nielezee kidogo tukio ambalo lilitokea asubuhi ili tuwaoneshe wananchi nidhamu ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, asubuhi leo tumeshuhudia kichekesho humu Barazani, nilikuwa najiuliza kama ni maonesho, ni rusha roho au ni mchezo wa kuigiza. Mimi binafsi Mhe. Naibu Spika, aliyefanya maajabu hayo ni saizi yangu wala hataki mwili, maana mimi kama nina kilo 40 na yeye ana kilo 40. Lakini hili ni Baraza Mhe. Naibu Spika, sio pahala pa malumbano.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya, leo aliyoyazungumza ni mambo ambayo yamemdhalilisha yeye, lakini yameidhalilisha Serikali nzima ya Mapinduzi ya Zanzibar. Imeonesha sura halisi kwamba uwezo wa Mawaziri ni hasira. Nimefanya utafiti mdogo tu, tangu asubuhi Mhe. Naibu Waziri wa Afya, alidhamiria na aliwaambia watu kwamba leo anakusudia kupambana na Wajumbe. Mimi ningejua kwamba hiyo ndio nia yake nisingemuuliza, maana mimi sina ubavu wa kupambana na Naibu Waziri.

Lakini ni jinsi gani serikali hii ilivyokuwa inaonesha kwamba ina udhaifu haiko pamoja na watu. Nimshauri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, awaangalie Wajumbe wake. Kama kuna Wajumbe ambao wamekesha kwenye mkesha wa rusha roho wa harusi, basi awashauri wasichangie Barazani wala wasiulize maswali. Nina wasi wasi ule mkesha wa rusha roho kule basi baadae Mjumbe anarudi Barazani anajisahau anaona kama yuko Bwawani kwenye Salama Hall.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri wa Afya, leo amenikopesha sindano na mimi iko siku nitamlipa mtaimbo mbele ya serikali hii. Mhe. Naibu Spika, wakati najibiwa majawabu yale, nimepokea *message* mbili. Moja kutoka kwa mzazi mmoja na moja kutoka kwa mfanyakazi mmoja wa Wizara ya Afya, ameniambia hayo ndio majibu ya serikali yetu chini ya Wizara ya Afya. Kumbe wafanyakazi wa Wizara ya Afya hawashangai majibu yale, kumbe ndivyo walivyozoea kujibiwa. Kwa hivyo, Mhe. Mohammed Aboud mimi nakushukuru unanikumbusha kwamba nimekopeshwa sindano, kuna siku utapokea mtaimbo kumlipa Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kusema kwamba ripoti hii naipongeza sana, na mimi sina wasi wasi na ripoti hii, wenzetu wamefanyakazi ya kina. Mimi nina neno moja tu kwa ufupi kwamba niliwahi kufanya ziara na Mhe. Hamza Hassan Juma, tuliamua kuondoka hapa kuelekea mashamba Kusini hadi Nungwi.

Tukaoneshwa maeneo ambayo wakubwa wa serikali hii wamechukua maeneo ya wananchi kinyume na utaratibu. Eneo moja ambalo tulitembelea ni hili eneo la Mr. Bruno, ambalo tuliambiwa wazi wazi kwamba huyo mchukuaji alikwenda sikukuu pili na gari yake na familia yake, akagawa pale zawadi za mjini, unajua watu wa shamba kwa zawadi ndio kawaida yetu. Pipi, keki, mambo ya soda watu wakagaiwa pale. Hatimaye siku ya pili eneo likapigwa *dozer* na akapewa aliyepewa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo mimi na Mhe. Hamza Hassan Juma tukaenda Nungwi, tukaoneshwa maeneo ambayo wamegawana watu wanne na yananadishwa kila moja dola 800,000. Dalali akatwambia kwamba nimeambiwa niuze dola milioni moja, wateja wangu wamefika dola 800,000 sijauza, Kwa hivyo, naomba nisaidiwe kwa sababu hili eneo bwana litachukuliwa. Nikamwambia mimi bahati mbaya si dalali wala sina uzoefu huo, lakini tuambie basi haya maeneo ni ya nani. Mhe. Naibu Spika, waliotajwa siku ile na dalali ni viongozi wa serikali hii na nusu na robo ni Mawaziri.

Je, kweli ni eneo lao, kwa bahati mbaya sikupata hati, lakini waliotajwa na huyo dalali ni viongozi wa serikali hii. Sasa ripoti hii Mhe. Naibu Spika, imenishtua sana. Humu aliyetajwa kuchukua eneo ni Mhe. Ali Juma Shamuhuna, kumpa mwanawe bwana Said. Nikajiuliza aah! Kwa kuwa Mhe. Ali Juma Shamuhuna, ni mfupi ndio akaonekana, kwa kuwa Shamuhuna keshakuwa kizee kidogo ndio akaonekana, na kwa nini eneo dogo la Mr. Bruno likaonekana mwanzo kuliko yale maeneo ambayo yananadishwa dola milioni moja.

Mhe. Naibu Spika, najua majibu ya Mhe. Mwenyekiti, ataniambia ni hadidu rejea. Lakini kama walichambua hoja za Wajumbe, *hansard* yangu ipo nilizungumza wazi wazi kwamba yapo maeneo yananadishwa kwa dola milioni moja, na kwa bahati mbaya hawakwenda.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati afuatilie kwa kina hoja hizi na afanye uchunguzi wa kina, ili kuokoa rasilimali za nchi ili wajanja wachache wasinufaike kwa mgongo wa wanyonge.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nikipongeze Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, mimi ni CUF lakini penye uzuri ni lazima tupongeze. Nachukua nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi CCM, na niipongeze Kamati Kuu ya CCM. Mjumbe wake tunaye humu ndani Dk. Salmin Awadh Salmin; Mnadhimu wa CCM.

Juzi Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi waliwaita Mawaziri saba, chini ya hoja ya Katibu Mkuu wa CCM kaka yangu Abrahman Kinana, kwamba mawaziri saba hao wahojiwe kwa kwenda kinyume na ilani ya CCM. Kumbe CCM bwana ina ilani nzuri sana, kwamba ukifanya kosa kinyume na utaratibu wa ilani unahojiwa. Lakini Mhe. Issa Haji Ussi Gavu, mara nyingi huniambia kwamba kuna CCM dume na CCM jike, kwamba kule Bara ni CCM dume na hapa Zanzibar ni CCM jike labda. Kwamba Bara labda ukifanya kosa...

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba sana swahibu yangu, rafiki yangu Mhe. Hija Hassan Hija, atuombe radhi sisi CCM hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, Chama cha Mapinduzi ni kimoja tu, na mimi niliyesimama hapa ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na alimtaja vile vile Mnadhimu wangu wa Chama cha Mapinduzi yeye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu, CCM ni moja hakuna jike wala dume.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba sana swahibu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, naomba afute kauli yake ya kusema kwamba sisi CCM Zanzibar ni jike. Sisi ni CCM dume, tena dume la mbegu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tukichangia yaliyokuwa hayahusu tusiyashirikishe, twende kwenye hoja ya kuchangia. Tunalidhalilisha Baraza letu, tuseme yale mambo ambayo tunayajua na yamo ndani ya *point* zetu. Sasa mkitia tena vionjo ndio vinaharibu. Kwa hivyo, futa kauli yako halafu uendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nimeombwa, na ukiombwa kama ni muungwana unakubali. Lakini ningeachiwa nimalize sentensi yangu ingekuwa raha zaidi, lakini nakubali kwamba CCM Zanzibar ni madume kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika: Endelea na mchango Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nilichokusudia kusema ambacho kidogo nimenyimwa raha, lakini kaka yangu Mhe. Hamza Hassan, hiyo ndio demokrasia napongeza sana, ahsante sana.

Hoja yangu ni kwamba Chama cha Mapinduzi kwa kupitia Kamati Kuu ya CCM juzi iliwaita mawaziri saba. Leo asubuhi nimemsikia Mjumbe wa kamati. Kama nitakosea naomba kuelekezwa, Katibu wa kamati ya Itikadi na Uenezi kaka yangu Nape Nnauye. Alihojiwa kwa nini mkawaita mawaziri saba. Ameeleza maelezo mengi ya msingi Mhe. Naibu Spika, lakini nimekamata manne kwa sababu nilikuwa sijaamka vyema.

Hoja ya kwanza ambayo alisema kwamba waliwaita kwa sababu wamedhoofisha ilani ya CCM kwa kupeleka fedha kidogo chini ya asilimia 40 kwenye miradi ya maendeleo. Nikajiuliza kumbe Waziri wa Fedha akipeleka fedha kidogo kwenye mradi wa maendeleo CCM hili wanakataa, ndio maana nikawapongeza sana kwa ujasiri wao.

Hoja ya pili Mhe. Naibu Spika, ni kwamba waliangalia ripoti ya *CAG* kwamba imetaja ubadhirifu na hakuna hatua iliyochukuliwa, napongeza tena.

Hoja ya tatu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hakuna hatua ndogo ambayo serikali imewachukulia wale wabadhirifu ambao wametajwa kwenye ripoti mbali mbali, kwa hivyo CCM kwa kupitia Kamati Kuu wakaamua kuwaita Mawaziri kwa nini mmechukua hatua ndogo kwa wabadhirifu waliotajwa.

Lakini hoja ya nne ambayo nimeikamata Mhe. Naibu Spika, ni kwamba walichukia Kamati Kuu urasimu na uhangaishaji kwa wawekezaji wageni unaofanywa na watendaji wa serikali Tanzania. Mhe. Naibu Spika, hii ndio CCM Kamati Kuu ambayo iliwaita mawaziri saba.

Mhe. Naibu Spika, nimejiuliza lipi kati ya haya hapa Zanzibar halipo, na kwa nini Chama dume hapa Zanzibar CCM hawajachukua hatua ya kuwaita, kwa nini? Kwa nini ilani ni moja upande mmoja uchukue hatua na upande mmoja kidogo uchelewe kuchukua hatua?

Mimi nikiombe Chama cha Mapinduzi, chama cha baba, maana baba yangu ni CCM sana. Niwaombe sana Chama cha Mapinduzi mfuate maelekezo ya ilani yenu na kwa maslahi yenu..

TAARIFA

Mhe. Mohammed Aboud Mohammed: Mhe. Naibu Spika, mimi namshukuru sana Mhe. Hija Hassan Hija. Mhe. Naibu Spika, ni vizuri kama ulivyosema tukasikiliza maelekezo yako. Mhe. Ismail Jussa Ladhu leo alikuwa akizungumzia sana kifungu cha 67 hapa, msingi wake tuweke heshima ya Baraza hili.

Sasa yeye Mhe. Hija Hassan Hija, hawezi kujua siri ya Chama cha Mapinduzi kinavyofanya kazi, kinavyowaita mawaziri wake, kinavyoita serikali na namna ya inavyosimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi. Ni vizuri akatoa mchango wake, asikizungumzie Chama cha Mapinduzi kwa sababu kina utaratibu wake, kinajua nini kinafanya Zanzibar na Tanzania. Kinajua utaratibu mzuri wa kusimamia mambo na ndio maana kimepewa heshima kubwa na wananchi kuitawala nchi hii.

Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Hija Hassan Hija, atoe mchango wake kusudi tusilete mivurugano na kuanza kuleta hisia ambazo si vizuri kuanza kuchanganyana wakati huu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hija Hassan Hija, naomba sasa uende kwenye ripoti yetu, mifano imeshatosha ya Chama, haya endelea kuchangia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, inaelekea hamtaki nichangie, mie sijaona siri, kama siri msingezitia kwenyevyombo vya Habari labda kwasababu nimesikia mie ndio imekuwa siri. Mimi napongeza hatua za Chama cha Mapinduzi, kama ni siri sawa nimefanya makosa.

Mhe. Naibu Spika: Pongezi zimeshatosha, tunashukuru na zimeshapokelewa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Vyenginevyo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anambie kama hataki niseme haya, basi aseme tu. Mhe. Naibu Spika, ninachosema *report* hii imemtaja Mhe. Ali Juma Shamuhuna, kuchukua eneo kumpa mtoto wake. Ni kweli mimi nimekwenda na Mhe. Hamza Hassan Juma, tumeona hilo eneo. Lakini namwambia Mhe. Waziri wa Ardhi, kwamba bado wapo watu kama hawa wakubwa zaidi ambao wana maeneo na ni lazima yatafutwe tuyaone kwa maslahi ya vizazi vyetu na maendeleo ya nchi yetu.

Report hii Mhe. Waziri, aifanyie kazi, aendelee kuwasikiliza Wawakilishi malalamiko yao na wananchi wa kawaida ili apate nafasi nzuri ya kufanya kazi kwa maslahi ya nchi hii na kwa maslahi ya vizazi vyetu. Isije tu ikachukuliwa kwamba *report* hii ikaonekana kwamba haya humu yaliyotajwa ndio tatizo la ardhi peke yake. Bado kwa maoni yangu kuna tatizo kubwa la ardhi ambalo bila ya kusimama imara kwa Mhe. Waziri, na watendaji wake basi ardhi Zanzibar itakuwa na ugomvi mkubwa.

Humu wametajwa watu ambao wamepewa ardhi wengine wana vipande vitatu, wangine vinne, lakini wamepewa. Bado hoja yao itakuwa wamepewa ardhi kihalali. Lakini kuna watu wamechukua ardhi bila ya utaratibu.

Namuomba Mhe. Waziri wa Ardhi, aandae utaratibu wa kuwataka wawakilishi wote kuanzia Masheha, Madiwani, Wawakilishi mpaka Mawaziri, kila mtu ataje idadi ya maeneo aliyoyamiliki na aeleze kwa vipi amemiliki eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna watu wamemiliki mashamba 70 na tukaamua kupindua, leo kwa nini tusitangaze mali zetu. Mhe. Waziri nakuomba sana uandae utaratibu kwamba kila Mwakilishi au kuanzia Diwani mpaka Mawaziri ataje eneo lake alilolimiliki na aeleze vipi amepata eneo hilo. Nina wasi wasi kwamba kuna watu wana maeneo makubwa, mengi na hawakuyatapa kwa utaratibu halali wa kiserikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa leo kaka angu Mhe. Muhammed Aboud (Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais) hataki nichangie vyema, ninachosema tu kwamba tatizo la ardhi lipo tena lipo sana ni robo tu ya *report* hii ambayo imeletwa hapa na lazima lishughulikiwe kwa upana wake. Vyenginevyo Mhe. Spika, Wazanzibari watakosa haki zao na kwa kweli watakuwa wanadhalilishwa.

Madhumuni ya Mapinduzi yatakuwa hayafikii lengo ikiwa hatukulinda ardhi yetu kwa maslahi ya watu wetu. Baada ya mchango wangu huo naomba niseme tu kwamba naunga mkono *report* hii na kama serikali ni waungwana wa kweli kweli basi naomba *report* hii ifanyiwe kazi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu na nchi kwa ujumla. Ahsante sana.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii kuweza kuchangia tatizo kubwa na sugu ambalo lipo nchini na linaendelea, suala la ardhi. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kutoa mchango wangu mzito kuhusu tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu hivi sasa imevamiwa sana na tatizo hili la ardhi. Hili suala tangu enzi ya ukoloni lilikuwepo. Liliwezekana kumalizika na likatolewa uamuzi wakati wa uhai wa Hayati Mzee Abeid Amani Karume 1964 alipotoa maamuzi ya kila mwananchi wa nchi hii aweze kupatiwa ekari tatu za kuweza kuishi yeye na familia yake. Mimi mwenyewe nilifaidika na hilo pamoja na familia yangu na hadi leo tunaishi bila ya matatizo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mwaka 1964 naona wazi serikali zote zilizopita hazikufuata nyayo za Raisi wa kwanza wa Zanzibar. Nasema hivyo kwa sababu awamu zote hazikutoa tena sheria ya umiliki wa ardí. Vyenginevyo wakuu wetu wanawapa mwanya baadhi ya wananchi wetu kujikatia mpaka mtu mmoja ana ekeri 20 bila ya hati miliki na bado serikali inamtizama tu. Naipa hongera sana awamu hii ya saba kuweza kulirudia hili suala la mwaka

1964, kwa kweli Rais Ali Muhammed Shein anastahili hongera sana na Waziri wa Ardhi, Maiji, Nishati na Ujenzi kuweza kulisimamia suala hili kwa vitendo.

Mhe. Naibu Spika, nikitizama nyayo za serikali ya awamu ya saba sijasikia Rais wetu ana ekari angalau 5. Ninamfahamu sana na Waziri wake namfahamu, wote ni watu ambao wanaishi katika jimbo la Koani, Rais wangu ana ekari tatu tu anaishi pale Kibele na nnamjua mpaka nyumba yake anayoishi. Waziri wangu na yeye pia sijamfahamu kuwa ana eneo jengine isipokuwa ekari tatu. Iweje viongozi wengine wa awamu ya sita, tano, na nne wawe na ekari 50, 60? Hii mimi naona inakwenda kinyume sana na ile Sera ya Raisi wa Kwanza kwamba watu wote wawe na ekari tatu tatu tu.

Ni vyema kuanzia sasa Waziri apitie upya mikataba ambayo imetiwa saini tangu awamu ya pili mpaka awamu hii ya sita, maeneo ambayo watu wameweka uzio, kuchukua nafasi za wananchi bure, sehemu zote hizo zirudi serikalini na zigaiwe kwa wananchi ili kila mwananchi aweze kupata ekari tatu na kupata kuishi na familia zao.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa mgogoro wa ardhi ni janga kubwa sana kwa nchi yetu na tukiliachia litazamisha nchi bila ya wenyewe kujua na halafu tutakuja kujikuta tuna mizozo mingi, tutakuwa sawa sawa na Rais wa Zimbabwe, Robert Mughabe alivyowaondoa Wazungu kwa nguvu hata nchi yake ikasusiwa. Na sisi kama tutakuwa hatukuliangalia hili tutakua na majukumu makubwa sana kwa wenzetu.

Hivi sasa Mahakama zimejaa mizozo ya mambo ya ardhi. Mahakama kwa kweli zimeshindwa kutatua mizozo hii. Utaona Mahakama hivi sasa inamueka mwananchi miaka 10 anafuatilia mzozo wa ardhi yake na bado kila siku anaambiwa kesho kesho, matokeo yake anakuwa kama mtoto wa kuku na hakuna chochote kinachotokea isipokuwa kuteseka na yule muhusika akachukua mali kirahisi.

Ni lazima tulichangie hili na tuwe wakali kwa hili ili mizozo hii ya ardhi imalizike kwa awamu hii ya saba na kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata haki zao. Tukiangalia mizozo hii haitoweza kumalizika kwa kwenda Mahakamani tu. Mizozo hii imo katika ngazi zote kuanzia Mikoa, Wilaya, Majimbo, Wadi na Shehia zetu zote. Kwa kweli viongozi ni lazima wasimamie ardhi zilizokuwepo sehemu zao.

Mhe. Naibu Spika, Iweje mtu mmoja aachiwe atoke Mji Mkongwe akachukue mali katika jimbo la Koani aseme hekari 20 zinamuhusi yeye, kazipataje? Haiwezekani suala hili likaachiwa. Isipokuwa watu wa jimbo la Koani wakae

wenyewe waweze kuamua suala la jimbo la Koani. Kesi hii inawezekana ikaamuliwa na wenyewe wananchi wa sehemu hiyo na viongozi ambao wamewachagua na wale walioteuliwa kuweza kushughulikia masuala ya jimbo lao.

Naomba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ifuatilie upya maeneo yote yaliyotolewa ya ardhi yawe na hatimiliki za uhakika na za ukweli, pasiwe na rushwa. Nchi yetu kwa kweli bado rushwa imezidi kuliko ukweli. Sehemu nyingi zimechukuliwa kwa rushwa na sio kiuhalali. *Report ya* wenzetu ambao walikwenda kushughulikia na wakaweza kutoa mapendekezo, tunaomba iheshimike na masuala haya yachukuliwe hatua na serikali yetu na si vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, Fedha nyingi sana zimetumika za wavuja jasho. Hili suala linatakiwa lipate ridhaa ya serikali na lichukuliwe hatua, ili tufuate nyayo za Rais wetu wa kwanza hayati Abeid Amani Karume, tufuate fikra zake, na kutokuwa na utapia mlo kama Mhe. Rais wetu wa sasa anavyosisitiza. Si hivyo, itakuwa kila siku tunasimama hapa na kuimba nyimbo kama tuko kwenye taarab. Hili jumba ni jumba la heshima na linapanga masuala ambayo yanahitajika katika nchi na kuhakikisha mambo yote yanayozungumzwa hapa ni yale ya kisheria na yanafuatiliwa na kutekelezwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sikutoa hongera sana kwa Mwakilishi mwenzetu aliyeongoza jopo hili kwenda kutayarisha waraka huu na kutufikia hapa. Sitokuwa na mchango mkubwa zaidi isipokuwa naipongeza sana Tume hii. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Asante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi nami nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa na uzima, akatuwezesha kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Pia nikushukuru Mhe. Naibu Spika, nami kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo tu katika *report* hii.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kusema naipongeza Kamati Teule kwa *report* waliyotuletea hapa katika Baraza lako Tukufu. Nimeiangalia sana *report* hii nimeona jinsi walivyokwenda ndani mno, waliangalia hadidu rejea walizopewa kwenda kuzifanyia kazi. Lakini hawakutosheka na hilo waliingia hadi kwenye *hansard* na kuanza kuibua mambo mengine na kupata hadudi 21, nasema hongera sana Kamati Hii.

Mhe. Naibu Spika, nianze na mchango wangu kwa kuweka nukuu ya marehemu hayati Mzee Abeid Amani Karume aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Alisema nini Mzee Karume?

"Sisi tumejitawala ili uchumi wa nchi yetu hii uwe mikononi mwetu. Ikiwa yupo kiongozi anayewapa wageni fursa ya uchumi wa nchi basi huyo hafai. Tunataka pato la nchi hii liwarejee wananchi wenyewe. Mwenyezi Mungu ametujaalia mambo mawili makubwa sana katika nchi yetu, kwanza sisi ni kidogo tu, pili tunayo ardhi nzuri yenye rutba ambayo wengi duniani wanaitamani"

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa *report* yetu inagusa jambo ambalo tangu mwanzo marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliliona na akalipa umuhimu mkubwa, leo limeibuka tena hapa likiwa katika hali na sura nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kuna hadidu rejea ambazo wamepewa wajumbe kuna mambo mbali mbali ambayo wengi katika wajumbe waliyazungumzia kwa kina kabisa. Kwa maoni yangu, mimi nimeona kwamba serikali imekosa utaratibu na mpango mzima madhubuti wa kuielewa ardhi ya Zanzibar na kuigawa katika utaratibu unaokubalika, kama taifa linalohitaji maendeleo ya wananchi wake.

Ardhi hii iliachwa tu bila ya kufanyiwa utaratibu. Laiti kungelikuwa na utaratibu uliopangwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii, tukagawa ardhi gani itatumika kwa ajili ya kilimo na nzuri inafaa kwa hilo. Lakini pia ni ardhi gani ambayo inafaa kwa uwekezaji na pia tukajiwekea utaratibu kwamba ni ardhi gani ambayo itakua kwa ajili ya makaazi ya wananchi. Kama tungelikua na utaratibu huu sidhani kama tungefikia hatua hii. Ulafi huu uliojitokeza sasa wa wachache kutaka kutumia nguvu kwenye migongo ya wanyonge ungelikuwa haupo.

Naishauri Wizara husika na serikali kuweza kufanya tathmini ya ardhi kwa wakati huu na kuweza kuona ardhi tuliyonayo ambayo haijatumika na ile ambayo iko mikononi kinyume na taratibu kuweza kuihakiki. Lakini pia kuiwekea utaratibu unaokubalika ambao utaweza kuondoa migongano na mizozo hii mikubwa ambayo sasa imeikumba Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika hii *report* nimeona kwamba utaratibu wa kutokutumiwa sheria, na utawala wa kuheshimu sheria. Tumekuwa tukitunga sheria nyingi nzuri, madhubuti lakini mara nyingi sheria hizo zinaachwa katika vitabu bila ya kutumika. Hii inatuonesha wazi pale tunapoona kuna baadhi ya watendaji wa serikali wanatakiwa kutoa ushahidi au *documents* fulani akathubutu kusema kwamba haziwezi kupatikana.

Mimi niliwahi kuchangia katika Baraza lako hili nikagusa sana hoja ya uwajibikaji kwa wafanyakazi wetu. Nimesema kwamba tumepoteza maadili na taratibu za kazi na wafanyakazi wengi wanakiuka na uwajibikaji umekuwa

mdogo na hali imekuwa mbaya sana katika taasisi za serikali. Hili leo linadhihirishwa wazi kwamba sisi kama Baraza lako tukufu limeunda kamati Teule, imekwenda kwa watendaji lakini wanakoseshwa *documents* au hawawezi kutoa ushahidi! Nasema huu si utaratibu mzuri, na hautoleta mashirikiano baina ya mihimili yetu mitatu ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, ni lazima kila mmoja ajifahamu, na utaratibu ueleweke. Hiki ni chombo cha wananchi, ambao waliwachagua Wawakilishi hao kwa ridhaa zao kuwataka wawakilishe katika Baraza lako hili tukufu na hatimae wanatokea wababe wanasema wao hawawezi kutoa ushahidi huo. Naomba sana sheria zichukue mkondo wake. Namuomba Mhe. Rais hili aliangalie kwa kina.

Mhe. Naibu Spika, kinachotufanya tuweze kufanya shughuli zetu ni kuangalia nguvu kazi na uchumi tulionao. Rasilimali zetu ndio zinazotufanya tujue wananchi wetu tunawatekelezea yale matakwa yao kwa kiasi gani. Inashangaza na kusikitisha sana kwenye *report* hii inaonesha kunyang'anywa ardhi kwa mtu ambae alikuwa anaipatia serikali pato kubwa kinyume chake akapewa muwekezaji mwengine anaeonesha kutoa fedha ndogo. Ndio lile lile tunalolisema kumbe wahujumu uchumi wamo humu humu, mjenga nchi ni mwananchi lakini na wahujumu uchumi ni wale wale wenyewe wananchi au wafanyakazi wa serikali.

Namuombe sana Mhe. Rais wa Zanzibar aiangalie kwa kina kabisa *report* hii ili aweze kuifanyia kazi, wakati hayati Karume alisema ili taifa liendelee lazima liwe na mambo manne, kwanza kabisa aliitaja ardhi, bila ya kuwa na ardhi hutokuwa na unachokifanya. Kuwe na watu, siasa na uongozi bora, hivi leo vipo vinapatikana hivyo? Tupo kwenye historia kukumbuka Mapinduzi lakini pia tunajiandaa na Sherehe za Miaka 50. Je, hivi vigezo vinne vipo na vinatumika kwa uadilifu na hii ndio nia ya Mapinduzi?

Mhe. Naibu Spika, mimi hii niiwache hapa nasema kwamba tusipoziba ufa, tutajenga ukuta. Nalisema hili kwa ajili ya kutoa tahadhari, nimeona katika hadidu rejea hapa, limetajwa eneo la Selemu. Hili ni moja katika eneo la serikali lililokuepo kwa muda mrefu sana ambalo wananchi wa eneo hilo waliozunguka wakilitumia kwa kilimo, ufugaji na shughuli zao mbali mbali na wengine masikini waliweza kujenga nyumba kwa kutumia taratibu za kisheria. Leo imefika pahala ardhi hiyo wamekuja wenye uwezo, wakubwa, wenye ubavu, wanawafukuza wanyonge kama labda hawana haki katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili ni la kusikitisha, ni jambo ambalo linawafanya Wazanzibari wanyonge wasijielewe kipi cha kushika. Imefika pahali sasa

wanajiuliza jamani sisi tuelekee wapi kwa sababu kilio chao hakisikiki, machozi yanawadondoka lakini hakuna mtu anayesikia mayowe ya kilio chao. Hii ni huzuni na hawana wa kumlilia, tunamwambia Mhe. Rais wa Zanzibar aliangalie kwa macho ya umakini mkubwa tatizo hili. Haliwezi kutatuliwa tena na Mahakama kwani Mahakama ina kesi zaidi ya 1800 kwa wakati huu na zote hazipatiwi ufumbuzi. Hivi tuseme kwa hizi chache ambazo Kamati hii imekwenda kuzifanyia kazi na kuna 1800 na zaidi na nyengine tukianza kufanya utafiti zitagundulika. Je. Mahakama hii inamudu kuzifanyia kazi?

Tunasema kwamba wanyonge wataendelea kudhalilika siku hadi siku, hili si jambo jema. Huu si utaratibu mzuri, huu sio uongozi mwema, hii sio siasa safi. Mimi leo nakuja na kadhia ya eneo la Kiombamvua, Shehia ya Kiombamvua katika ukanda wa pwani ya Nyanjale. Nilitangulia kusema usipoziba ufa utajenga ukuta.

Mhe. Naibu Spika, nilitangulia kusema usipoziba ufa utajenga ukuta. Mimi nilipata tetesi kwamba kuna tatizo katika ukanda huo, nilikwenda kuona na nilipoondoka pale nilikwenda Idara ya Mazingira katika Ofisi hiyo tukiwa kama Kamati. Nilijaribu kuhoji jamani mmempa muekezaji, lakini mlifanya tathmini za mazingira? Tulichogundua wao pia watu wa mazingira hawakuweza kufanya tathmini ya kimazingira na muekezaji aliyepewa hakusita kusubiri tathmini ya mazingira aliendelea kung'oa miembe, minazi, mifenesi, michungwa na miti kadhaa ya eneo hilo inayozidi elfu kumi. Muekezaji huyo katika eneo la ukanda huo aliwakuta wananchi zaidi ya 500 wakiwemo wanawake wenzangu, vijana na wazee wanajitafutia rizki.

Muekezaji huyo walipokuwa wanajaribu kutaka kumuuliza, waliambiwa wao hawana haki ya kuhoji serikali ikiamua imeamua na itafanya hivyo. Muekezaji aliwazuia mpaka vyombo vya habari visisogee pale, je kuna nini? Lakini pia, alikataa kufanyiwa tathmini yakimazingira hii tuliipata kwenye Kamati. Mimi niliitoa hii hoja tukimuuliza Mkurugenzi wa mazingira anasema wanaujua huo mradi, lakini walipotaka kufanya tathmini hawakuruhusiwa.

Mhe. Naibu Spika, tunauliza ina maana huu ndio utaratibu tuliojiwekea sasa mwenye nguvu mpishe? Nasema kwamba wananchi sasa wameanza kupoteza imani katika mambo haya ya ardhi na wala tena hawawezi kuvumilia.

Serikali imedai haina tena uwezo wa kutoa ajira, wananchi wamejiajiri wenyewe zaidi ya 500, lakini ubabe unatokea kupitia serikali yao waliyoiweka kwa mikono yao kwa kuwaondosha bila ya ridhaa, bila ya utaratibu na hawana pa kushtaki. Mimi nauliza je, ukimwambia mwananchi hana pa kushtaki unamkusudiaje? Ninamuomba sana, kwa mapenzi makubwa

Mhe. Rais wa Zanzibar aliangalie sana eneo la uekezaji, eneo hili nililolitaja, muekezaji anaweka nguzo na anataka kuweka uzio na kuzuia njia kubwa kabisa ya asili ambayo iliwasaidia wavuvi, waanikaji dagaa, wafanya shughuli mbali mbali, sasa anataka kuifunga. Maana anawaambia wananchi hamna pa kukimbilia sisi wawekezaji wageni sasa ndio wenye nafasi.

Mhe. Naibu Spika, ninaiomba sana serikali sisi wanawake hatuna ubavu, wanaofanya kazi pale wengi wao ni wanawake, wanapika dagaa, wanaanika na kujipatia rizki. Wanafanya kazi zile ili wapate kutoa michango ya ada za watoto wao mashuleni, lakini pia serikali imesema kwamba wajiendeshe wenyewe. Kuna visanduku vyao (vikoba) wanapata kuchangia, hivi ukiwaondoa pale serikali inawapeleka wapi? Serikali haijenda kuzungumza nao na kama imezungumza nao watwambie wamekubaliana nini? Mimi ndie ninaekaa eneo hilo husika, hakuna mtu aliyepewa chochote, wananchi hao wanahangaika huku na kule kwa viongozi hawa na wale.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alibahatika mwenzangu kwenda kuona hilo eneo. Lakini pia, niliishauri kamati ambayo inahusika na Ofisi ya Mazingira twende tukaone kwa bahati mbaya sana hatujenda, lakini mimi binafsi ninayesema hapa nina uhakika, nina ushahidi, ardhi hiyo ilikuwa nzuri ina mimea, ina miti ambayo watu wanaitumia kwa matunda, ina minazi zaidi ya elfu tano na imen'golewa ovyo ovyo na tathmini ya kimazingira haikuelezwa.

Hili mimi sikubaliani nalo kabisa na nasema kabisa hapa hapa itakapofika wakati wa bajeti ya Wizara hii husika, kama hili halikufanyiwa utaratibu nikajua watu wale mia tano wapi wapo na nini wanafanya sitokubaliana nayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo niseme sasa hivi jamani kwa nini tunataka kwenda pahala ambapo hapakuwa katika utaratibu sisi ndio tuliofanya mapinduzi na tunayasifia na keshokutwa tutafurahia miaka 50, tunataka kuwaambia nini wananchi kuhusu ardhi ya Zanzibar ambayo 1964 waliifanyia Mapinduzi.

Nadhani leo serikali ichukue tatizo hili kama chachu ya kulifanyia kazi na kuona kwamba wanarejesha imani kwa wanyonge walio wengi Zanzibar. Hususan maeneo ya uekezaji ambayo inaonesha dhahiri kwamba wengi katika viongozi wetu ndiko walikoegemeza na wao miradi yao, huo ndio ukweli na wamejifanya na wao ni wawekezaji.

Naiomba sana serikali kwa kuwa imeandaa sherehe ya aina yake ya miaka 50 ya Mapinduzi, basi jamani na Mapinduzi yakumbukwe tena katika historia ya

kuwarejeshea wananchi wale hadhi na heshima ile ambayo ilikusudiwa kufanyika katika Mapinduzi ya 1964.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba nami niunge mkono *report* hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa mchana huu kupata dakika chache za kuweza kutoa mawazo yangu machache juu ya suala hili lililo mbele yetu. Kwanza nianze nami kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa kuendelea na shughuli za kawaida.

Pia, nikushukuru na wewe kunipa nafasi. Pia, nimpongeze kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa Kamati Teule kwa kuchunguza kadhia ya ardhi Mhe. Ali Mzee Ali, kwa umahiri, uwezo, ujuzi na umakini wake. Kwa kweli muda aliosimama pale kuna vijana hawawezi kutumia muda wote pale kusimama, alisoma bila ya kutumia miwani kuna, vijana hawawezi kufanya vile naomba, nimpongeze sana kwa uwezo wake huo.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Ali Mzee, kwa uzoefu wake na ujuzi wake wa mambo hususan haya ya matatizo ya ardhi kabla na baada ya Mapinduzi, ajifungie pahala atunge kijitabu kidogo kinachohusu matatizo ya ardhi Zanzibar ili vijana wetu ambao wamekutia tu Mapinduzi yapo, wajue ardhi huko nyuma ilikuwa inamilikiwa namna gani na leo inamilikiwa vipi ili historia yetu isipotee.

Mhe. Naibu Spika, kulingana na historia aliyoitoa Mhe. Ali Mzee Ali, inaonesha huko nyuma ardhi ilikuwa ina wamiliki na wachache kama sabiini na kidogo. Lakini kwa njia moja au nyengine wamiliki hawa walikuwa na nyaraka, kwa sasa tunaita hati za kumiliki. Baada ya Mapinduzi kuonekana kuwa wanyonge walio wengi hawana ardhi hata ya makaazi licha ya kilimo, kwa sababu ardhi walizokuwa wakilima ni za hao makabaila au mabepari na ilikuwa wanatozwa kodi kwa kulima katika ardhi hizo. Ndio serikali ya Mapinduzi hatimae ikatoa tangazo la kutangaza kuwa ardhi yote ya Zanzibar ni mali ya serikali.

Tangazo hilo lilipokelewa na serikali ikachukua hatua ya kuwagaia wazanzibari waliobahatika eka tatu tatu za ardhi. Sasa Mhe. Naibu Spika, wengi wa watu ambao ardhi zao au mashamba yao hayakukatwa zile eka tatu tatu, waliona kwa *time* zile si mali ya serikali ni za kwao wenyewe. Na hata ningelikuwa mimi kwa sababu sehemu yangu haikuchukuliwa ningeliona kwamba hii bado si ya serikali. Na mpaka leo bado tunatumia nyaraka zetu za

asili zenye *stemp* ya Said Khalifa bin Haroub bin Thuwein kwa halali ya kumiliki sehemu ninayoimiliki.

Mhe. Naibu Spika, hata eneo hili tuliopo nina hakika wapo watu ambao wanaweza kudai kuwa hapa ni sehemu yao. Kwa hivyo, umilikaji Mhe. Naibu Spika, kwa wakati huo ulikuwa unaenda hivyo na hadi leo kwa yale maeneo ambayo serikali haijatokea haja kuyachukua kwa kuyatumia, sisi tunaomiliki tunahisi si ya serikali ni ya kwetu.

Kwa hivyo, ninaungana na Kamati Teule taaluma itolewe kwa wananchi kujua kuwa ardhi ni ya serikali, sehemu uliyo nayo umeachiwa tu kwa matumizi yako. Lakini tujaalie, je, mimi sehemu yangu bado haijataifishwa pamoja na kuwa imetangazwa ardhi ni mali ya serikali pindipo nikifariki, kwa nini ikawa warithi wangu wana haki ya kurithi na ardhi si yangu ni ya serikali?

Kwa hivyo, hapa Mhe. Naibu Spika, ningetaka ufafanuzi kuwa Zanzibar bado tunaendelea kurithi mashamba na ardhi, lakini serikali inasema ardhi yote ni ya serikali. Sikatai kuwa watu wasirithi. Sasa kama yote ni ya serikali ndio nikasema itabidi tuelimishwe tujue kuwa sisi ni watumiaji tu wa ardhi, kama ilivyokuwa ni wakaazi tu kwa hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, huko nyuma kulikuwa na bwana Udi mmoja, aliambiwa kuwa kamiliki zaidi ya mashamba 50, lakini sasa mbona hawa mabwana Udi wanaongezeka? Ile azma ya Sheikh Karume tunaipiga teke? Kila mmoja anajikatia atakavyo yeye, lile lengo ambalo Mhe. Ali Mzee Ali, Kamati yake wamelitaja la Mapinduzi kwa kuigawa ardhi kwa wanyonge linaenda wapi?

Je, sisi wanasiasa na watawala na matajiri na wageni tuliochukua ardhi ndio wanyonge? Kwa sababu hivi sasa ardhi inamilikiwa na watu wanne wakubwa. Watawala yaani serikali, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi baadhi yao, matajiri na wageni wanaokuja kuekeza. Huyu mwananchi ambaye yalifanywa Mapinduzi ili ardhi apate yeye umemuweka wapi?

Je, ile azma nzima ya Mapinduzi inazingatiwa? Au sisi tulikuwa tunawaonea choyo wale makabaila wachache tukataka sasa ile nafasi yao tuichukue sisi watawala wa leo. Hoja ya Sheikh Karume ni nzuri, ardhi ije kwa wanyonge, lakini hawa ni wachache wanaopata. Walio wengi wanyonge hawana kitu .

Mhe. Naibu Spika, iko haja ya kufanya marekebisho ya matumizi ya ardhi ili iendane na azma ile ya Mapinduzi ya kuwagaia watu ardhi kwa ajili ya makaazi na shughuli zao za kilimo. Vyenginevyo itakuwa serikali inakwenda

kinyume na lile tangazo la Baraza la Mapinduzi mara tu ya *assassination* yaani ya kuwawa kwa Mzee Karume. Sheikh Aboud Jumbe baada ya kukaa madarakani pale alisema "Mzee Karume amekufa, lakini kilichokufa ni kiwiliwili chake tu mawazo, fikra na vitendo vyake vipo na vitaendelea kudumishwa milele". Na ikawekwa kuwa Baraza la Mapinduzi ndio lililotamka vile.

Sasa mbona tunakwenda kinyume na tangazo lile la Baraza la Mapinduzi la 1964? Sisi wakubwa wa leo tumekumbwa na shetani gani wa kuona kuwa kila kitu kiwe chetu badala ya kuwa cha wananchi? Baada ya kuhudumia wananchi tunajihudumia sisi na familia zetu. Huu ndio utawala bora? Mchangiaji mmoja wa asubuhi alisema haya tunayoyafanya hapa yote kama kisiasa, kiuchumi, kiutawala, yanaandikwa na iko siku yatasomwa, kama mazuri sawa, kama mabaya *inna lillahi wainna ilayhi raajiun!* Tujitahidini tuache utashi wa kutaka utajiri kinyume na taratibu.

Mhe. Naibu Spika, hadidurejea nyingi za humu zinaonesha baadhi ya mwahala kuna mvutano miongoni mwa wananchi juu ya ardhi, lakini kuna maeneo ni mvutano baina ya serikali na wananchi. Ina maana serikali imekuja kuhodhi ardhi pahala ambapo wananchi wanaitumia. Kwa mfano imetajwa humu Bambi, wananchi walipewa kwa ajili ya kilimo, lakini serikali pahala pale sina hakika kwa maslahi ya kitaifa, au kwa maslahi gani wakahisi bora wampe muekezaji.

Sasa hawa wanyonge chungunzima wanaolima pale waende wapi, wakalime wapi? Mabondeni warudi ndio kwenye nyumba zao za kuishi. Kwa nini hapa serikali isione umuhimu wa hawa watu, tukaona umuhimu wa huyu muekezaji tu?

Mhe. Naibu Spika, ningeiomba serikali iwaonee huruma na iwape hadhi ya juu wananchi wake kuliko wanavyompa mgeni. Gadafi moja ya jambo alilogombana na dunia ni kuwahifadhi raia wake wawili waliotuhumiwa kufanya hujuma ya ndege miaka 1980, yeye akatakiwa awatoe wahukumiwe kimataifa akakataa jinsi ya alivyokuwa akiwaheshimu na kuwapa hadhi raia wake. Palipokuwa na vita vya Wa-Phalestin na Israel, akikamatwa Muisrael mmoja tu, wako tayari wawaachie Waphalestin elfu moja, lakini kamanda wao aachiwe huru sisi tunakwenda *vice versa*. Tunamuheshimu muekezaji mmoja tunawatimua watu kadhaa raia wetu wanaotumia eneo lile kwa nini?

Mhe. Naibu Spika, ninukuu msemo wa Rais wa Kwanza wa Tanzania Mwalimu J.K.Nyerere aliesema kwamba "ili tuendelee tunahitaji vitu vinne. Watu, Zanzibar watu tunao kwa sababu serikali inaagiza uzazi wa mpango kwa sababu labda watu wapo wengi, Ardhi, hii ndogo iliopo, lakini akataja

mambo mawili makubwa ambayo ni Siasa Safi na Uongozi Bora. Je, hivi tunavyokwenda Zanzibar tumekosa nini baina ya siasa safi na utawala bora, yote au moja tu, ndio maana tunakwenda kama hivi tunavyokwenda.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tulifanya Mapinduzi kuwakomboa wanyonge, neno wanyonge kwa sababu kunyonga ni kuua sisi tunaitwa wanyonge ina maana tumeambiwa tuuliwe, lakini wanyonge kwa maana hii ni maskini.Kwa hivyo, tilifanya Mapinduzi ili kuwaokoa maskini, nikitarajia kuwa serikali katika dira zake za maendeleo itakuwa wana-*focus* hilo, kuwaboreshea maisha yao ili yatoke pale yalipokuwa na yaende mbele zaidi wala sio kurudi nyuma.

Kutokana na hali yangu kuwa si nzuri kwa kumalizia naipongeza sana Kamati hii kwa kazi nzuri walioifanya ya kuibua mambo mbali mbali na nirejee kusema kama ingelikuwa nina uwezo ku-*promote* watu kiwadhifa ningemwita Mhe. Ali Mzee Ali, kuwa ni *professor* kwa masuala ya siasa ya Zanzibar. Lakini kwa sababu sina uwezo huo Mhe. Ali MzeeAli, nimuombe atunge kijitabu kama nilivyosema mwanzo kinachoelezea historia ya ardhi ya Zanzibar kabla na baada ya Mapinduzi.

Baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii mia juu ya mia.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa ushirikiano wenu tangu asubuhi hadi hivi sasa. Pili, tunategemea hoja yetu tuimalize jioni, kuna wachangiaji wamebakia wanne miongoni mwao wawili wametaka dakika tano tano. Baadae tutamwita Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na baadae tutamwita Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Baada ya hapo tumalizie na Mwenyekiti wa Kamati ili afungie mjadala. Sasa naomba jioni tuje mapema na hao waliobakia nitawataja na wale waliochangia na wasiochangia waje wasikilize hoja zinavyotolewa.

Mchangiaji wa mwanzo atakuwa Mhe. Abdi Mosi Kombo, baadae dakika tano tano Mhe. Subeit Khamis Faki, na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Saleh Nassor Juma na mwisho atamalizia Mhe. Mohammed Mbwana Hamad. Waje mapema nikiita jina hayupo sirejei.

Baada ya hayo ninaakhirisha kikao hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kuniruhusu na mimi kuchangia ripoti ya Mhe. Ali Mzee Ali, juu ya migogoro ya ardhi iliyotukabili hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kwanza kutokana na hali ya migogoro hii ya ardhi hasa katika sehemu zetu hizi za Zanzibar kanda za mashariki ndiko migogoro ya ardhi imezidi, kwa sababu ndiko kwenye ardhi zilizokuwa mali sana hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, mimi huwa najiuliza migogoro hii inasababishwa na kitu gani. Sisi viongozi wa nchi hii hebu tujiulize migogoro hii inasababishwa na kitu gani. Wajumbe wengi walisema hapa kwamba migogoro hii inasababishwa na wawekezaji, wawekezaji wanawanyanyasa wananchi wa Zanzibar. Lakini mimi najiuliza kwani mwekezaji aliyetoka Ulaya akafika hapa Tanzania akaletwa mpaka Zanzibar amekuja kwa dhamana ya nani.

Mimi nafikiria kwamba mwekezaji yeyote aliyetoka nchi za nje yuko katika dhamana ya Wazanzibari. Sasa itakuwaje mgeni katoka nje akafikia kumnyanyasa mwananchi wa Zanzibar, amnyang'anye haki zake au asitoe haki za Wazanzibari kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Spika, katika hadidurejea nambari 9 imetajwa kwamba mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa Pwanimchangani na Mwekezaji. Mhe. Naibu Spika, kama ingelikuwa sisi viongozi pamoja na watendaji wa mawizara ya serikali tunawatendea haki kweli wananchi wa Zanzibar, basi nahakikisha migogoro isingekuwepo.

Lakini sasa watendaji wa mawizara hususan hawa watendaji wa ardhi wameshajenga tamaa kwa Wazungu na tamaa ni mbaya, hata Waarabu wanasema kwamba "*Waminfadhilaka Sayyidaka",* ataekufadhili kakuumiza. Kwa hivyo, sisi tushaumizwa na Wazungu na madhali tushaumizwa wananchi wetu watakuwa hawatendewi haki hata kidogo, tuna tamaa tuondoe tamaa, wananchi wa Zanzibar tuwafanyie haki.

Kwa mfano huko Pwanimchangani kulikotajwa kuna mwananchi mmoja anaitwa Vuai Hamad, mwananchi huyu ana sehemu yake imepimwa na watu wa ardhi akapewa mwekezaji. Baada ya kupewa mwekezaji wakafanya tathmini ya miti yote iliyokuwemo mle na wanaijua na Mkurugenzi wa Ardhi anajua, kijana huyo wameshindwa kumlipa haki zake mpaka leo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nampa habari kwamba Pwanimchangani wako watu hao na kijana huyo yupo na hata kesho akitaka nitamletea amueleze shida zake.

Vile vile, namuomba Mhe. Waziri, baada ya kikao hiki tufuatane mguu kwa mguu twende Matemwe nikampeleke kwa wananchi walioathirika na wawekezaji ambao wamenyang'anywa haki zao na hawakunyang'anya wao, wamenyang'anywa na watendaji wa serikali, kwa sababu ndio wenye amri, Mzungu hana amri hapa, Mzungu tumemuweka sisi. Lakini sasa Mzungu akiendewa anasema serikali ndio iliyoniweka hapa. Kwa hivyo, nendeni katika serikali yenu. Sasa mwananchi akiondoka hapo akienda katika serikali hapati ufumbuzi na ndio sababu ya migogoro.

Mhe. Naibu Spika, mwananchi huyu tokea Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipokuja akafungua Tawi la Pwanimchangani na akaweka jiwe la msingi miaka minne iliyopita na mwananchi huyu akaomba kuzungumza nae juu ya shida yake hio. Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete akaamua kwamba apewe mafao yake, amri ya Rais haikukubalika mpaka leo. Kwa hivyo, watendaji wetu mpaka zile amri za Rais hawazikubali na mpaka leo kijana huyu hajapata mafao yake.

Sasa namuomba Mhe. Waziri, afanye kama iwezekanavyo kijana huyu akapate mafao yake ambapo Wakurugenzi wa Ardhi wanamjua.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikiendelea tena katika sehemu iliyoathirika sana kwa utalii ni Matemwe. Lakini sasa serikali naiomba itenge maeneo maalum ya utalii ili wananchi wetu hii ardhi waipate sehemu nayo angalau wapate kulima. Kwa sababu sasa hivi ardhi ya Matemwe imekuwa mali, sasa ardhi haipo imekwisha. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri, sasa hivi afanya kama iwezekanavyo atenge sehemu za utalii kwa sababu utalii sasa hivi uko mpaka vichochoroni. Naiomba sana serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati itenge maeneo maalum ya wawekezaji.

Nikiendelea katika mchango wangu mimi ningeliomba kwa sasa ikiwa anakuja mwekezaji sehemu zenye utalii basi washirikishwe wananchi wenyewe kwanza, waulizwe kama sehemu hii wanaitumia kwa kilimo basi serikali itafute pengine. Kwa sababu kuna sehemu kama kule Matemwe sehemu nyingi wananchi wanazitumia kwa kilimo na hivi sasa zishachukuliwa na utalii. Kwa hivyo, hili jambo lazima tulifikirie Mheshimiwa, ikifika miaka 15 ijayo Zanzibar haina kilimo.

Jengine kuna watalii wanavunja sheria ya kujenga huu utalii hasa sehemu za fukwe. Kuna sehemu ambazo wananchi wanazitumia kwa kupita kwenda baharini au kupita kwa haja zao, lakini sasa hivi zile njia wanaziba wanajenga makuta na wananchi wanapata shida, wanatupa matatizo na ndio migogoro hii inapotokea. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

iangalie jambo hili kwa karibu sana na wananchi wakati wanapopeleka malalamiko yao hawasikilizwi. Wazungu hivi sasa wamepewa *power* kubwa sana kuliko wananchi, hatuwajali wananchi tunajali maslahi ya Wazungu tu, sasa tukiwa tunajali maslahi ya Wazungu tu migogoro itakuwa haimalizi.

Mhe.Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu ni kwamba wanapokuja wananchi wanaambiwa kwamba matatizo yenu kamalizeni kwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya atamaliza matatizo ya ardhi? Matatizo ya ardhi ayamalize mwenyewe Mhe. Waziri. Mimi namuomba Mhe. Waziri, afanye ziara rasmi aje Matemwe aangalie wananchi waliokuwa wamechukuliwa hizi haki zao na Wazungu waamuliwe hawa ili tupate usalama.

Nikimalizia Mhe. Naibu Spika, vile vile, naomba hivi sasa kama tutafanya utaratibu natoa ushauri, ndani ya majimbo yetu hususan yale majimbo ya ukanda wa pwani ndio yenye utalii mkubwa sana hivi sasa, bora zipangwe kamati za shehia zishughulikie ardhi. Wakati anapowekwa mwekezaji zile kamati ambazo zinashughulikia mpango huu, basi wananchi wenyewe wakusanywe na wakishakusanywa waulizwe sehemu hizi ambazo wanataka kupewa Wazungu, wananchi washauriwe kama wanazitumia kwa kilimo basi wazitumie kwa kilimo, kama watatumia kwa uwekezaji, basi serikali iweke sehemu maalum za uwekezaji na sehemu maalum wapewe wananchi wenyewe walime.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia ripoti hii ya *Professor* Ali Mzee Ali juu ya Migogoro ya Ardhi na mimi naunga mkono hoja hii, ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana jioni hii ya leo na mimi kupata fursa kuchangia Ripoti hii ya Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi. Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi napenda niwapongeze sana Wajumbe wa kamati hii kwa kufanya kazi yao vizuri kamati inayoongozwa na mzee wetu mahiri, Mhe. Ali Mzee Ali, *professor* wetu na kweli katika hotuba yake ameonesha kama yeye ni mzee wa Baraza hili na inafaa kujifunza kwake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ripoti ni nzuri sana na ripoti imesema waziwazi imeonesha kila penye matatizo. Sasa lilibokia ni serikali nayo kuona kama kuna haja ya kuziangalia kwa umakini kabisa ripoti hii.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kidogo naomba niseme kwamba Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, watendaji wake wakuu wote bahati mbaya mno au bahati nzuri ni wapya. Waziri ni mpya wa wizara hii, Katibu mkuu ni

mpya, Naibu Katibu mkuu ni mpya na watendaji wengine karibu wote wa hii wizara ni wapya. Lakini pamoja na upya wao ni kwamba sasa wamekuja kukuta hili suala.Hivyo, itabidi walifanyie kazi pamoja na upya wao, ukikabidhiwa nyungu kupika basi unaonja kwanza wewe, unaonja chumvi, je, imekolea vizuri. Kwa hivyo, na wao itabidi waonje chumvi halafu waone chakula chetu kimepikika vizuri ili kuweka mambo sawa.

Mhe. Naibu Spika, pamezungumzwa suala la viwanja vilivyotajwa Tumbe. Mimi naiomba serikali iwaangalie kwa jicho la huruma sana wananchi wake na iwafanyie vizuri wananchi wake. Kwa sababu baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 Marehemu Mzee Abeid Amani Karume au serikali ilitangaza kama ardhi yote ni mali ya serikali, ni vizuri sana kama ardhi yote ni mali ya serikali, lakini walisema kuna sheria inasema kwamba, mtu anayemiliki ile ardhi na akaitumia kwa kipindi ambacho kinakuwa ni kikubwa zaidi sijui miaka mingapi, lakini baadae yule mtu anakuwa ile ardhi pamoja na kuwa ni ya serikali, lakini inakuwa kama yeye kamiliki. Sasa serikali inapotaka kutumia ile ardhi, basi wananchi huwa wanalipwa fidia na serikali kwa ajili ya kutumika kwa umma.

Sasa kule Tumbe wananchi wa huko ambao wengi wao wanaolima pale Tumbe ni wananchi wanaotoka katika Jimbo langu la Micheweni. Mhe. Naibu Spika, vile viwanja kupimwa na serikali ni haki yake, sawa serikali inataka kutumia kwa ajili ya kuweka miji ya kisasa. Lakini linalosikitisha ni kwamba wale wananchi wanaoitumia ile ardhi kwa muda tangu Mapinduzi ya mwaka 1964 mpaka mwaka 2010, palipopimwa viwanja wale wananchi hawakupewa. Mimi nimetizama katika orodha zilizokuwemo za majina ya waliopewa zile nafasi za kupewa viwanja wale wananchi wenyewe wahusika hakuna hata mmoja aliyekuwemo.

Kwa hivyo, Mheshimiwa, hawa hawakutendewa haki, serikali kwa kweli haikuwatendea haki wananchi ambao wako katika maeneo yale ya Tumbe sehemu ya Chwaka. Haiwezekani Mhe. Naibu Spika, kuwa wale wanaomiliki ardhi zaidi ya miaka thalathini na zaidi ardhi imekwenda kupimwa hawakupewa hata kiwanja kimoja kimoja, hivi kweli tumewatendea haki wananchi wale.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwajutie sana na iwahurumie wananchi wake. Hivyo, naomba kama wale wahusika wenye eneo lile basi serikali iwape na wao viwanja na sio wawape viwanja kama ilivyowapa, nasikia kuwa walikwenda wakapewa Ndaambani ndani huko, kwa kweli Mheshimiwa hawakutendewa haki. Kwa hivyo, naiomba serikali ione kwamba na wananchi wana haki ya kupewa hasa ukizingatia kuwa serikali imesema mtu akimiliki ardhi kama serikali inataka

kuitumia inalipa fidia. Sasa wao wamelipwa fidia gani, mana hawajapewa fidia ya pesa wala hawakupewa ardhi, ilikuwa wanapewa viwanja wakapimiwa na wao wajenge na hakuna mwananchi hata mmoja wale wanaolima maeneo yale yaliopo aliyepewa, hawakupewa kabisa.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, alizingatie hili na wale wananchi waonewe huruma hasa ukizingatia kwamba wengi wao wanatoka Jimbo la Micheweni. Kila siku mkija hapa mnasifu Jimbo la Micheweni kama ni jimbo kame, wananchi wa Micheweni ni masikini, sasa wanatoka kule maweni kuja kulima pale, ardhi yao imechukuliwa hawakupewa kitu chochote.

Naomba sana serikali iwaangalie kwa jicho la huruma na iwahurumie na iwafanyie bidii angalau na wao wapate hata kama ni hivyo viwanja vya kujenga wapewe, lakini si kwamba vichukuliwe wao wasipewe. Kweli ardhi ni mali ya serikali, lakini washamiliki kwa muda mkubwa sana. Kwa hiyo, waonewe imani na wao.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nizungumze ni eneo la Nziwani. Mhe. Naibu Spika, na eneo lile wananchni wa Micheweni pamoja na wenzao majirani pale walikuwa wanalima, walikuwa wanalima mtama, mahindi, muhogo, kunde na vyakulka vyengine wakawa wanajifaidia na watoto wao. Lakini kwa bahati mbaya mno lile eneo lilichukuliwa akamilikishwa mama mmoja hivi, sasa mama yule aliyepewa eneo lile halimi, alipewa eneo lile kwa ajili ya kulima na kufuga, halimi wala hapafugwi.

Sasa eneo lile kajenga nyumba na nyumba ile imekuwa kama ni kero kwa wananchi. Kwa sababu nyumba iliyopo pale imekaa inatumiwa katika matumizi ambayo siyo, wanatoka watu huko wakifika pale wanakodishwa nyumba wanakaa wakizungumza kwenye starehe zao.

Mheshimiwa, hilo ni tatizo na linawakera wananchi pale. Kwa hivyo, naomba lile eneo yule mama kwa sababu makusudio aliyopewa hafanyi basi warudishiwe wananchi eneo lile wapate watumie, lakini pale limekaa tu kulima halilimwi, kufugiwa halifugiwi, linatumika kwa matumizi ambayo siyo. Zikifika siku za sikukuu pale watu wanakwenda wakifanya starehe zao na kuwakera wale majirani walioko pale.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hili suala kuna kipindi nililipigania na nikazungumza sana, nikaja nikapewa hatimiliki alizomilikishwa yule mama, lakini hizo hatimiliki alizomilikishwa aliandikiwa akenda akapewa baada ya kelele zetu nyingi. Sasa Mhe. Waziri, naomba lile eneo kwa sababu halitumiki wale wananchi warudishiwe wenyewe. Nasikia sina uhakika kama huyo mama yeye keshammilikisha mtu mwengine yeye keshaliacha, sasa kama

kaliacha hili eneo kwa nini wasipewe wenyewe na lile eneo lilichukuliwa kwa sababu watu wa kilimo wanataka kutumia.

Watu wa kilimo walikuwa wanafanya eneo lile kama ni eneo la nasari kama kupandia miti na mambo mengine, lakini baada ya wale watu wa kilimo walipoliacha, kwa nini wasipewe wenyewe akapewa mtu mwengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa, hili suala nililipigia kelele sana na leo bado naendelea kuzungumza kama yule mama makusudio aliyokusudia hafanyi katika eneo lile, basi warudishiwe wenyewe wale wananchi waonewe imani, wapewe maeneo wapate walime. Leo tunawahimiza watu walime, lakini maeneo ya kulima ni yale yaliyochukuliwa na watu wameyaweka tu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, na hilo naomba liangaliwe kwa kina kabisa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala hili tunalolipigia kelele la wawekezaji kuwanyanyasa wazalendo. Mimi nasema hili ni kosa la serikali, mimi nasema kabisa ni kosa la serikali, si wananchi. Kwa nini niseme ni kosa la serikali, kwanza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya kosa tulipoamua kama sasa tunataka kuingia kwenye utalii, tunakaribisha watu kuwekeza kwenye utalii tulifanya makosa makubwa.

Serikali ilifanya makosa kwa sababu haikuwapa elimu wananchi wake wakajua jinsi ya kuwekeza. Wawekezaji walipokuja wameuziwa maeneo na eneo kuliuza ni kulitupa, kwa nini wananchi hatukuwapa elimu kwamba waingie ubia na wawekezaji, tungekuwa tumefanya jambo zuri kweli kweli. Kwa sababu wananchi wetu wangepata faida kubwa sana na wangekuwa wanatumia mpaka mwisho wa maisha yao katika maeneo ya ardhi yao.

Lakini walipokuja watu hawakupewa elimu, ikawa watu wanauza maeneo sasa na kuuza ni kutupa mtu akishauza eneo kapewa shilingi milioni, anaona kapata keshokutwa eneo lile linafika shilingi milioni mia mbili. Sasa kama tuliwapa elimu wananchi wetu vizuri sana na serikali ikawakalisha kitako ikawapa elimu vizuri, wangetoa maeneo kwa kuingia ubia na wawekezaji, wakiondoka basi wananchi wetu wangekuwa wanafaidika na maisha yao. Lakini leo tumewatelekeza wananchi bila ya kuwapa elimu.

Naiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Unguja tulifanya kosa, lakini Pemba bado maeneo mengi hayajaingia utalii kwa sababu bado wananchi wa Pemba nawashukuru wao hawajataka kuwekeza huo utalii. Lakini hicho kipindi ambacho serikali itakuja kutaka kuwekeza, basi naomba isije ikafanya kosa lililofanyika Unguja, wananchi wapewe elimu ili waingie ubia na wawekezaji na wapate kutumia kwa muda mrefu sana.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka na mimi nipate kuchangia japo kwa dakika tano na ninaheshimu sana kauli yangu niliyokwambia. Kwa hiyo, kwa kuwa nilikuomba unipe dakika tano, naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa angalau kutoa mawazo yangu kuhusu ripoti ya kamati hii iliyokuwa inaongozwa na Mhe. Ali Mzee Ali, ambae kwa kweli huyu mzee laiti ingelikuwa mimi nina *political say* katika nchi, basi ningelimtunukia *degree* ya siasa na mambo ya historia, ni *degree* ya uzamivu (*PhD*) *in Economic and Political Science*.

Kwa kweli huyu mzee ni mzee moja makini sana na kwa kweli huyu mzee nadhani kuna haja kama alivyosema *Professo*r Mohamed Haji Khalid, kwamba angejiweka pahala akatutungia kijitabu kidogo hivi ili tukaweza kupata rejea rejea katika maandiko yake. Nadhani hili ni wazo zuri namuomba sana mzee afanye hilo ili na sisi huku tupate la kushika.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la kuweka *hansard* sawa, naomba kidogo na mimi katika hii Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi Zanzibar mwaka 2013 katika ukurasa wake wa kwanza niweke *hansard* sawa uniruhusu nifanye nukuu kidogo.

> "Baada ya wewe Mhe. Spika, kutafakari kwa umakini na kwa busara kubwa siku ya tarehe 10 Ogasti, 2012 uliwateuwa Wajumbe wafuatao kuunda kamati teule hiyo, Mhe. Abdala Mohamed Ali, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Ali Mzee Ali, Mhe. Fatma Mbarouk Said na Mhe. Nassor Salim Ali"

Mhe. Naibu Spika, naomba *hansard* ikae sawa kidogo kwa sababu hapa katika jina nambari mbili alikuwa na kamati teule nyingi huyu Mheshimiwa ikabidi akaondolewa na hatimaye mimi nikapata barua ya uteuzi wa Kamati hii. Kwa hiyo, na mimi nilikuwa Mjumbe. Kwa hivyo, na-*declare* rasmi kwamba na mimi nilipata barua. Hivyo, katika kamati hii teule nilikuwemo. Sasa *hansard* ione pamoja na nyinyi Wajumbe kuwa na mimi ni miongoni mwa waliokuwa Wajumbe wa hii kamati na kwa vyovyote vile naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tatizo la ardhi ni la kihistoria katika nchi hii kama ilivyoeleza ripoti yetu hii. Na serikali yoyote iliyo makini sana katika uendeshaji wake lazima iwe makini katika suala zima la usimamiaji na ugawaji wa ardhi. Kwa sababu isipokuwa makini serikali huweza kuleta matata baina ya wananchi na wananchi au baina ya wananchi na serikali yao

wenyewe. Migogoro mbali mbali Mheshimiwa katika nchi mbali mbali imetokea kwa serikali za nchi hizo kutokuwa makini katika suala zima la ardhi.

Mhe. Naibu Spika, hapa Zanzibar kuanzia katika miaka ya nyuma huko kabla ya Mapinduzi ardhi ilikuwa ni tatizo kumilikiwa na Muafrika. Sisi kule Pemba ardhi kubwa ilikuwa inamilikiwa na watu wenye asili ya ki- Asia na watu wengine, ni Muafrika mmoja tu aliyekuwa akimiliki ardhi kule Bw. Shamte Mmadi, yaani Shamte bin Hamadi. Shamte bin Hamadi ni baba yake Muhammad Shamte Hamad Al-Shirazy aliyekuwa Waziri Mkuu wa mwanzo wa nchi hii, ndio mtu kepee aliyekuwa akimiliki ardhi pale.

Sasa Mhe. Naibu Spika, wengi wetu katika miaka hiyo ya 1940 mpaka kufikia 1950 tulikuwa tunaishi tukiwa kama manokoa katika ardhi zetu na tulikuwa tukitumia ardhi kwa *renting of land to the land law*, tulikuwa tukikodi ardhi kwa matajiri wa ardhi *with the share of the crops*, kwa kutumia kuwa wao tunawalipa yale mavuno, tukivuna ndio na wao tunawapa *share* yao na sisi tunachukua yetu, ukawa mzozo mkubwa mno, tuliishi katika mazingira hayo kwenye miaka kadhaa huko nyuma.

Lakini mpaka siku ya tarehe 12 Januari, 1964 Mhe. Abeid Amani Karume, aliyekuwa kiongozi wa Afro-Shirazi akawaelekeza Wazanzibari katika kujikomboa pamoja na mambo mengine ili na wao wapate ardhi. Kwa hivyo, yakatokea mapinduzi na kila Mzanzibari baada ya mapinduzi alipata ardhi, eka tatu tatu ulikuwa unapewa pale za makaazi na mambo mengine.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nilidhani kwa sababu sasa hivi tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa (*GNU*) iliyounganisha vyama viwili vikubwa katika nchi hii. Lakini sera zinazotumika ni za Chama cha Mapinduzi. Mimi nilidhani Mheshimiwa, kwa sababu Chama cha Mapinduzi hata sisi CUF wengine tulikuwepo huko huko kwenye *Afro*-Shirazi. *Afro*-Shirazi ilileta ukombozi katika suala zima la kuwakomboa wananchi ili waweze kupata *national cake* ikiwemo hii ya ardhi.

Leo inasikitisha sana watendaji wetu katika serikali hii iliopo ya *GNU* ambayo inaendeshwa kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi. Inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, wamekuwa kama vile pweza. Pweza anatoa wito anajivutia yeye, huku wengine wanapata shida. Wakati wa ukoloni tulikuwa kama manyokoa, tunakwenda kufanya kazi kwa matajiri wanaomiliki ardhi. Lakini sasa tumejitawala hivi sasa tatizo liliopo Mhe. Naibu Spika, hebu tuangalie hapo Mziwanda kwa Mhe. Subeit Khamis Faki, wakulima 80 waliondoshwa katika ardhi ile, waliokuwa waki *earn living* kupitia ardhi ile

wameondosha wakulima hao, akaja mama mmoja pale nyumba ndogo ndogo hivi.

La kusikitisha sasa jana tumepitisha mswada wa ukimwi hapa, ame-*create* mazingira hatarishi katika suala la *HIV and AIDS*, pale pana mazingira hatarishi. Wakati wakulima 80 walikuwa waki-*earn living* kupitia ardhi ile wameondoshwa na kupelekwa huko hawana la kufanya, baadae tumeekewa mazingira hatarishi yanayoweza kupelekea ukimwi na virusi vya ukimwi. Jamani hilo si tatizo.

Sasa mimi ninadhani Mhe. Naibu Spika, inatosha, *enough is enough*. Mwaka 1964 tuliingia katika boma tukavunja boma tukapindua ili tupate ardhi tukiongozwa na Jemadari Mzee Abeid Amani Karume. Sasa mkoloni tushamuondosha tunataka kumpindua nani na sote ni sisi kwa sisi. Mimi ninamuomba Mhe. Rais katika hili namuomba Mhe. Rais wetu asivumilie, hii si dhamira ya mapinduzi, hawa watendaji ulionao serikalini wana-*betray* dhamira nzuri ya mapinduzi ya mwaka 1964. Hebu aangalia tunawapa madaraka Mhe. Naibu Spika.

Hebu angalie pale katika jimbo langu Mhe. Naibu Spika, kwenye Jimbo langu la Wawi. Katika ardhi ya Makaani ni sehemu ya hadidurejea iliyopewa kamati yetu. Taarifa zimo, sitaki kuzi-*refer* munaweza mukazi-*refer* wenyewe, lakini Mhe. Naibu Spika, pale sisi ndio maisha yetu tuliopoteza pale kwenye ardhi ya maweni, tunapanda tungule, mihogo, nyanya na sijui nini, tumezaliwa sisi tukasoma kupitia hivyo, tukasomesha watoto wetu. Lakini sasa pale wamekuja majuja wa mamejuja, hawa watendaji wa siku hizi wameichukua ile ardhi na sasa tunafanya manokoa katika nchi yetu.

Ingelikuwa wakoloni tungeliwapindua, lakini kwa sababu ni sisi, Mhe. Rais tuondolee hawa. Hebu aangalie leo kwa sababu tunampa *DC*, hebu aangalia viwanja alivyonavyo pale. Ninataka mu-*refer* hii kwenye ripoti yetu kwamba mama mmoja anaitwa Mwanajuma gani sijui anamiliki viwanja vitano. Sheria inasema unaweza ukamiliki kiwanja kimoja cha kuishi katika nchi hii, halafu ukenda sehemu ukamilikishwa chengine, ukitaka kufanya biashara ukaweza kupata chengine.

Huyo mama hii nchi si yake, hii nchi ni yetu tulipindua sisi, tumewapa dhamana na hizi dhamana tunaziweza sisi, si kama hatuziwezi, sisi dhamana wenyewe tunaziweza. Lazima muweze kufanya mambo vizuri katika nchi hii, hii nchi si yenu, tumewasomesha kupitia kodi zetu mukapata hiyo elimu na tukawapa nafasi mutuongoze.

Leo munaanza kujifanya Mhe. Waziri, katika hili ninakushauri mbali ya maelekezo uliopewa na kamati yetu, wale wote wafutie ardhi uchukue mwenyewe serikali, pale utakapotumia matumizi ya maendeleo ya nchi hii, utatueleza ili tuweze kujua. Lakini sio mtu anakuwa kama joka la mdimu, wamemiliki ardhi ile Mhe. Naibu Spika, katika miaka yote hawajaiendeleza pale, sisi hatupati kwenda kuchunga pale, hatupati kuchimba jiwe, hatupati kulima, wao wameiweka tu hii ardhi kule.

Tatizo Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tatizo lipo pale Vitongoji, Makaani kule hakikisha kwamba ili haki itendeke ardhi irudi serikalini ili na hawa waliochukua kama joka la mdimu, sisi tunataka tulime wao wanatuzuia wameiweka tu hii. *This is a public asset,* sio *asset* ya mtu mmoja. *That's a national cake must be even distributed,* sio mtu akachukue ardhi yote, sisi wengine tuwe hatuna pa kukaa. Mhe. Naibu Spika, katika hili lazima uwe makini sana, tutakupa mashirikiano ya hali ya juu kuona kwamba haki inatendeka katika nchi yetu.

Hawa vijana muliowapa madaraka, Makatibu wenu Wakuu sijui, Maafisa Tawala sijui nani, hawa wameshapata walivyopata viwanja vifutwe vyote virudi serikalini, serikali wananchi watumie na pale serikali itakapoamua sasa kutumia kwa mambo mengine ya maendeleo, tuje tuelezwe sisi ni walimu wazuri wa kuwaeleza wananchi, wala sio wakaidi wananchi wameshafahamu. Lakini hawa muwafutie.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninaiunga mkono ripoti hii, ninampongeza tena mwenyekiti wangu Mhe. Ali Mzee Ali, na mimi tukijaaliwa nipo mbioni kushauriana na *Professor* Idriss Rai ili tukampatie degree ya hali ya juu katika udhamini kwenye masuala haya ya *Political Science and Economy*. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa tunampa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, na baadae kwa upande wa uchangiaji tutamalizia kwa Mhe. Mohamed Mbwana Hamad.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii jioni hii na vile vile nikupongeze kwa dhati kabisa jinsi ulivyoendesha kikao asubuhi ya leo, uliposhuhudia malumbano yale na ukatumia hekma na busara zako za kijitu kizima.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, ninataka kutoa pole ya kifo cha ghafla kilichomkuta Mjumbe wetu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, kwa kufiliwa na mama yake na alikuwa akinywa chai katika mkahawa wetu nyuma hapo na yeye mwenyewe akapinduka kidogo, hakupata fahamu mpaka Waheshimiwa

wenziwe wanawake wakamsaidia ndio tukamchukua tukampeleka uwanja wa ndege na hivi sasa yupo Pemba na ninategemea maziko yatakuwa leo saa kumi.

Kwa hivyo, nilikuwa ninataka kutoa pole kwa kifo hicho na sisi vile vile, tukae tukikumbuka ni watarajiwa wa maiti wakati wowote na saa yoyote na dakika yoyote. Hapa tunapita njia tu, tukashindana na kulumbana humu ndani. *Alhamdullah, Innalillahi waina ilahi Raju-un.*

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nianze kuipongeza kamati iliyoongezwa na Mhe. Ali Mzee Ali, kwa kazi nzito waliyofanya kwenye kipindi cha mvua na jua. Baada ya hapo ninataka nimpongeze Mhe. Waziri, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kwa uwezo na nguvu zake na muda mfupi tu, tumeiona wizara hii inavyoanza kuelekea. Kipindi kifupi hivi sasa hatujasikia malumbano ya migongano ya ardhi kutoka kuikamata wizara hii, ninavyokumbuka mimi kwa upande wangu, maana yake kila mmoja na mchango wake. Nikupongeze sana Mhe. Waziri. (*Makofi*).

Nije kwenye watendaji wako Mhe. Waziri, yaani Wakurugenzi wako wa ardhi, nao wamekuwa chanzo kidogo cha migogoro ya ardhi. Ardhi moja inapimwa hati mbili. Alizungumza Mnadhimu wangu wa Chama cha Mapinduzi, chama kikubwa kuliko chama chochote Tanzania. Haya ndio yanayochangia matatizo haya, ardhi moja itatolewa hati mbili na mifano ipo hai.

Nije kwa upande mwengine wa ufutaji wa ardhi Mhe. Naibu Spika. Ufutaji wa ardhi kwa Wazanzibari kidogo imekuwa wanaonewa na wana haki yao katika nchi hii. Huwezi kumfutia tu Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hajaweza kujenga. Pesa ni ngumu na utaratibu wake unajulikana.

Mimi nimkumbuke na tena nimshukuru sana Mhe. Mansour Yussuf Himid, enzi zake. Haya tuzungumze ukweli ijapokuwa kwa uchungu. Sikukumbuka kufuta ardhi yoyote Mhe. Mansour Yussuf Himid, kwa kipindi chote alichokaa uwaziri kwa kuwajali wananchi wa nchi wa visiwa hivi.

Sasa utamkuta Mkurugenzi tu atakwenda atakuta kiwanja kimetiwa ukuta atakulazimisha ujenge, pesa ukazitoa wapi, wewe maskini pesa zitoke Uarabuni ziletwe zijengwe. Leo mnyonge wa nchi hii unakwenda kumfutia kiwanja Mzanzibari wa nchi hii, kitu cha kusikitisha sana Mhe. Naibu Spika. Iangaliwe na kuhusu kwenye ujenzi, mtu uwezo wake ni kujenga nyumba ya chini, Mkurugenzi wa mipango miji atakwambia wewe ujenge nyumba ya ghorofa, uwezo upo wapi. Ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Naibu Spika.

Na migogoro mengine yote hii inasababishwa kupelekwa Mahakamani kupewa kazi nzito Mhe. Haji Omar Kheir, katika Mahakama ya Ardhi, ninafikiri hivi sasa ndio kunakoongoza kesi kuliko Mahakama Kuu, hivi sasa kwa migogoro ya ardhi ya nchi yetu. Kuna Mahakimu wameongezwa watatu na bado hawajatosha, kesi zimekuwa za mgongano na vitu vyengine hata havielekei.

Kwa hivyo, niwanasihi sana wenzangu Wakurugenzi wa Ardhi wanapoangalia kupima waangalie wasije wakatoa hati mbili mbili au tatu tatu kuja kutafuta migongano. Mifano ipo hai wala haitaki tochi kuja kumurika.

Mhe. Naibu Spika, nimuomba sana Mhe.Waziri dhamana wa wizara hii hasa kwenye jimbo langu kumekuwa na migogoro mikubwa ya ardhi na Mhe. Waziri, alipokuwa anakaimu Wizara ya Kilimo aliniahidi tutakwenda kuna sehemu, lakini kutokana na majukumu pengine yamemzonga, safari yenyewe imekuwa mbaya, hatukuwahi kufika tena.

Kwa hivyo, ninawanasihi sana Masheha wanaoneshwa mipaka yao, sisi Wawakilishi wa jimbo tuna kazi sio ndogo. Leo mtu wa Mkongoroni anagongana na mtu wa Kitogani, leo mtu wa Kitogani anagongana na Paje, Paje anagongana na Jambiani, Shehia yote moja hujui utamuokoa nani. Kwa hivyo, Mashekha waonyeshwe mipaka yao ya ardhi ili watu wasije kupata kugombana katika mipaka ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, kwenye masikitiko yangu kidogo naomba uniruhusu kusema Mhe. Spika. Tunaitwa Waheshimiwa kutokana na wananchi kwa kukubali Katiba hii ndio tukaitwa Waheshimiwa. Tumeitwa Wajumbe kwa ajili yao, wananchi wameamua kutuchagua, nendeni huko mukazungumzie masuala yetu. Kwa hivyo, itakapofika pahala kama hatutimizi wajibu wetu, ninarudia yale maneno ambayo tunasema humu Barazani, kwamba tutakwenda kuulizwa Waheshimiwa Wajumbe maneno yale kila mtu ajue mwenyewe kwamba ipo siku tutakwenda kuulizwa namna gani tumetimiza wajibu wetu katika kuendeleza maisha ya wananchi, hatutofanya hivyo. Mhe. Naibu Spika, hayo maneno si yangu aliyazungumza Mhe. Spika, siku ya Ijumaa tarehe 19 Oktoba, 2012.

Kitendo kilichotokea leo ni kitendo cha kusikitisha. Mimi jana nikahoji kuhusu hospitali yangu hapa kwenye Jimbo la Muyuni, akatoka Mjumbe mmoja tu akaitetea hali ile, lakini shida ya mwenzio ni gunia la usufi, kitanda usichokilalia hukijui kunguni wake.

Leo ushahidi umepatikana hapa Mhe. Naibu Waziri, amejibu hapa, hichi chombo cha wananchi Wizara ya Afya, wizara ambayo Dr. Ali Mohamed

Shein kaiteuwa kuwa ni Wizara ya Afya, sio kwa sababu ni Wizara akaipa umuhimu, ni kuwajali wananchi. Mimi ninamshukuru sana Dr. Shein kwa hilo, kafanya mengi kwa Wizara ya Afya; kaiondoa huduma ya mama wajawazito kwa kujali wananchi wake. Leo Naibu Waziri watu wanatusikiliza, chombo kizito kama hichi, tunafanya nini.

Humu Mhe. Naibu Spika, kuna milango mitatu ya kuingilia ukaitwa Mheshimiwa. Mlango wa kwanza utakuwa ni jimbo la Ikulu, mlango wa pili ni viti maalum na mlango wa tatu ndio sisi, tuliokuwa hatukubahatika kupata majimbo kutoka Ikulu. Tumetoka kwetu tumechukua dhima kwa wananchi tutakwenda kuulizwa, tuje tuwatetee.

Mimi Mhe. Naibu Spika, nimestahamili sana Wizara ya Afya yamezungumzwa humu mengi ya uwongo. Leo nimekuja kusikitika Mhe. Naibu Waziri, anakuja kuniambia mtoto wangu nimpeleka kule, mimi sina mtoto nimempeleka kule nimekuja kuomba msaada tu. Leo tokea asubuhi hapa tumekuja kulumbana. Leo mutanitambua, wewe nani, mimi nani.

Hatuwezi kufanya kazi namna hiyo Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Twende kwenye taarifa tuliyonayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa hilo.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naona nimalizie hapa. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Sasa tunamaliza kwa wachangiaji Mhe. Mohamed Mbwana Hamad na baada ya hapo tutamwita Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na baadae tutamwita Mhe. Waziri (OR) Makamu wa Pili wa Rais, na mwisho na tutamalizia na mwenyekiti wetu kufanya majumuisho.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Lakini nichukue nafasi pia ya kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule ya kuchunguza migogoro ya ardhi na kamati yake Mhe. Ali Mzee Ali.

Na pia, ninachukua nafasi hii kumpa pole ndugu yetu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, kwa kifo cha mama yake kilichotokea nyakati za mchana wa leo Mwenyezi Mungu ampe moyo wa subra na familia yake na pia mama huyu amlaze mahali pema peponi, *Amin.*

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi wangu huo, mimi nitazungumza machache sana katika hotuba hii ya migogoro ya ardhi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli migogoro ya ardhi hapa Zanzibar imekuwa ni kero la muda mrefu kama ilivyoripotiwa na Kamati iliyokwenda kulichunguza suala hili la migogoro ya ardhi. Lakini Mhe. Naibu Spika, tukijiuliza kwamba migogoro hii inasababishwa na nani na imesababishwa na nini. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi hapa ninakosa jawabu, kwa sababu tunaotunga sheria ni sisi, lakini sheria tunashindwa kuzifuata.

Kwa hivyo, mimi niwaombe watendaji wanaohusika na kuzisimamia sheria, wazisimamia sheria kama ilivyo ili wawe waaminifu kwa wananchi wanaowasimamia na pia wawe waaminifu kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, ninafikiri tunajua kwamba sisi sote ni wachunga na kila mchunga ataulizwa namna gani alivyokichunga kile anachokisimamia. Kwa hivyo, kama kiongozi ni mchunga juu ya anaowasimamia.

Mhe. Naibu Spika, ninataka nirudie kidogo katika kitabu chetu cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, kila siku ya Mungu hapa asubuhi kabla ya kitendo chochote Mhe. Spika, Naibu Spika au anayeongoza kikao anatusomea dua ya kuiombea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini pia anatusomea dua ya pili ya kuliombea Baraza la Wawakilishi.

Naomba kunukuu vipande vichache tu katika dua hizo. Dua ya kwanza ya kuiombea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, dua inaendelea kipande ninachotaka kusema kinasema hivi:-

"Tuepushe na tamaa mbaya, chuki na ubinafsi"

Mhe. Naibu Spika, niulize tamaa mbaya ni ipi, chuki ni ipi na ubinafsi ni upi. Lakini ikiwa tupo katika migogoro ya ardhi, ardhi iliopo ndani ya nchi yetu, ardhi ambayo ni ndogo kwa sababu sisi tuna visiwa, ardhi ambayo tumo ndani ya maisha hatujui miaka inayokuja, watoto wetu watakuwepo wapi. Je, nini maana ya neno liliomo ndani ya dua hii, "utuepushe na tamaa mbaya, chuki na ubinafsi".

Lakini niende katika dua la kuliombea Baraza la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, dua imeanza hivi:-

> "Tunakuomba Mwenyezi Mungu mwenye rehma, mwingi wa utukufu, muumba mbingu na ardhi, uliyeweka katika dunia hii serikali za wanadamu na Mabaraza ya mataifa ili haki itendeke kwa kufuata sheria kama vile upendavyo wewe"

Sio wewe Mhe. Naibu Spika, kama vile upendavyo wewe Mwenyezi Mungu.Nini maana ya maneno haya. Tunayafahamu vipi maneno haya tukiwa tunayasoma kila siku na tukiwa watendaji wa serikali na tukiwa wasimamizi wa haki za watu na tukiwa tunajitanguliza kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli migogoro ya ardhi ni mingi Zanzibar, inatisha na kuna hatari ya watoto wetu wanaokuja baada ya miaka 20 au 30 ijayo kukosa pahali pa kukaa kwa kuvamiwa na watu wenye tabia mbaya, watu wasiojali maslahi ya nchi, watu wanaojijali wao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mzunguko mzima wa migogoro ya ardhi tuliyonayo, nina kitabu hapa kimeandikwa "Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Zanzibar, eneo la ardhi sehemu ya nyuma ya Chuo cha Afya Mbweni".

Mhe. Naibu Spika, imetumwa Kamati Teule kuchunguza baadhi ya mambo na baadhi ya maeneo. Lakini tukichunguza kuna matatizo na migogoro iliyopo hapa Zanzibar, basi hata majengo ya serikali na maeneo ya serikali ambayo yameshapewa hati miliki yanavamiwa na mwisho wake lengo lililokusudiwa halifikiwi.

Kama Chuo cha Afya Mbweni kuna viwanja kumi wamepewa watu kwa nyumba zao binafsi. Viwanja hivi kwa kweli inasikitisha kwa sababu eneo hili kwa mujibu wa ripoti hii inaelezwa kwamba eneo hili limetengwa kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Rufaa kwa ajili ya Wazanzibari na kwa manufaa ya wanafunzi wanaosoma chuoni pale.

Mhe. Naibu Spika, tutafika wapi. Chuo kina mamlaka, kina hati miliki, lakini kuna ukuta wa chuo umevunjwa na watu wamejenga, Mkuu wa Chuo amemaliza maombi ya kila taasisi inayohusika, hatua inayochukuliwa kulinusuru eneo lile hakuna.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na matatizo haya yanayotukabili Zanzibar kama watendaji hawakuwa makini, basi Zanzibar tunaipoteza *plan* yake, tunayapoteza malengo ya mapinduzi, tunapoteza kila ambacho kinaweza kuleta haiba, nuru na uzuri wa Zanzibar katika malengo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abeid Aman Karume, Rais wa mwanzo wa Serikali ya Zanzibar, alikuwa na lengo zuri. Tukiangalia vyuo vingi vya Zanzibar vimejengwa kando ya mji ili kila chuo kipate kujitanafasi na wanafunzi wake ili ile haja ya chuo husika ikamilike. Lakini leo migogoro iliopo katika ardhi kila mtu anawania eneo nyeti ajenge yeye na watoto wake na watu wenye pesa nyingi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaiomba serikali sana ilizingatia sana suala hili, vyenginevyo Zanzibar itakuwa ni chaka la kukimbilia wakubwa maeneo nyeti na kuwapotezea watoto wetu wajao maeneo ya kukaa.

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Afya ni chuo cha Wazanzibari, wamekwenda viongozi mbali mbali akiwemo Rais wa Zanzibar, akiwemo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na wametoa maoni yao kwamba maeneo yaliyovamiwa yaachiwe chuo na mpaka leo hatua yoyote haijachukuliwa.

Naiomba serikali miongoni mwa masuala ya kuyafuatilia basi hili ni moja. Kulihakikisha kwamba eneo la chuo linaachiwa huru kwa kujenga majengo yake.

Mwisho nizungumze na watendaji wale ambao kamati ilikwenda kuwasaili au kuwauliza na kutaka baadhi ya vielelezo na watendaji, wakashindwa kutoa vielelezo. Serikali ianze kuchukua hatua kwa watu hawa kwa sababu tunapokwenda katika kamati, mimi nilikuwemo katika Kamati Teule ya *ZECO* ya Shirika la Umeme, tuliwakusanya wafanyakazi kuwauliza mambo mbali mbali, walichotwambia ni hichi, aah! kamati gani, zimepita kamati ngapi hapa, hakuna kinachokuwa na nyinyi njooni hapa mutupumbaze, muchukue pesa zenu halasi.

Je, kamati zetu za Baraza la Wawakilishi tumalizie hapo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Asaa Othman Hamad, jana alisema hivi na mimi ninataka niseme maneno yangu kwa sentensi ya Mhe. Asaa Othman Hamad na nimalize neno jengine.

Afro mama tunakuaga, hukutufanyia baya. Jamani tumejenga au tumeunda *CCM* kutufanyia mabaya.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi sina budi kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi kuzungumza juu ya ripoti ya Kamati Teule inayoshughulikia masuala ya migogoro ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, ninakumbuka kwamba nilipokuwa ninaliomba Baraza lipitishe bajeti yangu na kwa kuwa walizungumza sana juu ya masuala ya migogoro ya ardhi, Mjumbe mmoja akapendekeza kwamba anaona ni vyema iundwe Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza migogoro ya ardhi.

Nilikubali mimi mwenyewe tena nilikubali kwa moyo thabiti kabisa na watu wakashangaa kwamba imekuaje hata nikakubali kuunda Kamati ya kuchunguza migogoro ya ardhi, walishangaa sana. Mimi mwenyewe nilikuwa ninajua kwamba kutokana na malalamiko yaliyotokea katika mazungumzo yale ya bajeti, kama kamati itaundwa basi itanisaidia sana katika kuongoza wizara hii.

Leo nimepata *documents* hizi mbili, kwa kweli kwangu mimi kwa ajili ya kuendesha wizara ni hadidurejea nzuri sana. Mimi ninamshukuru sana Mhe. Ali Mzee Ali, pamoja na kamati yake kwa kazi kubwa waliyofanya katika kufanya utafiti juu ya kuchunguza sababu mbali mbali za aina mbali mbali ya migogoro ya ardhi Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ninataka niseme tu kwamba migogoro ya ardhi haikuanza leo. Ndio maana hata hiki kitabu chenyewe utaona sheria ya mwanzo kabisa iliyoandikwa kushughulikia masuala ya ardhi na hasa *public land*, iliandikwa mwaka 1921 wengine hata hatujazaliwa. Ina maana yalikuwepo mambo wakati huo yaliyosababisha serikali kukaa kitako na kuandika sheria. Kwa hivyo, hayakuanza leo yalianza zamani.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba migogoro ya ardhi ipo karibu ulimwengu mzima, haipo Zanzibar peke yake. Kila ukisikiliza taarifa za habari, ukisoma magazeti Tanzania Bara, Kenya na kwengineko migogoro ya ardhi ipo na inaendelea kuwepo. Tunachotakiwa kufanya tuishughulikie. Kwa hivyo, ripoti ya kamati hii itatuwezesha kuishughulikia migogoro ya ardhi iliopo hapa kwetu Unguja na Pemba. Hiyo ni kazi ya kudumu, na ni kazi ambayo kila anayekwenda katika eneo la ardhi kazi hii atalazimika aifanye.

Mhe. Naibu Spika, nataka nirudi katika ile nakala ya gazeti la kweupe. Ukisoma katika gazeti la kweupe hii iliyotiwa katika hii ripoti kwenye masuala ya ardhi, Azimio la Jamuhuri ya Zanzibar. Wakati Mzee Abeid Aman Karume alipotangaza kuwa ardhi ni mali ya serikali, azimio lilisema hivi. Ardhi yote iliyo khalia ni rasilimali ya serikali, ni marufuku kwa mtu yeyote kuingilia ardhi kama hiyo, yaani ardhi khalia kwa kupanda kitu chochote kile bila ya amri na matengenezo ya serikali.

Kifungu hiki ni muhimu sana na wananchi wote wanatakiwa wakielewe, kwamba ardhi khalia ni mali ya serikali na azimio lilitangaza hivi na ndio maana hii sheria iliyokuja hapa namba 12 ya 1992 ilitilia mkazo azimio hili la ardhi kuwa ni mali ya serikali moja kwa moja. Hapa tunatakiwa tupafahamu sote, tusipopafahamu hapa basi migogoro haitokwisha katika nchi hii na tutaendelea kuwa nayo siku hadi siku. Tupafahamu vizuri sana hapa katika kifungu hiki ni pahala muhimu kweli kweli katika kazi zetu tunazozifanya.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachotaka kusema kuwa sitakiwi kujibu hoja ya ripoti hii au michango ya Wajumbe waliyozungumza hapa, ninachotakiwa mimi ni kupokea maelekezo ya Wajumbe na kwenda kuyafanyia kazi, sio kujibu hoja, kwa sababu mimi sikuwasilisha hii ripoti, imewasilishwa na Mwenyekiti, kama kuna hoja za kujibiwa basi Mwenyekiti atazijibu, lakini mimi nipokee tu. Nawashukuru Wajumbe wenzangu kwa kutoa michango mizuri kabisa juu ya utaratibu mzima wa kushughulikia migogoro ya ardhi. Hii ripoti inakwenda serikalini, serikali bila shaka itatakiwa kutekeleza yaliyomo katika ripoti hii, hilo nalijua vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nasema ni vizuri Wajumbe nao na wananchi kwa jumla, wasije wakafikiri kwamba ardhi ya Zanzibar tangu Mapinduzi mpaka leo haijatupatia faida yoyote, wasije wakafikiria hivyo. Hiyo ndio itabidi nieleze maneno machache kidogo faida ambayo tumeipata kutokana na ardhi ya Zanzibar katika kipindi hiki ambacho kinaendelea.

Mhe. Naibu Spika, nataka kusema kwamba baada ya Mapinduzi eka zaidi ya 66,000 ziligaiwa kwa mpango wa eka tatu tatu kwa kupewa wananchi. Maana yake kama ni eka tatu tatu basi familia 22,000 zilifaidika na ardhi hii, na hii ilikuwa ni kutekeleza suala hili ambalo limetolewa kwenye gazeti. Sasa tujiulize, wananchi ardhi hii wameitumia inavyotakiwa au wameiingiza katika migogoro. Hili swali la kwanza tujiulize. Hizi eka 66,000 zilizopimwa wakati huo ambapo hivi sasa ziko tayari zinatumika kwa jina la eka na watu wanapata faida, hili ni kosa moja limetokea katika maswali ya ardhi. Lakini serikali ilijitahidi kuzigawa eka 66,000 kwa ajili hiyo.

Mhe. Naibu Spika, *master plan* ya mwaka 1982 viwanja baina ya 10,000 mpaka 15,000 viligaiwa kwa wananchi katika kipindi hicho, wananchi waligaiwa viwanja kutokana na ardhi hii tuliyonayo sasa hivi. Miaka ya 1990 maeneo 400 yametengwa katika maeneo ya uwekezaji Unguja na Pemba, yaani hayo maeneo 400 yaliwekwa kama ni maeneo ya uwekezaji kwa Unguja na Pemba, faida gani iliyopatikana. Faida iliyopatikana katika kutenda hayo ni kwamba hoteli zaidi ya 300 zimejengwa na zinafanya kazi.

Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, asilimia 70 ya pesa za kigeni zinatokana na hoteli hizi ambazo zimejengwa, yaani utalii huu ambao tunauzungumza sasa hivi. Nimeona nianze na hilo kidogo kabla sijaenda huko. Asilimia 27 ya pato la taifa linatokana na utalii, ni kwa sababu ya matumizi ya ardhi. Tunategemea kwamba kilimo pamoja na karafuu yanatupa asilimia 30 mpaka 32 ya pato la taifa, lakini tunategemea tutakapofika mwaka 2015 basi utalii utaipita karafuu bila shaka yoyote ni kwa matumizi haya ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, sisemi kwamba hakuna makosa yaliyofanyika katika ardhi, sisemi hivyo. Nasema yako makosa yanafanyika katika ardhi, lakini zipo faida zinapatikana kutokana na ardhi hii ambayo tunayo katika nchi yetu, hivyo ndio nakusudia kusema. Sasa tufanye nini baada ya maelezo ya Wajumbe hawa.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba napenda niwajulishe Waheshimiwa Wawakilishi, ili tuweze kuijua migogoro ya ardhi na kuweza kuitatua. Zanzibar sasa hivi tumeanzisha utaratibu wa kuwatambua wamiliki wa haki ya matumizi ya ardhi kwa kuwapimia na kusema taarifa zao kwa kuwajazisha fomu za madai, kitaalamu inajulikana kama ni *claim form*, yaani fomu za madai kwa ajili ya ardhi zile ambazo wananchi wamekaa nazo. Unaweza kusema hii itasaidia nini. Mhe. Naibu Spika, hii itasaidia kumjua mtu aliyekuwa na ardhi jee ni yake? Kaipata kihalali au amevurunda tu? Ndio maana ya usajili huu tunaoutumia hivi sasa wa ardhi.

Mhe. Naibu Spika, Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi watilie mkazo sana suala hili la kuwataka wananchi waingie katika suala la usajili huu wa ardhi, kwa sababu hapa ndipo itakapojulikana mbichi na mbivu ya mtu anayemiliki ardhi. Maana katika suala la usajili anajulikana mtu namna alivyoipata ardhi, kairithi, kapewa anazo shahada za kupewa au kaichukua hivi hivi kiholela.

Hii ndio itakayofanya kazi katika kujua matatizo mbali mbali ya ardhi. Hii hatua tunaichukua sasa hivi na tumeshaanza kazi hiyo ya kufanya hivyo *system* ya *registration* ili tujue kwamba ardhi hizi ziko katika mikono ya watu wetu kihalali. Sasa kama kuna mtu ana eka 30, sijui kama atakuja kuandikisha eka 30, na kama hakuja kuandikisha eka 30 maana yake anatuambia hizo eka tukachukue wenyewe ndio maana yake hiyo, hakuna njia nyengine.

Mhe. Naibu Spika, katika kupokea maelezo ya Wajumbe hawa nataka kusema yafuatayo.

Nataka kusema kwamba wawekezaji wasiolipa kodi. Mimi nashukuru kwamba kuna Wajumbe wameeleza hapa kuwa kuna wawekezaji hapa hawalipi. Sisi tumeweka ma-*agent* wa kukusanya kodi ambao ni *ZRB*. Nawataka *ZRB* watupe taarifa kama kuna muwekezaji halipi kodi ili sisi tumnyang'anye hiyo ardhi na tumtafute mtu mwengine tumpe, hilo ni suala muhimu kabisa tulifanye.

Halafu wawekezaji wenye miradi hewa. Imezungumzwa hapa miradi hewa. Kuna ardhi mtu kaichukua kaiweka haitumii. Hili zoezi Mhe.Naibu Spika, tumeanza na mpaka sasa hivi najua kwamba kuna maeneo manane tayari

tumeshafuta katika utaratibu wa namna kama huu, na mengine tunaendelea kuyafuta yaliyokuwa katika utaratibu kama huu, na ardhi hiyo tunataka tuirejeshe serikalini, ndivyo tunavyotaka kufanya sasa hivi.

Kwa hivyo, wawekezaji hawa ambao wataalamu wa ardhi wanaitwa *speculators* ni watu ambao wamechukua ardhi na wanakwenda kuranda Ulaya kutafuta watu wa kuja kuwapa ile ardhi. Ardhi ni mali ya serikali, huwezi kuiweka ardhi.

Mhe. Naibu Spika, kuna ardhi zimezuiliwa zinafika mwaka wa 8, 10, mpaka 15 sasa hivi zimezuiliwa na zimezungushwa makuta basi. Ardhi zile zote nasema itabidi tuzirejeshe kwenye mikono ya serikali na tunawaweka wawekezaji *serious* tuwape ardhi zile. Hilo zoezi nataka kusema kwamba tumeshaanza.

Halafu kuna suala moja ambalo ni muhimu sana na linatuhusu sisi vile vile. Mtu anatakiwa apate kiwanja kimoja akajenge, anachukua kiwanja kimoja lakini hakijengi. Sheria inasema baada ya miaka miwili kiwanja kile tumnyang'anye kwa sababu hakukijenga, ndivyo sheria inavyoeleza, kiwanja kimoja ameshakaa nacho hakukijenga. Sasa unamkuta mwengine ana viwanja vitatu au vinne hajavijenga vyote, anaigeuza ardhi ni biashara, anataka aichukue ile ardhi halafu akauze kwa watu wengine. Nataka kusema hivi, tuondoe muhali, tunaanza kufuta viwanja vilivyokaa zaidi ya miaka miwili bila ya kujengwa. Tuondoeni muhali.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walifahamu suala hili. Wasije wakapenya kwa mlango wa nyuma wakamuambia Mhe. Waziri, huyu muachie kwanza. Hapana, sheria imeshavunjwa hapo ni lazima tuchukue ardhi yetu ile, kwa sababu keshakaa nayo kwa muda mrefu hajaijenga, lazima tuondoeni muhali katika hili.

Mhe. Naibu Spika, maeneo yaliyotolewa kinyume na utaratibu ambayo humu mengine yamo yameelezwa. Waturuhusu wizara maeneo hayo tuyarejeshe serikalini, Waheshimiwa wasirudi nyuma katika hili, nawaomba sana. Hili ni jukumu letu sote, tutayarejesha maeneo yaliyotolewa kinyume na utaratibu serikalini. Nasema zoezi hili tumeshalianza. Pia, limeshaanza kuleta malalamiko hapa. Kuna maeneo yametolewa kinyume na utaratibu tumeyafuta, malalamiko yameanza kuja na watu wanatufuata migogoni, wakati eneo lilitolewa kinyume na utaratibu. Tutayarejesha serikalini.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo yametolewa hati mbili au tatu eneo moja, nani atakwenda kujenga ardhi katika maeneo yale. Kwa sababu ukienda kujenga anakuja anakuambia aah! Hapa pangu mimi, mimi hati ninayo, na

mimi hati ninayo. Hii Mhe. Naibu Spika, ndiyo iliyonifanya mimi sasa hivi nikitaka kutoa kiwanja au kusaini hati nataka Mkurugenzi wa Ardhi awepo au msaidizi wake, na huyo mtu aliyekuwa anapewa hati awepo mbele yangu nimuone. Ninamuuliza Mkurugenzi pale.

Mkurugenzi unaniambia nitie saini hati hii, je, huyu unayempa hakuna mgogoro hapa unieleze kabisa nijue. Nashukuru anafika wakati anafanya mashaka, ananiambia bora hiyo hati nipe mwenyewe usiitie saini kwanza, nitakwenda kuishughulikia kwanza nijue ukweli wa suala hili.

Mhe. Naibu Spika, siku zote nasema ukitia saini kama unayesainisha mabuku ya skuli ya hesabu basi utafanya makosa, lazima utafanya makosa. Huwezi kusema umekuta rundo la mafaili pale juu ya meza yako halafu unasema leo yatanitambua haya, unakaa kitako, kwekweche unaliweka huko, unachukua jengine kwekweche unaliweka huko. Mna madudu mule huwezi kutia saini, huwezi tia saini namna kama hiyo ni lazima umwite mtu njoo bwana, ukiwaita watasema aaa! Huyu waziri gani, waziri hakujiamini hata kidogo, mpaka awaite watu wamuone mbele. Sio kujiamini, migogoro mingi na ni lazima tuipunguze. Sasa suala hili tunalichukulia hatua za makusudi ili tuweze kuyazuia masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, ripoti hii imezungumza machache tu katika migogoro ya ardhi, kuna mengine mengi sikuyaona humu, labda kwa sababu hayakuwemo kwenye hadidu rejea ambapo mimi baada ya kufika pale nimeshajifunza kwamba yapo mengime mengi kabisa, tuna kazi kubwa sana ya kufanya kuona kwamba tunapunguza migogoro ya ardhi katika nchi yetu hii. Tutaipunguzaje kama ilivyosema hii ripoti, tufuate sheria, kanuni na utaratibu peke yake tutapunguza.

Lakini hii isilete muhali, nawaomba wenzangu sana isilete muhali hii. Siwaombi Wajumbe wa Baraza tu, nawaomba mpaka viongozi waliokuwepo nje ambao sasa hivi wananisikiliza katika hili wasilete muhali, msifuatwe fuatwe migogoni wakati tunapochukua hizi hatua, hii migogoro imeshachosha sasa hivi, watu wanavunjika moyo. Kwa hivyo, tufanye kazi tuliyokusudia, tubadilike sasa hivi. Mhe. Rais anasema tubadilike sio *business as usual* sasa hivi, ni lazima tubadilike.

Kwa hivyo, tunalazimika kubadilika katika kufanya kazi hii, tutalishughulikia suala hili na mimi *Inshaallah* namuomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe katika kufanya mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, hakuna kitu ninachokichukia mimi kuliko kutoa ahadi au kulitamka neno katika Baraza hili halafu likawa halina ukweli, sipendi sana.

Hii ripoti kuna mahala imegusia suala la Ali Muradi, kwamba nilikuja kwenye Baraza hili nikasema kwamba mgogoro umemalizika, nilikuwa na sababu. Mimi mwenyewe nilimwita Ali Muradi ofisini, nilipoona tunataka kuelekea kwenye mgogoro nilimwita ofisini na alikuja, na shahidi ni Mhe. Waziri wa Fedha, alikuwepo tulikuwa pamoja.

Nikamwambia Ali Muradi nataka tumalize mgogoro, tusiingie kwenye mgogoro, tukutafutie kiwanja kizuri kikubwa tukupe tuondoke kwenye mgogoro. Akanipa sharti hili, akaniambia nitafutie kiwanja kizuri lakini katika eneo hili hili la Maruhubi kwa sababu hapa nataka kujenga kiwanda cha kushusha bidhaa kutoka melini moja kwa moja kuingiza katika maghala yangu hapa kwa kutumia mabomba makubwa kayaeleza. Ina maana nikikutafutia uko tayari katika eneo la Maruhubi, akaniambia niko tayari. Nikamwambia kama uko tayari basi mzozo wetu umeshamalizika. Nikawaomba maofisa wangu watafute kiwanja katika maeneo yale.

Mhe. Naibu Spika, nilishangaa. Mara namuona kafika akaniambia, unajua ule utaratibu siutaki tena mimi, akakataa siutaki tena mimi. Kwa nini mimi ninyang'anywe kiwanja hiki, nikaona eeh! Sina haja ya kuzozana, tunatakiwa twende vizuri tusizozane. Nikanyamaza kimya na ndio mpaka leo nimenyamaza kimya sijasema kitu katika suala hili.

Kwa sababu sina haja ya kuingia kwenye migogoro ya ardhi, lakini hii ilionesha alipokubali kwamba atafutiwe kiwanja, mgogoro huu ulikuwa ndio umemalizika tumpe kiwanja. Wanakuja watu wengine na migogoro huyu na huyu wananyang'anyiana, tunamwambia tukutafutie kiwanja kingine tunampa mgogoro unamalizika, unakuwa umeshakwisha hakuna matatizo tena. Sasa nikaona eeh! Hapa sijui nani kenda kuchochea tena, huyu bwana katubadilikia mara hii, nikasema basi, nikanyamaza sijasema kitu mpaka leo.

Vile vile, kuna lile suala la wawekezaji wanawanyanyasa wananchi. Mimi silipendi na wala sitaki litokee, kwa nini wawekezaji wawanyanyase wananchi? Lakini nataka niseme hivi na kwa sababu wananchi wananisikiliza hapa, kwa hivyo niseme vizuri wanisikie. Mwananchi anapokwenda mwekezaji maana hawa wawekezaji mnasema tunawapa maeneo ya kilimo na n.k, lakini hawa wawekezaji wako mbele zaidi kuuza maeneo yao, hata sisi tunaokwenda kupima hatujenda pale, wanauza wao kabisa.

Kuna mmoja amekuja juzi ofisini kwangu pale wameshamuuzia mtu. Mimi nikamwambia wewe kwa nini unauza ardhi kwani ardhi inauzwa. aa! Siwezi kuuza lile ni shamba letu la ukoo, kwa hivyo nataka *lease* yangu hii unitilie saini. Nikamwambia nikutilie saini hii *lease* yako, ina maana hii kampuni ni yako wewe.

Akaniambia sio yangu hiyo ni ya mzungu. Ni ya mzungu. Eeeh!. Haya, nikaisoma ile, mule ndani mna *memorandum of understanding* imeandikwa. Tukaisoma ile wewe bwana jina lako nani. Mimi jina langu fulani. Tukatizama *share holder*. Jina lake hamna mule na yeye mgongoni mwake ana ndugu zake wanafika 10 anawasimamia, humu jina lake hamna. Nikamuuliza hii *memorandum* humu jina lako wewe halimo. Akaniuliza hamna. Nikamwambia hamna, muna watu watatu humu. Mmoja ana *share* 51, huyu ndiye mwenye huu mradi, wa pili ana *share* 48 na huyu mmoja ana *share* moja. Wewe hamna jina lako humu. Ndugu yangu hamna, nikamwambia hamna hata mmoja humu. Nikamwambia wewe nikiitia saini hii keshokutwa utakuja kuniambia hapa mzungu kaninyanyasa kumbe wewe humo katika huu mradi wenyewe, watu wanatumia sheria zao, lakini wewe humo humu, hayo ni kweli. Akatoka pale akasema basi mimi narudi kwanza nyumbani nikafanye hiyo kazi kwanza, kumbe mimi simo. Nikamwambia humo wewe wala hayumo ndugu yako, wala hayumo ndugu yako mwingine, hammo nyote humu.

Maana yake atatulipa pesa na nini. Atawalipa pesa lakini mtanijia mimi baadae, mseme mzungu anatunyanyasa huyu hatupi pesa zetu, kumbe hammo kwenye ule mradi wenyewe. Haya yanatendeka, wananchi wetu ni lazima wawe macho kwenye masuala haya. Wanauza hawataki kusaidiwa katika masuala ya mikataba. Yaani wao wakishapewa pesa pale 50,000, 1,000,000, 5,000,000, au 10, 000,000 kisha anakwenda kwake anakwenda mbweo, anakuja kuingia kwenye matatizo mengine sasa. Pesa zimeshakwisha keshazitumia keshakwenda mbweo baaa! Keshashiba nyengine haziingii tena pale. Sasa linakuwa tatizo.

Hapa ndio panapokuja kuanza unyanyasaji wa wananchi na wakaanza kusema aah! Mimi pesa zangu yule mzungu ananinyanyasa hanilipi. Mzungu kasimama kwenye hii *memorandum* anasema alaa! Mimi sikujui wewe mimi namjua huyu, tena kuna baadhi ya wazungu wajanja anamuweka mbele Mswahili mwenziwe, yule Mswahili mwenziwe ndio anawazika wale waswahili wengine. Watu kumi kaleta majina pale, wote anasema sisi ndio ukoo wa ardhi hii. Nikamwambia rudi nyumbani katengeneze ndio urudi hapa tuje tuone kuwa wewe kweli umo humu na hawa ni ndugu zako utapata haki katika masuala haya usije kunirejea tena mimi. Mhe. Naibu Spika, haya ni matatizo ya ardhi tuliyonayo.

Sasa mimi ninachotaka kusema ni kwamba hii ripoti nategemea Wajumbe wataipitisha na kwangu mimi huu ndio msahafu nitakaokwenda kuufanyia kazi. Kwanza nataka niseme hapa sio kwa kupendelea, lakini huu msahafu una kurasa 4

Mhe. Mjumbe Fulani: Usiseme msahafu. Sema buku.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante, nakubali Mheshimiwa. Hili buku lina kurasa 488, kurasa hizi kuanzia ukurasa wa 9 mpaka 488 ni kurasa ambazo ni vielelezo vimetoka wizara yangu. Lakini kwa sababu kama alivyosema Mhe. Subeit Khamis hapa kuna baadhi ya nyaraka wamezikosa watu wangu kutokana na kwamba wengi pale ni wapya sasa hivi, tumebadilisha wafanyakazi pale nyengine hawakuzigundua. Unapomuhamisha mfanyakazi pahala, akikasirika basi baadhi ya *document* anaondoka nazo. Hilo ndio tatizo lililotokezea, sasa walipokuja wale wametafuta hawakuzikuta hizi, lakini hizi zote kuanzia nambari 9 mpaka 488 zimetoka katika wizara yangu, kwa sababu ziko ndani ya mafaili na wamezikuta watu pale. Kwa hivyo, huu ni ushahidi wa kuonesha kwamba hizi *document* zimetoka kwenye wizara, lakini kwa sababu ya upya wale wamekuja juzi juzi basi wameshindwa kuzigundua zile nyengine, kwa sababu pengine mtu kaondoka na waraka pale, anajua alichokifanya ndani ya waraka ule. Kwa hivyo, kaondoka nao na ndio maana haukupatikana wametafuta hawakuzipata nyaraka zile.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wayajue matatizo haya unapotaka kujenga yanatokea mahala popote na matatizo haya yametokea katika ofisi yangu kutokana na hali hii. Lakini sasa ninashukuru kwamba Wawakilishi wameshaniambia hapa kwamba tutashirikiana na watanisaidia katika kuona tunashughulikia matatizo ya ardhi. Nawaomba wanisaidie kweli kweli.

Sijisifu kwamba haya mimi nitayaweza peke yangu hapana. *Kidole kimoja hakivunji chawa*, ni lazima tupate mashirikiano ya hawa wote, wameshanipa matumaini makubwa kuwa tutashirikiana, wameniambia keshokutwa katika bajeti watataka mambo haya yote yawe nimeshayatekeleza. Kwenye bajeti mambo haya yote yatanishinda kwa pamoja, kwa miezi hii iliyobakia kwa pamoja yote haya, lakini yatakuwemo mambo humo tayari nimeshayafanyia kazi kwenye bajeti.

Lakini yote kwa asilimia mia moja, kwa yalivyo wingi wake yatanishinda. Sasa kama mtu kapewa kiwanja kwa miaka miwili imeshapita hakukijenga nitakirejesha, kaweka ardhi tupu pale hakuitengeneza nitairejesha serikalini. Kazi hii nitaifanya, na serikali bila shaka itaniongoza zaidi katika utekelezaji wa ripoti hii, hii ripoti inakwenda serikalini na itafanyiwa kazi serikalini bila shaka yoyote.

Mhe. Naibu Spika, mimi naiunga mkono ripoti hii na tupo tayari kuipokea *Inshaallah* na tupo tayari kuifanyia kazi *Inshaallah* nikiwa Waziri wa Ardhi,

Makaazi, Maji na Nishati. Msaada wa Wajumbe hawa ndio utakaonisaidia kufanikisha hili. Tunong'onezane bwana mambo haya, kama hatukunong'onezana itakuwa matatizo, *kidole kimoja hakivunji chawa* bwana, tuyashughulikie tutayapunguza haya na tunaweza kufika hatua kubwa kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, narudia kusema la mwisho kabisa. Muhali tuondoe, nasema tena muhali tuondoe, tusiwe na muhali katika utekelezaji wa ripoti hii. Mimi nitakuwa *very unpopular* katika ripoti hii. Muhali tuuondoe. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naipokea ripoti hii. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nipate kusema machache. Lakini kwa kuwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, takriban yale yote yaliyokuwa ya kuzungumzwa na serikali ameshayasema, hivyo nisingependa kuchukua muda wako mrefu. Isipokuwa nichukue fursa hii kuishukuru Kamati na Mwenyekiti wake kwa kazi waliyoifanya ya kutafuta njia ya kupunguza migogoro ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati Teule haiwezi kuwa muarubaini wa matatizo yetu ya ardhi, isipokuwa itasaidia katika kutafuta njia za kupunguza matatizo tuliyonayo. Kwa ufupi tunayo matatizo na tuna wajibu sote kwa pamoja kushirikiana na kuyatafutia ufumbuzi. Sio vyema hata kidogo kuyaona matatizo haya ni ya watu fulani, ni vizuri tukaelewa kwamba matatizo haya ni yetu sote, sisi viongozi pamoja na wananchi. Kama ilivyosema ripoti ni matatizo ya muda mrefu na yanahitaji ushirikiano wa pamoja kuyatafutia ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, leo hapa yalisemwa mengi, lakini moja katika maelezo ambayo yalikuwemo kwenye ripoti iliyozungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa, walizungumzia suala zima la kuwa serikali haina huruma na wananchi, serikali imedharau kuyashughulikia matatizo haya. Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba serikali hii siku zote itaendelea kuwatumikia wananchi na itakuwa ni kimbilio la wananchi, nia yake ni kuwatumikia wananchi na haitokuwa tayari hata siku moja, kuona kwa njia yoyote ile wananchi wanadhalilishwa au wanabughudhiwa. Serikali inachukua kila hatua ili kuhakikisha kwamba matatizo yanayojitokeza yanapata ufumbuzi. Mhe. Waziri, ameyaeleza kwa kina.

Mhe. Naibu Spika, leo kwa ufupi ninachotaka kusema kwamba sisi tutashirikiana na Kamati, tutashirikiana na Baraza lako tukufu kwa yale maamuzi ambayo yatafanywa na Baraza hili. Serikali kama kawaida yetu

tunashirikiana vyema na Baraza hili katika kutekeleza yale ambayo yataamuliwa na Baraza. Sisi kwa upande wetu tunasubiri maamuzi yatakayofanywa na Baraza hili tukufu ili tuyapokee na tukayafanyie kazi na tuje baadae tuyawasilishe hapa katika Baraza lako tukufu.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, naipongeza Kamati iendelee kufanya kazi kwa pamoja na kila tatizo basi tushirikiane katika kulitatua. Nia ya serikali ni kutoa matatizo yaliopo na kuondoa migogoro ya ardhi inayowakabili wananchi wetu. Kwa hivyo, yeyote yule anayeshirikiana na serikali katika hili tutakuwa pamoja ili kuyatafutia ufumbuzi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono maelezo yaliyotolewa na Kamati hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Mzee Ali (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi Zaznibar): Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Wajumbe wote wa Baraza hasa wale waliochangia na wale ambao wameleta barua za pongezi, waliotupigia simu, wa ndani ya Baraza na nje ya Baraza. Michango ya Wajumbe imesaidia sana katika kuweza kutupa moyo sisi Kamati, Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake na sasa tunaanza kufungua ukurasa mpya.

Mhe. Waziri, tumekusikia, tumepokea pongezi zako na yote uliyoyasema na sisi tuko pamoja na wewe. Nawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Waziri anasema tuwe naye, tumnong'oneze, kwa madhumuni ya kuweza kupunguza haya matatizo lakini si kumaliza. Lakini kwa sababu suala la ardhi ni endelevu basi tutaendelea.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, naomba kwanza nitoe maelezo yangu, nimefurahi kufika, kwanza napenda kuwataja wale wote waliochangia:

1) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2) Mhe. Hamza Hassan Juma,
3) Mhe. Salmin Awadh Salmin
4) Mhe. Bikame Yussuf Hamad
5) Mhe. Fatma Mbarouk Said
6) Mhe. Marina Joel Thomas
7) Mhe. Ali Salum Haji
8) Mhe. Asaa Othman Hamad
9) Mhe. Rufai Said Rufai
10) Mhe. Ismail Jussa Ladhu

11) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
12) Mhe. Hija Hassan Hija
13) Mhe. Mussa Ali Hassan
14) Mhe. Ashura Sharif Ali
15) Mhe. Mohammed Haji Khalid
16) Mhe. Abdi Mossi Kombo
17) Mhe. Subeit Khamis Faki
18) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
19) Mhe. Mohammed Mbwana
20) Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
21) Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapokea pongezi zote zilizotolewa na Wajumbe wote waliochangia ripoti hii na hata wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia, na wote tunawashukuru sana kwa kuiunga mkono ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, taarifa yetu haitokuwa kamilifu ikiwa hatukukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, wasaidizi wako pamoja na ofisi yako chini ya uongozi wa Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwa ushirikiano mkubwa uliotupatia kwenye Kamati katika kutekeleza kazi zake.

- Mhe. Naibu Spika pia tunawashukuru Makatibu Wakuu Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati,

- Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Maliasili,

- Wizara ya Mifugo na Uvuvi,

- Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba na Kusini Pemba,

- Wakuu wa Wilaya za Micheweni, Chakechake na Kati Kusini Unguja Kaskazini A,

- Maafisa Tawala wa Mikoa na Wilaya hizo,

- Mahakama Kuu ya Zanzibar,

- Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar, na

- Watendaji wa Taasisi zote hizo kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu hoja za Wajumbe, Mhe. Salmin yeye alitoa hoja na hoja yake ilikuwa zaidi nasaha, zaidi alisema hivi:

> "Mhe. Spika, kwa hiyo ile *terms* ya ardhi ni mali ya serikali ilitumika vipi, isipokuwa ilitumika vibaya kwa wakati ule. Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri, kwamba amepewa dhamana kubwa juu ya suala la ardhi na atajua kwamba amepewa dhamana kubwa juu ya suala la ardhi, pale Mwenyezi Mungu aliposema kwamba kutwambia wananchi kuwa ardhi na mbingu ni vyake, kwa hivyo sisi wanaadamu tusigombanie, ni vyake yeye Mwenyezi Mungu na hiyo ni tafsiri pana sana Mhe. Waziri.
>
> Mhe. Spika, jukumu hili tulilopewa la kusimamia ardhi tujue kwamba ardhi na mbingu mwenyewe ni *Allah*. Kwa hivyo, tutumie madaraka haya tuliyonayo na wadhifa na tuone kwamba tunawatendea haki hawa wananchi wetu ambao ndio tunaowategemea"

Mhe. Spika, naomba nieleze kwa nini nimeyanukuu maneno haya mazito ya Mhe. Salmin Awadh Salmin. Kamati yetu katika kuanza kazi yetu tulielezana kuwa tufanye kazi kwa uadilifu bila ya kumuonea mtu, bila ya chuki na bila ya kumpendelea mtu kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu. Tulitekeleza majukumu yetu ya msingi kama Mwenyezi Mungu alivyotujaalia.

Mhe. Spika, kamati Teule inazishukuru taasisi zote ikiwemo Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kutupatia nyaraka muhimu na nyeti, ambazo zimesaidia sana katika kufanikisha tofauti hii ya Kamati kwa nyaraka ambazo wameshindwa kuleta, imeonekana wameshindwa kuzipata hizo kwa mapungufu yaliyomo katika vyombo hivyo.

Sasa ni jukumu la serikali kulifanyia kazi suala hili na kulieleza Baraza wakati watakapokuja kutoa taarifa ya utekelezaji wa ripoti hii kwa upande wa Baraza la Wawakilishi. Kuna haja ya kuifanyia mapitio Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa ya Baraza la Wawakilishi, ili kuondoa mapungufu yaliyomo katika sheria hii na kuliwezesha Baraza na Kamati zake kutekeleza bila ya vikwazo vyovyote.

Mhe. Naibu Spika, hii Sheria ya Kinga nataka nitoe sio sheria ambayo iko Zanzibar. Mwaka 1993, Bunge la Jamuhuri ya Muungano liliunda Kamati ya Kuchunguza namna gani Zanzibar iliingia *OIC* kamati ya watu kama 12, ndani yake ilikuwa ina Wazanzibari wawili Wabunge. Kamati hii ikafanya kazi yake ya kuchunguza, kamati hii ikaripoti hivi:

> "Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi mmoja yaani kati ya tarehe 18 Machi, 1993 na tarehe 5 Februari, 1993 Kamati iliwaita mashahidi 25 na kuwahoji mashahidi 23, mashahidi wawili ambao ni raia wa Jamuhuri ya Muungano wanaoishi Tanzania Zanzibar walikataa kuitikia wito wa Kamati, tendo ambalo ni kosa la jinai chini ya Sheria Nam. 3 ya mwaka 1998"

Wakati wanafanya hitimisho ya ripoti yao walisema hivi:

> "Mhe. Naibu Spika, lililo baya zaidi ni mashahidi wawili muhimu sana katika suala hili nao ni Mhe. Taimur Saleh Juma na Mhe. Iddi Pandu Hassan, ambao walihusishwa moja kwa moja na suala la Zanzibar kujiunga na *OIC*, nao walikataa kufika mbele ya Kamati baada ya kutakiwa kufanya hivyo. Kitendo cha waungwana hao wawili kutofika ni kielelezo cha dharau kwa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Kamati yake. Kwa misingi hiyo Kamati inapendekeza rasmi kwamba Bunge liagize serikali ichukue hatua za kisheria zilizoainishwa katika Sheria Nam.3 1985 inayohusu Madaraka ya Kinga na Haki za Bunge"

Sasa hizi sheria ni *uniform* ziko kote. Jana Mhe. Salmin Awadh Salmin alisema kuhusu hatua, lakini kwa kweli hawa vijana nyaraka nyeti sana, nyaraka nzito sana wameleta. Kwa kweli tuliwapongeza. Kama nilivyosema natumai baadaye watayafanyia kazi kwa sababu si mengi sana ni mambo madogo madogo tu. Kwa hivyo nimeona niiseme hii Sheria ya Kinga yetu ya Zanzibar inatakiwa ifanyiwe marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengi waliochangia walitoa mapendekezo yao kutaka serikali kuifanyia kazi kwa dhati ripoti hii pamoja na migogoro mengine iliyotajwa na Wajumbe na ile ambayo haikutajwa. Kamati inatambua kuwa migogoro ya ardhi ipo mingi hapa Zanzibar. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya hawa Wajumbe wote.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndiyo ripoti yetu na nawaomba tena Wajumbe tuipitishe na nyote mlikubali, tufanye kazi naye Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati na *Inshallah* hamalizi kwa miaka mitatu na atakayekuja hamalizi, lakini kwa imani yangu mimi na Kamati yangu na nyinyi Wawakilishi kwa sifa mlizozitoa za Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati, ashirikiane na vijana wake asiwaondoe, Mkurugenzi abaki, Naibu Mkurugenzi, Katibu Mkuu, Maofisa, Mkurugenzi wa Ardhi na Upimaji, wote na wao tunawambia wafanye kazi kwa mujibu wa sheria, wasifanye kazi kwa maagizo, wafanye kazi kwa mujibu wa sheria.

Na Mhe. Waziri si mtu wa maagizo. Nakuombeni Wakurugenzi sisi tupo na nyinyi na Waziri mumsaidie, yaliyopita yamepita muanze ukurasa mpya.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka kumalizia kwa kufanya nukuu.

> "Mhe. Spika, napenda nisisitize tena Sera za Upemba na Uunguja si Sera ya Serikali yetu wala sio ya CCM. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kuwa serikali haitokuwa pamoja na kiongozi yeyote au afisa wa ngazi yoyote wa serikali anayefanya ubaguzi, sio tu katika kutoa nafasi za masomo bali hata katika kutoa huduma ambazo serikali imeziweka kwa ajili ya wananchi wote. Hivyo natoa tahadhari pia kuwa serikali haitomvumilia mtu yeyote atakayetoa taarifa za uongo, au kutoa madai ambayo hayapo katika wizara au taasisi ya serikali.
>
> Mhe. Spika, Wajumbe sote wa Baraza hili Tukufu lazima tuangalie kwanza mustakbali wa nchi yetu na maslahi ya wananchi wetu kuliko ubinafsi wetu. Maelezo ya michango yetu ndani ya Baraza hili Tukufu isaidie serikali yetu na ilenge katika kujenga nchi, wala isilenge kwenye imani ya itikadi za kisiasa za vyama vyetu. Kwa hivyo, tuepuke matamshi ya kupigiana vijembe vya chini kwa chini, na tuepuke kuponda serikali zote kutoka awamu ya kwanza mpaka ya leo. Vile vile, serikali ambayo Mzee Abeid Amani Karume ameanzisha Mapinduzi ya Zanzibar kwa dhana ya kuwa haikuleta maendeleo, Mapinduzi ndiyo yameleta maendeleo.
>
> Napenda ieleweke kuwa yale yote mazuri na mema yaliyofanywa na serikali ya awamu ya kwanza yatalindwa na kuheshimiwa na awamu zote. Aidha kukubali kuwa Mzee Karume ni baba wa taifa hili kwani alijitolea mchango wa maisha yake kuleta uhuru wa Visiwa vya Zanzibar.
>
> Mhe. Spika, sera ya Serikali ya awamu ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itashirikiana karibu zaidi na Serikali ya Muungano ya Tanzania na kuona kuwa maslahi ya Zanzibar kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, hayataathirika na kwamba faida ya kuunganisha soko la pamoja litapatikana. Lengo kubwa la ardhi kumilikiwa na serikali ni kumaliza uhasama wa miaka zaidi ya 300 ya kutawaliwa kwa nchi hii ambayo wananchi wanyonge na masikini hawakuweza kumiliki ardhi.
>
> Mhe. Spika, katika nchi yetu ardhi ni uti wa mgongo kwa kila maendeleo yetu. Napenda kutoa wito kwa taasisi zote za serikali

zinazoshughulikia ardhi kuwa waadilifu katika kutoa vibali vya utumiaji ardhi hasa wale maofisa wanaohusika wajiepushe na kupokea hongo. Tabia hii ya kupokea na kutoa hongo sio tu ni dhambi kwa Mwenyezi Mungu lakini ni adui mkubwa wa nafsi na ni uovu kwa jamii.

Nawaomba waheshimiwa Wawakilishi wote na wananchi kusaidiana na serikali katika kupiga vita uovu"

Haya ni maneno yaliyosemwa na Mhe. Dokta Gharib Bilal, alipokuwa anafunga Bajeti mwaka 1999 kwenye Baraza la Wawakilishi. Haya maneno nimeona niyaseme, niyanukuu kwa sababu suala la ardhi aliozungumza, umoja aliouzungumza na Uislamu unatufundisha tukumbushane. Ndio maana unaona asubuhi muadhini, Adhuhuri, Laasiri, Magharibi mpaka inamalizia Insha. Mtu anaweza akasali bila ya muadhini au unaweza ukasali rakaa 17, lakini kuna utaratibu rakaa mbili, nne, nne, tatu, nne. Sasa hata maisha yatu yanakwenda katika utaratibu.

Kwa hivyo, tumeshasema sana, tufuate utaratibu, tufuate sheria na tufanye kazi. Nimeona nitoe haya kwa sababu ni mambo ambayo yatasaidia kuweka mikakati. Jana wamesema hapa Mhe. Aboud Jumbe; Baraza kalianzisha, lakini haya aliyasema ndani ya Baraza hili na ni maneno muhimu sana na tuyafanyie kazi.
Mwisho kabisa naomba kumnukuu bwana James Madison kwenye *fade list paper no*. 51 ambaye alisema hivi:-

"Kama binaadamu angelikuwa malaika, kungekuwa hakuna haja ya kuwa na serikali. Kama malaika wangelipewa jukumu la kuwaongoza binaadamu, kungekuwa hakuna haja ya kuwa na udhibiti wa ndani wala wa nje kwenye serikali.Kwa hivyo, katika kutengeneza utaratibu wa serikali itakayoendeshwa na wanaadamu kuongozwa na wanaadamu wenzao, tatizo kubwa liliopo ni lazima kwanza tutengeneze utaratibu wa kuwezesha serikali kuwadhibiti wananchi inaowaongoza. Jambo la pili, kuilazimisha serikali kujidhibiti wenyewe. Hapana shaka udhibiti wa misingi ya juu ya serikali ni kuwatengea watu, lakini uzoefu umetufundisha binaadamu kwamba haja ya kuwepo tahadhari ya zaidi"

Nimeona nimalizie kwa haya na Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na niwashukuru Wajumbe wote. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunamshukuru Mwenyekiti wa Kamati teule na ametoa hoja. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale

walioikubali ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya kushughulikia mgogoro wa ardhi Zanzibar mwaka 2013 wanyooshe mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa kazi kubwa tuliyoanza jana na tumeimaliza leo. Kwenye *order paper* yetu inaeleza kuna kazi tumeiwacha ya Mhe. Hamza Hassan Juma kuwasilisha hoja yake, kwa kuwa kidogo bado ina marekebisho wanasheria wake, tumeamua hoja hiyo tuilete kesho asubuhi baada ya Maswali na Majibu. Sasa kwa kuwa muda wetu haujamalizika, tumuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais afanye utaratibu tuweze kuahirisha Baraza letu.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais: Kwa kuwa kutokana na orodha ya shughuli za leo zimemalizika, na kwa kuwa bado muda wa Baraza haujafikia. Naomba tuweke kanuni kando ya muda ili tuweze kuahirisha Baraza hili hadi kesho asubuhi saa 3:00.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyooshe mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe nimepewa taarifa na Mnadhimu wa Chama cha CUF kwamba Mheshimiwa mwenzetu amepata msiba amefiliwa na mama yake mzazi Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, nimeambiwa nikupeni taarifa hiyo. Na sisi kwa niaba ya Baraza tunampa pole na atakayejaaliwa kwenda mazikoni atoe taarifa Barazani ili tuweze kujua.

Baada ya maelezo hayo naakhirisha Kikao chetu hiki hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 19/12/2013 saa 3:00 asubuhi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Saa 12:55 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 19/12/2013 saa 3:00 asubuhi)